

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Saba – Tarehe 2 Februari, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 67

Ujenzi wa Ghorofa Jijini Dar es Salaam

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kumeibuka mtindo wa kujenga maghorofa mengi sana hasa katika Jiji la Dar es Salaam ambayo hayazingatii ubora na taratibu za mipangomiji:-

- (a) Je, ni Mamlaka gani inayosimamia ujenzi huo wa maghorofa katika jiji letu la Dar es Salaam?
- (b) Je, majiji hayo hayana Kanuni zinazosimamia ujenzi kwenye maeneo yake?
- (c) Je, ujenzi huo ambao utaongeza sana mahitaji ya huduma mbalimbali unazingatia huduma zilizopo au zilizopangwa kujengwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Miji, Manispaa na Majiji ndizo zenye jukumu la kupanga na kusimamia ujenzi wowote kwenye maeneo yao. Kwa mantiki hiyo, Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke ndizo zinazopanga na kusimamia ujenzi katika Jiji la Dar es Salaam. Mamlaka hizi, chini ya Sheria ya Mipangomiji, (*The Urban Planning Act, 2007*, Kifungu 7(1), 5(e)(i)(k) zina majukumu ya kiimipangomiji kama ifuatavyo; (1) Hupanga kanda mbalimbali za ujenzi zikiwemo kanda za ujenzi wa maghorofa. (2) Chini ya Kifungu 7(5)(m) waendelezaji binafsi wanaweza kupendekeza kwa Mamlaka aina ya ujenzi wanaoupendelea kwenye viwanja vyao na kisha Mamlaka hizo kuridhia au kukataa kutolewa kwa vibali vya ujenzi. (3) Mamlaka hizi zina jukumu la kusimamia ubora wa majengo yanayojengwa. Aidha, ujenzi wa maghorofa pia unao wadau wengine wanaosaidia kuona kuwa majengo yanayojengwa yanakidhi matakwa ya Sheria na kwamba majengo hayo yanakuwa salama. Wadau hao ni pamoja na Bodi ya Usanifu na Ujenzi, Bodi ya Wakandarasi na Bodi ya Wahandisi.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi mijini unasimamiwa na Kanuni (*The Urban Development Control Regulations, 2008*) zilizotolewa kupitia Gazeti la Serikali GN 242. Kanuni hizi zinaelekeza aina ya ujenzi unapaswa kufanywa kwenye viwanja vya ukubwa na matumizi tofauti, ujazo wa majengo kwenye viwanja hivyo na hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa ili kitolewe kibali cha ujenzi. Baada ya Manispaa kutoa kibali cha ujenzi, Mjenzi katika hatua mbalimbali za ujenzi hupaswa kutoa taarifa kwa Manispaa husika ili ujenzi huo ukaguliwe kabla ya kuendelea na hatua nyingine. Vilevile, Manispaa zina watumishi ambao hufuatilia shughuli za ujenzi, kubaini wanaokiuka Kanuni na kuwachukulia hatua, wakati mwingine hata kubomoa ujenzi uliofanywa bila kufuata taratibu.

(c) Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yanahitaji kuandaliwa mipango mipya ya uendelezaji yaani (*Redevelopment Schemes*) ili kuhuisha hali ya maendeleo na huduma zinazohitajika. Kila Halmashauri ya Manispaa ina mipango ya uendelezaji upya ili kuendana na hali ya maendeleo iliyofikiwa. Kwa mfano, Manispaa ya Kinondoni ipo katika hatua ya ukamilishaji wa kuandaa mpango mpya wa uendelezaji wa eneo la *Oysterbay* na Masaki. Maeneo mengine yaliyo katika mchakato huu ni Magomeni na Mwananyamala. Mipango hii mipya itawezesha kuhuisha uendelezaji huu mpya pamoja na mahitaji ya huduma muhimu. Mipango hii mipya ya uendelezaji itaainisha viwango vya majengo, idadi ya ghorofa na kupendekeza kiwango cha huduma na miundombinu inayohitajika.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Nina swali moja tu la nyongeza, kwa kuwa ujenzi wa majengo mengi Jijini Dar es Salaam haukwenda katika utaratibu mzuri na haupendezi na kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam ni kioo cha nchi hii je, Serikali inatoa utaratibu gani wa kudumu kwa majiji mengine ambayo yanazidi kuendelea hapa nchini hivi sasa ili yasije yakaingia katika utaratibu huu mbovu wa ujenzi wa kiholela na miji yetu iweze kupendeza kama miji mingine duniani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Cynthia Ngoye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi naomba nikiri kwamba huyo anayeuliza swali hili ni Mamlaka nakumbuka alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Lakini sasa hivi ndiye Mwenyekiti wa *NEMC* na kwa hiyo jambo analoli-address hapa ni jambo ambalo nina hakika kwamba analifahamu.

Kwa hiyo, nataka nikiri hapa kwamba Mheshimiwa Mbunge Cynthia Hilda Ngoye anajielekeza katika eneo ambalo limetuletea matatizo makubwa sana katika nchi yetu, nikisema hapa nipuuze swali hili utakumbuka kule Temeke kuna ghorofa liliwahi kuanguka kwa sababu ya mazingira hayahaya yanayozungumzwa hapa na ndiyo maana naomba kwa niaba ya Serikali nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Cynthia Ngoye ambaye amekuwa anafuatilia hata mabango kule Jijini Dar es Salaam yanayowekwa hovyohovyoye na ninataka niseme hapa kwamba nafikiri anachotaka mimi ni kutoa maelekezo hapa.

Nimesoma Sheria hapa na jana hapa mmemsikia Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu amepitisha hapa utaratibu ambao sisi wote tumeukubali tunasema kwamba utaanza kutumika na tumeiona busara ya Wabunge iliyotumika humu ndani, Wabunge ambao wana uzoefu katika haya maeneo ambayo tuliyapitisha jana wenzetu wote waliozungumza hapa wametusaikia sana.

Sasa natoa maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kutoa maelekezo kwa Halmashauri zote na hapa sizungumzii Dar es Salaam tu bali na Mwanza na Dodoma na wale walioko Mbeya na Arusha na majiji mengine na miji mingine ifuate Sheria hizi ambazo zimepitishwa na taifa na ambazo Bunge hili limeshapitisha, vinginevyo hatutasita kuchukua hatua madhubuti kwa wale wote ambao wataonekana kwamba wamekiuka utaratibu huu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maelezo ya ziada, karibu!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kuongeza majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri katika swali la Mheshimiwa Hilda Ngoya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi miji yetu karibu yote karibu 70% ni squatter wamejenga holeholela kwa hiyo haipendezi. Kwa hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji ambazo ndizo kwa kweli zina jukumu hilo kama alivyosema Naibu Waziri kwa tunashirikiana kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, ni kuongeza upimaji wa viwanja mijini, pale Wizarani tuna mfuko wa kuzikopesha Halmashauri za miji kupima viwanja na mfuko ule ni wa kuzunguka, wakikopesha wakirudisha wanakopa wengine, zile Halmashauri ambazo zimekopa na zimeshapwa viwanja warudishe ili tukopeshe wengine ili kasi ya kupima viwanja iwe kubwa tuondoe haya ma-squatter ambayo hayapendezi mijini.

Tumeanzia utaratibu wa kujenga miji midogo midogo kandokando ya miji mikubwa, tumeanzia na Dar es Salaam tunaita *Satellite Cities* kupanga vizuri kama pake kuna maeneo matano tumeanzia na Luguruni tumeshapata viwanja tayari ule mji utakuwa mzuri na utakuwa na huduma zote ili kwa taratibu tuanze kupendezesha jiji la Dar es Salaam kwa pembeni kule ambako kumechafuliwachafuliwa kuwe kuzuri zaidi na miji mingine tutakwenda Mbeya, Mwanza, Arusha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Swali la nyongeza fupi tu ili tupate uzoefu wa Mheshimiwa Charles Keenja.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo hili ni kubwa na kwa kuwa kwa kweli miji yetu yote imevurugika kabisa, je Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuanza kwa kuandaa master plan za kila mji na kusimamia utekelezaji wake badala ya kuziachia Serikali za Mitaa ambazo hazina uwezo wa kutatua matatizo haya?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha mle ndani tumetaja miji ambayo kwa mwaka huu wa fedha Wizara yangu na miji hiyo tunashirikiana kufanya master plan na mwaka ujao wa fedha kwa sababu Wizara yangu imeingizwa katika Wizara ambazo zitapata kipaumbele cha bajeti tutapanua wigo, tatizo ni kubwa kweli tumekuwa tunaweka fedha kidogo kwenye Wizara yangu na hata kwenye miji yenyewe pesa za mipangomiji pesa zimekuwa ni finyu sana.

Kuanzia mwaka ujao wa fedha Serikali imekubali kwamba sasa itaongeza fedha katika Wizara yangu na vilevile katika Halmashauri za Wilaya ili kazi hii sasa ya kuweka master plans na kupima miji yetu na kujenga kisawasawa iweze ikashika kasi. (*Makofi*)

Na. 68

Madhara Yanayotokana na Ongezeko la Joto la Jua

MHE. JACKSON M. MAKWETTA aliuliza:-

Kwa kuwa, madhara ya ongezeko la joto la jua ni makubwa kupitia hata madhara ya UKIMWI:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha kampeni ya kuelimisha Watanzania juu ya madhara hayo ili waweze kuchukua hatua?

(b) Je, kauli ya “Kilimo Kwanza” inazingatia madhara ya ongezeko la joto?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti wa Kisayansi umeonyesha dhahiri kwamba kumekuwa na ongezeko la joto duniani katika miaka ya karibuni. Tatizo la kupanda kwa joto duniani linasababishwa na ongezeko kubwa la gesijoto duniani zitokanazo na dhughuli mbali mbali za kiuchumihasa katika nchi zilizoendea na hivyo kuleta mabadiliko ya Tabianchi. Athari za mabadiliko ya tabianchi ni kuongezeka kwa majanga kama ukame na mafuriko ya mara kwa mara, kama tunavyoshuhudia katika sehemu mbalimbali za nchi yetu na duniani kwa ujumla.

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikiwaelimisha wananchi kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na masuala mengine ya Mazingira kwa njia mbalimbali. Elimu hii hutolewa kwa njia ya vipindi vya redio na televisheni, magazeti matamko ya Serikali, majarida, vitabu, vipeperushi, hotuba, Elimu mashuleni na kwa wadau wanaotembelea mabanda yetu ya maonyesho katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kauli mbiu ya “Kilimo Kwanza” suala la kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika kilimo limezingatiwa katika msingi mkuu wa kilimo na ufugaji endelevu. Uzingatiji huo unaonekana katika msingi namba (viii) wa kutunmia Sayansi na Teknolojia za kisasa za kilimo na ufugaji (suala la kudhibiti wadudu waharibifu na suala za kupanda kulingana na misimu na hali ya ukame); msingi namba (ix) unaolenga kuweka miundombinu ya kilimo (suala la kuongeza kilimo cha umwagiliaji) na misingi mingine inayolenga kuweka mbinu mbadala za kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Aidha, kwa kuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ina Kitengo cha Mazingira na zaidi ya 90% ya Halmashauri zimetoea ama kuajiri maafisa mazingira kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (Sura 191), tunategemea kwamba utekelezaji wa Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza utawashirikisha Wataalamu hawa ili kuhakikisha kwamba suala la mazingira ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi linazingatiwa. Kaulimbiu ya Kilimo kwanza ni kilimo cha tija siyo kilimo cha kuvuruga ardhi yote kwa kukata miti au kulima milimani ili kupanua mashamba.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa maneno sawa, lakini kwa vitendo mambo si sawa kwa sababu bado ng’ombe wanatembea nchi nzima, kilimo cha kuhamahama bado kinaendelea na moto kichaa unaendelea, kwa hiyo gharika kuu inakuja tujenge safina.

Kwa kufuatana na uchambuzi wa Kisayansi wa mabingwa wa mazingira duniani wanasema kwamba ifikapo mwaka 2010 50% ya uzalishaji chakula katika Bara la Afrika utapungua na 40% ya Bara la Afrika itakuwa jangwa.

Kwa kuzingatia hali hii na hatua ambazo hazilingani na uzito wa tatizo je, Waziri anakubali kwamba hivi vipeperushi, vitabu na matangazo haya yangefikishwa kwenye vijiji na kwa kila kijiji na mji katika Tanzania ili Elimu hii iweze kuwafikia watu wengine zaidi?

Kwa kuwa, hali hii ya mazingira bado haiieleweki na ndiyo maana nimelinganisha uzito wa tatizo na UKIMWI, kwa kuwa suala la mazingira inaonekana kwamba haiieleweki yaani ni suala la watu wachache walio na nuru ya kisomi zaidi.

Je, isingekuwa vizuri tuunde Kamati za Ukaguzi ambazo zitatoa taarifa ya hali ya mazingira kila mwaka kwa nchi nzima kusudi tuwe tunajua hali inavyowekwenda?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Jackson Makwetta kwa jinsi alivyokuwa mwanamazingira na mhamasishaji mkubwa sana, Mheshimiwa Jackson Makwetta alizungumzia kwa uchungu mkubwa matatizo ya mazingira na mimi nikampa changamoto ya kuja na mikakati ama ushauri ambao utaweza kutusaidia kwa kweli nakiri kwamba Mheshimiwa Jackson Makwetta ametengeneza waraka huu ambao unaitwa Gharika Kubwa inakuja. Waraka huu nimeupitia nimeupitia na nimeona kwa kweli ni jinsi gani alivyoweza kuzama kwa kina kwa lugha nyepesi kabisa na tutaupitia sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais ili tuweze kuongeza na baadhi ya mambo mengine tuweze tukavisambaza kama alivyoshauri katika swali lake kusambaza na kutoa Elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikutana juzi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma katika kuwahamasisha hasa ukizingatia kwamba leo ni siku ya Ardhi Oevu Duniani, wanafunzi wa Chuo Kikuu walisema safari kiongozi atakayekuja kuomba kura bila kuzungumzia masuala ya mazingira hatutamuelewa.

Kwa hiyo, mimi nasema kwa hali hii Mzee wangu Jackson Makwetta ulivyoanza ni mtaji mzuri na siyo tu kwamba unatishia kwa kusema Gharika Kubwa Linakuja, ni kweli kuna waraka huu umetolewa na waraka huu unaonyesha kwamba ifikapo mwaka 2070 kijana wa miaka 50 ataonekana wa miaka 85, maji ambayo sasa hivi tunaweza kunywa hata glasi 8 kwa siku ambazo tunatakiwa tonywe basi ifikapo mwaka 2070 nusu glasi ndiyo itapatikana, vifaa na silaha za maangamizi zitatumika kwa ajili ya kuweza kunyang'anya na kutafuta maji. Tukiishi katika hali hii ya business as usual kuendelea na utaratibu huu tunaoendelea nao tutafika huko tunapokusudia.

Kwa hiyo, mimi nakubali Kamati za Mazingira ni muhimu lakini tunazo Kamati za mazingira katika Wilaya kulingana na Sheria tuliyounda, Waheshimiwa Wabunge waraka huu

utatusaidia ili uwe ni ngao na sisi Wabunge kuona wajibu wetu kama Wabunge wa kusimamia Kamati hizi zifanye kazi katika ngazi ya Wilaya na katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nadhani majibu yanatosheleza, naomba tu hizi nyaraka mbili tuweze kugawiwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Tunahamia sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii swali linaulizwa na Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole.

Na. 69

Usimamizi wa Hali ya Mazingira Nchini

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI aliuliza:-

- (a) Je, usimamizi wa Mazingira nchini ukoje?
- (b) Je, Serikali inatumia njia gani ya kutoa elimu ya kutunza mazingira kwenye vijiji ambavyo redio hazisikiki wala machapisho na vipeperushi haviwafikii?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani juu yakuwapa zawadi wananchi wanaofanya juhudi kubwa ya kutunza mazingira?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ya mwaka 2004 imeweka muundo wa kitaasisi ambao unaeleza wajibu wa kila mmoja katika shughuli za utunzaji wa mazingira kwa ngazi ya Kitongoji/kijiji/mtaa hadi Taifa. Sheria inaelekeza wazi kila Wilaya kuwa na Kamati ya Mazingira na kuwa na Mratibu wa Mazingira. Aidha, kila Sekta ina Mratibu wa Mazingira. Tayari Wakaguzi wa Mazingira 21 na 90% ya Waratibu wa Mazingira wa Halmashauri wameteuliwa au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuna program na mikakati mbalimbali inayolenga katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira nchini kwa mfano, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa, Programu ya Hifadhi ya Bonde la Ziwa Tanganyika, Program ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Mkaa kutokana na Ukataji Miti Hovyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) au *Reduction of Emission from Forest Degradation*. Aidha, yapo Mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya Kiserikali, vyombo vya habari na vikundi mbalimbali vya jamii wamekuwa wakishiriki kikamilifu katika kutoa elimu ya Hifadhi ya Mazingira kupitia redio, magazeti, luninga, vipeperushi na machapisho mbalimbali. Kwa maeneo ambayo vipeperushi na machapisho

hayafiki wala redio hazisikiki elimu ya mazingira huwafikia wananchi hao kupitia Kamati za Mazingira za vijiji kwa baadhi ya meneo na hupitia katika *program* za elimu kwa umma na mashuleni. Mkakati ulioponi kuwezesha Kamati za Mazingira za vijiji ziweze kufanya kazi zake kwa kzingatia Sheria. Kwa kushirikiana na *RED CROSS* tumeweza kuendesha semina kwa walimu kuhusu hifadhi ya mazingira kwa baadhi ya maeneo. Lakini vilevile kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu tumetoa tayari semina kwa Walimu zaidi ya 80 na tunategemea uwe ni mkakati wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imekamilisha maandalizi ya Tuzo ya Rais ya Kutunza Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Tuzo hii itaanza kutolewa mwaka 2010 wakati wa kilele cha Siku ya Mazingira Duniani na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuzo hii itahusisha kaya, vijiji, Wilaya, asasi na taasisi za Serikali, Taasisi zisizokuwa za Serikali na sekta binafsi. Tuzo inatarajiwa kuongeza ufahamu wa wananchi katika umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) inashindanisha Shule za Msingi na Sekondari kuandika insha kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, kwa kushirikiana na *WWF* na *Care International* tumeanzisha mpango wa malipo/motisha kwa jamii zinazotunza maeneo ya hifadhi za vyanzo vya maji katika milima ya Uluguru na matarajio yetu mpango huu utasambaa nchi nzima. Wenzetu wa *WWF* watakuwepo leo mchana ili kuongea na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Mazingira kuhusu mkakati huu wa kutoa tuzo kwa wanaohifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

Vilevile, ili kupunguza kasi ya matukio ya moto katika misitu ya nyika, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi ya Vyanzo vya Maji umeelekeza kila Wilaya kutoa zawadi kwa mtu au kikundi kitakachotoa taarifa za matukio ya moto na kushiriki katika kuzima moto huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Waheshimiwa Madiwani pamoja na uongozi wa Wilaya katika ngazi zote kuhamasisha na kuelimisha wananchi wote kwa ujumla kuhusu fidia za kiuchumi na kijamii zitokanazo na utunzaji wa Mazingira katika maeneo yao kwa faida yetu na ya vizazi vijavyo.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, moja kati ya makundi 6 makubwa ya athari za mazingira ni utowekaji wa mapori na upunguaji wa maliasili yaliyomo. Je, Serikali inachukua hatua gani katika kukabiliana na changamoto hii?

Kwa kuwa, ongezeko la idadi ya watu nchi limekuwa ni tatizo kubwa linalochangia uharibifu wa mazingira na kwa kuwa tatizo hili halijapewa uzito unaostahili. Je, serikali inasema nini juu ya tatizo hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakar Shamis Faki ,Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kabisa kumekuwa na utowekaji mkubwa wa mapori na uchomaji wa misitu na hasa kwa kisingizio kwamba kuna sasa hivi Kilimo Kwanza watu wanapanua mashamba. Sisi kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Waziri Mkuu lakini vilevile Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika tunaendelea kutoa Elimu kwa wenzetu kuhakikisha kwamba suala hili linakoma.

Lakini vilevile kupitia mkakati niliousema wa kuangalia masuala mazima ya uchomaji wa misitu na utunzaji wa mazingira tunaweka motisha katika vijiji ambavyo vitaanza kupanda miti katika maeneo yaliyokatwa miti pamoja na kutunza uoto wa asili kutakuwa na mkakati wa kuweza kuwapa motisha ili wasifanye tena shughuli zile ambazo zilikuwa zinaleta uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, suala zima la utunzaji wa mazingira na uchomaji wa moto misituni suala zito na kuna Sheria sasa hivi tunasema kwamba sisi sote tuwe wasimamizi wa hii Sheria, Sheria iko katika lugha ya Kiswahili tumesema tutazigawanya vijiji vyetu vyote vipate lakini na sisi Waheshimiwa Wabunge tutaletewa tena nakala ili Sheria hii ya Kiswahili iweze ikapatikana na ikatusaidia katika kuhamasisha na kutoa Elimu kwa wapiga kura wetu.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge mazingira tumeyazungunza robo saa sasa naomba tuendeleo kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na swali linaulizwa na Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe.

Na. 70

**Utendaji Mbovu wa Bohari ya Dawa (Medical Stores
Department (MSD)**

MHE. MARIAM R. KASEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa kwa kipindi kirefu kumekuwa na malalamiko makubwa juu ya utendaji mbovu wa *MSD*:-

Je, hadi sasa Serikali imechukua hatua katika kuishauri na kuisimamia *MSD* ili iweze kutoa huduma bora kwa wakati kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuisimamia Bohari ya Dawa ili kuboresha utoaji wa huduma. Hatua hizo ni pamoja na kuiwezesha Bohari ya Dawa kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa miaka sita hadi kufikia mwaka 2013.

Mpango huo unalenga kuimarisha utendaji na tija ili kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma, kurekebisha mfumo wa kompyuta ili kuboresha mfumo wa ugavi na mawasiliano na wateja, kujenga uwezo wa raslimali watu na kusogeza huduma karibu na wateja kwa kuongeza uwezo wa Bohari za Kanda kuhifadhi bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Bohari ya dawa imeongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi kutoka asilimia 60 hadi 80.

Aidha, imeongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa kutoka mita za mraba 27,250 mwaka 2007/2008 hadi kufikia 36,559, mwaka 2008/2009 kwa kujenga maghala makubwa mawili katika Bohari za Kanda za Moshi na Iringa. Bohari ya dawa inatarajia kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa kwa kujenga maghala katika kanda za Mbeya, Mtwara, Tabora Makao na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya ukuaji wa mahitaji ya maghala, Bohari ya Dawa imeanzisha mikataba ya muda maalum na wazabuni ijulikanayo kama *framework contracts*. Aidha, inaandaa utaratibu wa kuwataka wazabuni kufikisha bidhaa moja kwa moja kwenye bohari za kanda badala ya mfumo wa sasa wa kupokea bidhaa zote Makao Makuu, Dar es Salaam. Lengo la utaratibu huo ni kufikisha huduma karibu na wateja wake.

Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imeanzisha mfumo unaojulikana kama *total quality management system*. Mfumo huo unaweka vigezo maalum vya kuhakiki ubora wa bidhaa na utoaji wa huduma. Mfumo wa Kompyuta umefanyiwa tathimini kwa lengo la kuuboresha ili kukidhi mabadiliko ya mfumo wa ugavi kutoka makasha (*kits*) kwenda mfumo wa ugavi kulingana na mahitaji (*integrated logistics system (ILS)*).

Mheshimiwa Spika, Bohari ya dawa imekasimu madaraka zaidi kwa bohari za kanda ili kuimarisha mfumo wa usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Aidha, imeandaa utaratibu wa kukutana na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Waganga wafawidhi wa Hospitali na Wafamasia wa Wilaya na Mikoa ili kupata maoni ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake. (*Makofi*)

MHE. MARIAM R.KASEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na maelezo marefu sana ambayo yanaleta angalau matumaini ninataka kujua kwa kuwa; Serikali imeongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kutoka asilimia Sitini (60%) hadi asilimia themanini (80%) na huduma hii katika Mkoa wa Mtwara hospitali zetu hasa ya Mkomaindo Wilaya ya Masasi, bado kuna malalamiko makubwa ya kukosa vifaa vyenye ubora na madawa

ya kutosha hivyo kupelekea wagonjwa wanapoenda kupata matibabu kukosa huduma ya vipimo na madawa kuelekezwa wakanunue kwenye maduka ya madawa.

Je, ni lini huduma hii itapatikana kwa asilimia mia moja (100%) ili kuwaondolea wananchi hawa adha hii wanayoipata wanapoenda kupata huduma hizi?

Kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba, Serikali imeandaa utaratibu wa kukutana na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Waganga Wafawidhi na Wafamasia.

Je, ni lini utaratibu huu utanza ili watakapokuwa wanakutana kuhakikisha kwamba, taratibu zilizopangwa zinafuatwa na wananchi wanapata huduma iliyo bora?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, majibu. Leo Waheshimiwa mna maswali ya nyongeza marefu sana, sijui mnaweza kupunguza kidogo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kasembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kasembe kwa kufuatilia masuala ya dawa hasa kwa wananchi wake wa Mtwara. Kama nilivyosema, tulivyojipanga ni kwamba, dawa zitapatikana na ndiyo maana tumesema kwamba, tuna Kamati mbalimbali na mikakati mbalimbali kama nilivyoitaja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vyenye ubora na ambavyo havina ubora ambavyo vinapatikana kule Mkomaindo na Mtwara kwa ujumla; Mimi nashauri tu kwamba, iwapo itatokea vifaa ambavyo wanachukua vinaonekana kama havina ubora, tunaomba tafadhali watupatie taarifa haraka sana ili tuweze kufuatilia tatizo limetokea wapi.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoiliza, wale wataalamu wa ngazi zote watakutana mara moja kwa sababu nia ya kukutana kwetu ni kwamba, tatizo linaloonekana hapa sasa hivi ni kwamba, hata kama mpango huo tuliouweka dawa zitakuwa zinafika katika Makao Makuu ya Wilaya, bado kuna tatizo kubwa sana ambalo linatokea kwamba, usambazaji wa dawa kutoka Wilaya au Makao Makuu kwenda katika vijiji hivyo tutakapokuwa tumezungumza na hawa watendaji wa ngazi zote tukishirikisha na Halmashauri tutahakikisha kwamba, hizi dawa zinawafikia kwa wakati na kwa maana hiyo hata ule utambuzi wa matatizo ambayo yanatokea vikiwemo vipimo vinaweza kupatikana kwa wakati zaidi ili kuweza kuwahudumia wananchi.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati yako ya *LAAC* inazunguka nchi nzima, inapitia vitabu vya Halmashauri zote, inakagua hata hospitali zenyewe na mara nyingi malalamiko makubwa ni dawa hazipo, fedha zinazopelekwa na Serikali moja kwa moja *MSD*, *MSD* haipeleki

taarifa Wilayani na fedha hizo zinazobaki katika akaunti ni nyingi sana na wananchi wanakosa madawa.

Je, Serikali iko tayari kufikiria sasa kwa vile imekiri kwamba, inatimiza asilimia themanini (80%) tu, asilimia angalau hizo ishirini basi zipelekwe moja kwa moja kwa Wilaya ili wao waweze kujinunulia dawa na vifaa popote pale zinapokatikana badala ya kungojea *MSD*? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Kaimu Mkuu wa kambi ya Upinzania, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba saa nyingine unakuta pesa inayopelekwa *MSD* inakuwa inabaki pale na kwa sababu hiyo unakuta wengine wanakosa zile dawa, lakini kama mnakumbuka tulizungumza tulipokuwa tunatoa Bajeti yetu ya afya, kwamba tunaangalia utaratibu wa kuweza kuona kama tunaweza kuchukua baadhi ya pesa tukapeleka katika halmashauri zetu. Lakini tulichokuwa tunakifuatilia ni kuweza kuona kwamba, ni jinsi gani zile fedha zitaweza kudhibitiwa kule katika Halmashauri kwa sababu tulikuwa tunaogopa kwamba, tukipeleka pesa kule na akaunti nyingi ambazo ziko kule inawezekana ule usimamizi wenyewe ukaonekana kwamba fedha nyingine zitapotea.

Mheshimiwa Spika, kama anavyosema mwenyewe kwamba, vitabu vinakaguliwa na katika hospitali na baadhi imeonekana kwamba, kuna matatizo ya kifedha. Kwa hiyo, bado tunaliangalia hili tuweze kuona, lakini nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni utaratibu mzuri mbali ya zile fedha ambazo ziko katika mifuko mingine tukiwapelekea hizo wanaweza wakanunua dawa au vifaa ambavyo vinakosekana.

Na. 71

Hati Punguzo ya Chandarua kwa Akina Mama Wajawazito

MHE. MTUTURA A. MTUTURA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeazimia kupambana na ugonjwa wa malaria; na kwa kuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wakati akihitimisha hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2008/2009 alitangazia Taifa kuwa Hati punguzo ya chandarua kwa akina mama wajawazito ni Tsh. 500/= (mia tano) badala ya Tsh 3500/=.

Je, Serikali imetekeleza agizo hilo kwa kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Hati Punguzo ulioanzishwa mwaka 2004 kwa lengo la kumpunguzia gharama mama mjamzito ili aweze kupata chandarua kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa malaria kwa kuongezea kiasi kidogo cha fedha. Kutokana na sababu za uhuru wa soko, fedha ya nyongeza ambayo mama mjamzito anatakiwa kuongeza ili kupata chandarua imekuwa ikitofautiana katika sehemu tofauti za nchi, huku ikiongezeka kulingana na umbali wa kutoka Dar es Salaam, kwa kisingizio cha ongezeko la gharama ya usafiri. Katika baadhi ya maeneo, hasa vijijini kiwango cha fedha za nyongeza kilifikia sh. 3,000/= kwa chandarua kimoja. Kutokana na gharama hii kuwa kubwa baadhi ya wajawazito hawakuweza kupata vyandarua kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutambua tatizo nililolitaja hapo juu, kuanzia mwezi Oktoba, 2009 Wizara imeanzisha mpango wa Hati Punguzo mpya. Kupitia Mpango huu mama mjamzito anatakiwa kuongeza kiasi cha sh. 500/= tu ili aweze kupata chandarua chenye dawa ya kudumu (*long lasting insecticide treated net*) mahali popote alipo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2009 mafunzo ya uhamasishaji yametolewa kwa watoa huduma nchi nzima ikiwa ni pamoja na kugawa Hati Punguzo mpya. Hadi kufikia Desemba, 2009 jumla ya vyandarua 10,083 viligaiwa kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Tunaendelea kuwahimiza akina mama wajawazito kuhudhuria kliniki ili waweze kupata Hati Punguzo. Kama nilivyokwisha tangulia kusema hapo juu, mama mjamzito anatakiwa kuongeza sh. 500/= ili aweze kupata chandarua chenye dawa ya kudumu katika wakala yeyote wa Hati Punguzo mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, ni maarufuku kwa Wakala yeyote kumtoa mjamzito zaidi ya sh. 500/= kwani kwa kufanya hivyo anavunja taratibu na makubaliano na uwakala wake unaweza kusitishwa.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tamko la Hati Punguzo kuwa shilingi 500/= kutoka shilingi 3,500 ambazo ndiyo msingi wa swali lilitolewa mwezi *August*, 2008 lakini utekelezaji wake umefanywa mwezi Oktoba, 2009 kipindi hiki ni takribani miezi 15.

Je, Serikali inatwambia nini, kwanini utekelezaji wa tamko hili umechelewa kwa kiasi hicho kikubwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kipindi cha miezi 15 ni kipindi kikubwa sana na kwa kuwa uchumi wa wananchi wa Tanzania bado uko chini, naamini katika kipindi hicho akina mama wengi wajawazito wamepoteza maisha kwa matatizo ya malaria.

Je, Waziri atakuwa tayari kutoa rambirambi za jumla kwa Watanzania waliopoteza maisha kwa kuchelewa kwa Wizara hii kutekeleza tamko hili?, Serikali inaaahidi nini ili jambo kama hili...

SPIKA: Hilo liache litakuwa la tatu sasa, mawili yanatosha. (*Kicheko*)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Ahsante Mheshimiwa Spika.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nimesema kwamba, Serikali imekuwa ikifuatilia na ilipoliona hili tatizo ikawa ilikaa na kuzungumza na kufanya uhamasishaji ili kuweza kuona kwamba, akina mama wanapata neti kwa shilingi 500?=. Kwa hiyo, siyo kwamba tulikuwa tumechelewa, tumeliona hili tatizo na tukalifanyiakazi na ndiyo maana tulipoona tulikaa na watu wakapewa mafunzo ya uhamasishaji ili kuwa na mpango wa Hati Punguzi mpya.

Kwa hiyo, nilitaka tu niseme kuwa, hatukuwa tumezembea kwani baada ya kuliona lile tatizo tulifuatilia na nikasema kwamba watu walikuwa wanatoza viwango hivyo kwa visingizio, kwa hiyo tulifanya utafiti na sisi tukaona kwamba, kweli kulikuwa na makosa yanafanyika lakini siyo kwamba tulikuwa tumeacha na hatukuwa tunatenda, tulikuwa tunaendelea na utendaji wa kuhakikisha kwamba, mambo yanakwenda sawa,.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili; nakubali kabisa kwamba, akina mama wamepoteza maisha, lakini siwezi nikasema kwamba, moja kwa moja katika kipindi hiki akina mama wamepoteza maisha kwa sababu ya kukosa hivi vyandarua. Ninaamini kabisa kwamba, hata kama kuna waliokuwa wamepata matatizo walikuwa wamelipwa, kwa sababu kutotumia chandarua cha Hati Punguzo sio sababu kuu inayosababisha vifo vya akina mama. Lakini hata hivyo, kwa wale ambao kwa namna moja au nyingine labda wamekwazika katika zoezi hili basi Serikali inapenda kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi zake na kwamba, sisi kama Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba, vyandarua vinatolewa kwa Hati Punguzo na yeyote atakayekiuka atachukuliwa hatua mara moja, ahsante sana.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, baada ya jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, ambalo linamtoa nyoka pangoni nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nionavyo mimi chandarua sio suluhisho pekee kwa sababu wakati mwingi sisi wenye nyumba, mtu na mkewe na wanawe wanakaa ukumbuni, wanakaa kwenye meza ya kula, wanazungumza. Je, hawa ambao wakati wa kulala bado utawalazimisha walale au watakapokuwa huko watafanya nini, nini suluhisho? (Makofi/kicheko)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa na ninafurahi kwamba na Mheshimiwa Haroub ananiunga mkono kwamba, chandarua peke yake siyo suluhisho.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokuwa tunazungumza hapa ndani ya Bunge lako Tukufu, tulikuwa tunazungumzaia kuweza kuona ni utaratibu gani utakaotuwzesha kutokemeza malaria na katika kutomeza malaria mojawapo ya njia ni kutumia vyandarua. Lakini pia

tunazungumzia usafi wa mazingira, pia Serikali inaenda mbele zaidi kuweza kuona ni jinsi gani tutaanzisha mpango wa kunyunyizia dawa katika nyumba ili kuua mbu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado tunaendelea kutoa elimu kwa sababu, suala la kuua mbu siyo la suala la Serikali, tunatoa elimu kwa wananchi ili waweze kuweka mazingira yao katika hali ya usafi, kufunika madimbwi na vile vitu ambavyo vinaweza vikasababisha mazalia ya mbu ambao hatimaye wanaweza wakaambukiza ugonjwa wa malaria.

Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwakumbusha ndugu zangu wananchi kuweza kuendelea kuweka mazingira ya usafi katika nyumba na kufunika madimbwi yote ili kuhakikisha mbu hawazaliani lakini na wakati huo na sisi Serikali tunajipanga kama itawezekana tuweze kufanya unyunyizaji ili kuua vimelea wa mbu. Lakini vilevile kuzuia mbu wasiweze kuingia ndani na kumng'ata mtu, ahsante. (*Makofi*)

Na. 72

Kuutambulisha Mlima Kilimanjaro kwa Watalii

MHE. BASIL P. MRAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa, ni kweli usiopingika kuwa Mlima Kilimanjaro upo Tanzania, Wilaya za Rombo, Longido, Hai, Siha, na Moshi Vijijini na kwa kuwa watalii bado hawana ufahamu wa kutosha kuhusu mlima huo:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi kuzunguka mlima huo ili kuhakikisha kuwa Watalii wanalala na kutembelea maeneo husika kwa wingi zaidi?
- (b) Je, Serikali kupitia *TANAPA* na *KINAPA* ina mpango gani na mkakati gani kuongeza shughuli za kitalii kwenye maeneo hayo? na
- (c) Je, ni lini Serikali kupitia Wizara husika itazipatia Halmashauri zinazopakana na mlima huo mgao mkubwa zaidi wa mapato halisi yatokanayo na utalii na hifadhi za mlima Kilimanjaro?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, swali lake lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wageni wanafahamu uwepo wa Mlima Kilimanjaro nchini Tanzania na hivyo kutembelea kwa wingi, Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

Imekuwa ikitumia kauli mbiu ya Tanzania: *The Land of Kilimanjaro, Serengeti and Zanzibar* ambayo inatambulisha vivutio vikuu vya utalii vya Tanzania, ukiwemo Mlima Kilimanjaro. Kuongeza jitihada za kutangaza utalii wetu na vivutio vyake kwa:-

(a) Kuongeza Bajeti Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) ya kutangaza utalii kutoka Tsh. 3.4 bn mwaka 2005 hadi Tshs. 7.63bn mwaka 2008.

(b) Kushiriki maonesho ya utalii sehemu mbalimbali duniani ambapo mwaka 2008 Tanzania ilishiriki maonesho 22 na mwaka 2009 maonesho 18 yakiwemo ya Indaba (*RSA*), *ITB* (Ujerumani), *WTM* (UK), *BIT* (Italy) na *FUTUR* (Hispania) .

(c) Matangazo yamekuwa yakioneshwa kwenye vyombo vya habari vikuu duniani kama *CNN* (*International* na *Domestic*), *WABC TV New York*, *Epic Global Media* (Waliotengeneza *DVD* inayooneshwa *CNBC TV* na *National Geographic Channel*)

(d) Kuchapisha matangazo kwenye majarida ya kimataifa kama *US Travel Agent* (nakala 100,000 mwaka 2009), *Africa Travel UK* (mwaka huo huo nakala 60,000) na *China Business week* (nakala 200,000 mwaka 2009).

Mheshimiwa Spika, jitihada zingine ni pamoja na zifuatazo:-

Kwa kushirikiana na wadau wa Sekta binafsi, Wizara na Mashirika yake imekuwa ikiratibu ziara za wageni maarufu duniani na misafara ya vyombo vya habari vya kimataifa. *TV* zinazopiga filamu za Korea, Japan, Canada, Australia na Spain zilitembelea na kupanda Mlima Kilimanjaro mwaka 2009 kwa lengo la kupiga picha na kuweza kuzionesha huko kwao.

Jitihada hizi zimeongeza idadi ya wageni wanaotembelea Tanzania na mapato kutoka 612,756 (US\$ 823.05) mwaka 2005 hadi 770,376 (US\$ 1,269 bn) mwaka 2008. Kati ya wageni hao, wageni 42,000 walitembelea Kilimanjaro.

Kwa upande wa malazi, Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*), liliweka kwenye mpango wake wa miaka 5 (2005-2010) kuongeza idadi ya vitanda kufikia 1,333 kutoka 500 mwaka 2005 kwa kutenga maeneo mapya 23 kwa ajili ya uwekezaji wa mabanda na *Lodge* za kulala wageni.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kujibu kipengele (b), Bodi ya Utalii Tanzania, *TTB* kwa kushirikiana na Idara ya Utalii ya Wizara, imekuwa ikiendesha utalii wa kupanda mlima kama shughuli kuu za utalii Mlimani Kilimanjaro. Hata hivyo, ili kuongeza shughuli za utalii na kufanya wageni wakae muda mrefu katika eneo hilo, *TTB* na Idara ya Utalii imeanzisha utalii wa Utamaaduni (*cultural tourism*) ambapo vikundi 5 kwa mkoa wa Kilimanjaro vimeanzishwa na vikundi katika Wilaya 30 kitaifa vimekwishakuanzishwa. Aidha, Idara inafikiria na kufanyia Utafiti uanzishwaji wa shughuli zingine za utalii wa michezo kama *Kili Marathon* ili kuongeza wigo wa utalii wa Kilimanjaro.

(c) Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifashi la Taifa (*TANAPA*) ambalo ni shirika la umma la kitaifa limekuwa likichangia shughuli za maendeleo kwa wilaya zote zinazozunguka

Mlima Kilimanjaro kupitia mpango wake wa ujirani mwema. Kupitia mpango huu, shirika limechangia jumla ya Tsh. 649, 235,459/= kwa wilaya za Moshi, Rombo, Hai, Moshi Vijijini na Longido kati ya mwaka 2005 na 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa shirika hili ni la kitaifa, *TANAPA* limekuwa pia likilipa kodi Serikali Kuu ambapo mwaka 2009 jumla ya Tsh. 6.6 bn. zililipwa kama *VAT* na *Corporate income Tax*.

Mchango wa *KINAPA* kwa Kilimanjaro na maeneo jirani na Mlima huo ni zaidi ya fedha zinazotolewa kupitia ujirani mwema, bali pia unapatikana kupitia:-

- Ⓟ Uchumi jumla wa Mkoa wa Kilimanjaro ambapo uwepo wa hifadhi hiyo huchangia 40%, ambayo ni takribani Tshs. 40 bilioni kwa mwaka.
- Ⓟ Hali ya hewa nzuri inayoruhusu kustawi kwa mazao kama Kahawa na Migomba.
- Ⓟ Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ndicho chanzo pekee cha maji kwa miji ya Rombo, Marangu, Moshi na miji mingine kandokando ya mlima. Pia mlima huu ni chanzo cha mito mingi inayopeleka maji Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo ni chanzo cha nishati kwa taifa letu na sehemu kubwa ya shughuli za uvuvi kwa ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kwa kuzingatia kilio cha Waheshimiwa Wabunge, *TANAPA* sasa imeanza mchakato wa kupitia upya utaratibu wa kuchangia miradi kupitia ujirani mwema ili kupata njia bora zaidi ya kusaidia jamii jirani, Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa jibu refu lakini lenye habari nyingi za kufanyia kazi. Pili niishukuru Serikali kwa kufanya jambo la msingi kuzunguka mlima Kilimanjaro, nalo ni uamuzi wa kujenga barabara ya lami kuzunguka mlima ili hata watu wasioweza kupanda mlima kupitia Marangu au kule Rombo wazunguke tu mlima kujionea mandhari na kuona mlima wenyewe pindi wakiendesha magari yao, au pikipiki au hata baiskeli.

Je, Wizara haioni kwamba, kinachohitajika sasa ni *Tourism Development Master Plan*, mpango kabambe wa kuendeleza utalii kuzunguka mlima Kilimanjaro, jambo ambalo halipo. Je, Serikali iko tayari kupokea wazo hilo na kulifanyiakazi na kutushirikisha sisi ambao tunaweza tukatoa mawazo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Basil Pesambli Mramba, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana kwa wazo lake ambalo kimsingi Wizara inakubaliana nalo kabisa. Kwa sasa hivi Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*) baada ya mpango wao wa miaka mitano kuwa umemalizika mwaka huu 2010, sasa hivi wameanza tena

mpango mwingine wa miaka mitano unaojumuisha *component* ya utalii, lakini kwa kuzingatia uzito wa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie tu kwamba, Wizara itashirikiana na wenyeji wa eneo hili na watu wengine wenye uzoefu katika sekta ya utalii ili kuweza kuwa na mpango kabambe utakaoleta manufaa kwa taifa na hasa kwa wananchi wa eneo hilo. (*Makofi*)

MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, nami niungane na Mheshimiwa Basil Mramba, kumpongeza Waziri na Serikali kwa ujumla.

Kutokana na swali la msingi na kipengele (b) kinachoulizia Serikali kupitia *TANAPA* ina mpango na mkakati gani kuongeza shughuli za kitalii kwenye maeneo haya. Ningependa nimwulize Mheshimiwa Waziri, kwamba kutokana na ahadi inayotekelezwa sasa ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kwasaadala kwenda Masama ambayo pia nayo inatufikisha katika vilele vya Mlima Kilimanjaro;

Je, sasa Serikali imeishajiandaa vipi kwa kuitumia hii barabara ili kuongeza kipato cha taifa na kipato cha wale wananchi wa Masama?

SPIKA: Sina hakika kama hii barabara ni ya utalii hasa, nadhani inaunganisha sehemu moja hadi nyingine, lakini Naibu Waziri amesimama pengine ana jibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu pendekezo la nyongeza la Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ombi la kuongeza njia za kupandia mlima limekuwa likijitokeza mara kwa mara na kwenye Bunge la Bajeti lililopita swali hili lilijitokeza na Mheshimiwa Waziri alikwenda Marangu, kwenda kuona njia iliyokuwa ikipendekezwa ya Maua lakini katika ziara yake hiyo mwezi Septemba, mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwamba, *TANAPA* na Serikali kwa ujumla sasa hivi wanafanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kuongeza njia zingine, kwa maana hiyo jambo hili tunalo, utafiti unafanyika na baada ya utafiti kukamilika tutaweza kusema ni wapi ambapo kiikolojia na kiuchumi panafaa kuanzishwa njia nyingine.

Na. 73

Serikali kutoa taarifa sahihi ya Pesa za Mfuko wa Wajasiriamali

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inatakiwa kutoa taarifa sahihi kwa Bunge juu ya Fedha za J.K. kwa ajili ya mikopo ya Wajasiriamali kwa kuwa ni fedha za walipa kodi kama zilivyo fedha nyingine:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuliambia Bunge hili fedha za J.K. kwa ajili ya Mikopo ya Wajasiriamali inapatikana katika fungu lipi au Bajeti ya Wizara gani?

(b) Je, ni lini Ofisi ya Mkaguzi itakagua fedha hizo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Kigoma, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Shilingi bilioni 21 zinazojulikana kama Mabilioni ya J.K. ambazo ziliidhinishwa na Serikali kuwawezesha wananchi kiuchumi unasimamiwa na Benki Kuu kama wakala wa Serikali chini ya makubaliano na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mpango huu unatekelezwa kaatika awamu mbili; kila moja ikihusisha shilingi bilioni 10.50 Katika kutekeleza mpango huu, Benki Kuu iliingia Mkataba na Benki za *NMB* na *CRDB* kwa mfumo wa udhamini na awamu ya pili ilihusisha taasisi ndogondogo za fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na mkataba kati ya Benki Kuu na mabanki ya *CRDB* na *NMB*, benki hizi zilipewa dhamana ya shilingi bilioni 5.25 kila moja kutoka Benki Kuu kwa udhamini wa Serikali na benki hizi kutumia fedha zao kukopesha mara tatu ya kiasi cha udhamini huo.

Hivyo, mikopo iliyotolewa kwa wajasiriamali ilizidi kiwango cha bilioni moja kwa kila Mkoa na kwa maana hiyo kuweza kuwafikia wananchi wengi. Kwa utaratibu huo, hakukuwa na fedha kutoka kwenye Bajeti ya Serikali wala fungu la Wizara yeyote.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mikopo hii ilitolewa na mabanki kwa kutumia Fedha zao wenyewe, ukaguzi wa akaunti ya mikopo hiyo kwenye mabanki hayo unafanyika kwa utaratibu ambao benki hizo hutumia wakaguzi wao wenyewe walioidhinishwa na kuorodheshwa Benki Kuu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, atakagua endapo kutakuwa na madai ya malipo ya fidia chini ya udhamini uliotolewa na Serikali.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa *NMB* na *CRDB* ni *private* na hazikaguliwi na *CAG*, na kwa kuwa udhamini wa *BOT* maana yake ni udhamini wa Serikali kwa kodi za wananchi.

Je, Bunge hili linapataje taarifa kamili iwapo waliokopa wameshindwa kulipa mikopo hiyo na zitatoka fungu lipi, kwa kuwa hazikupitishwa na Bunge ingawa udhamini huo wa shilingi bilioni 10.5 umetolewa na Serikali?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yapo malalamiko kuwa pesa hizo hazikuwafikia walengwa na vilevile Serikali imesema imeweka udhamini, kwa maana hiyo Serikali inao uwezo wa kupata taarifa kamili juu ya wananchi wangapi wamepata pesa hizo na taasisi zipi au SACCOS ngapi zimepata pesa hizo, ili kuondoa malalamiko yaliyojengeka kwamba, pesa hizo zimetumiwa na wajanja na walengwa ambao walikuwa wajasiriamali wadogo wadogo hawakupata pesa hizi? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):

Mheshimiwa Spika, mpango huu ulipoanza kuandaliwa mwaka 2006 lakini mikopo ikaanza kutolewa mwanzoni mwa mwaka 2007 mmoja ya masharti ya Serikali kupitia Benki Kuu ilikuwa kwamba akaunti maalum za fedha hizi zifunguliwe kwenye Benki ya CRDB na vile vile kwenye NMB na jambo hilo lilifanyika na akaunti hizi mbili moja ambayo iko *Bank House* kwa NMB na nyingine ambayo iko Azikiwe kwa CRDB zinasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kwa hiyo, tayari Serikali inapata taarifa kamili za mwenendo wa akaunti hii. Lakini la pili, Benki Kuu na Serikali yenyewe huwa inazitaka hizi Benki mbili kutoa taarifa za mara kwa mara na ikiwa Waheshimiwa Wabunge wanahitaji taarifa hizi basi ziko tayari na tunaweza kuzileta pale ambako zitahitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malalamiko ya kuwa fedha hizi hazikuwafikia walengwa, hiyo naomba niseme siyo kweli. Tunazo taarifa kamili za ni nani alipewa mikopo hii ambayo bado inaendelea.

Lakini naomba niseme hivi kwa Waheshimiwa Wabunge kudhani kwamba kila mmoja wetu anaweza kugema tembo tutakuwa tunakosea. Ni sawa sawa na kusema kila Mtanzania anayekwenda kuomba anaweza kuwa mjasiriamali si kweli. Ndiyo sababu tunasema hizi fedha zilikuwa hazitolewi sio kama za kugawa, ilikuwa mikopo isipokuwa Serikali ilichofanya hapa ni kwamba mikopo hii iwafikie wale wananchi ambao wanaendesha biashara ndogo ndogo ama uzalishaji mdogo mdogo kwa masharti nafuu na masharti hayo yalikuwa ni pamoja na kutokutozwa ada za kuomba mikopo ni pamoja na kiwango cha riba kisizidi asilimia 10. Hilo ndilo Serikali ilichofanya.

Kwa hiyo wazo la kwamba hazikuwafikia walengwa si sahihi na mimi nitaomba wakati utakapofika sisi tutaleta kwa Waheshimiwa Wabunge mchanganuo ni nani alipewa fedha hizi na ni nani hakupata isipokuwa hatutawapa majina. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda niongezee jibu zuri alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi kama ifuatavyo hasa kuhusu tathmini ya namna *impact* ya mfuko huu ulivyo kwa nchi nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Rais ambaye ndiye aliyetoa fedha hizi au ndio mfuko wake. Ma-RAS wote nchi nzima wameagizwa kuleta tathmini kupitia kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zetu kuona ni jinsi gani fedha hizi ziliwafikia watu, nani alipata akiwa ni eneo gani alifanya nini amefaidika vipi na hali ikoje. Kwa sasa Wizara yangu pamoja na Ikulu tunaratibu majibu haya kutoka kwa RAS katika nchi nzima.

Ningependa nichukue nafasi hii kwa wale wachache ambao hawajaleta kutoka Mikoani walete taarifa hizo Ikulu na nakala kwetu kama ambavyo wengine wamefanya na baada ya hapa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kushirikiana na Ofisi ya Rais itakwenda huko kuhakikisha jinsi ambavyo majibu haya kweli yalivyo sahihi kwa maana ya kuona *impact* ya mfuko huu. Hii ni kuwezesha sasa Rais na Serikali kwa ujumla kuona kwamba je kulikuwa na kasoro gani ili Rais akiamua kwamba utaratibu huu uendelee katika awamu ya pili turekebishe nini na kitu gani kilikuwa hakijakaa sawa sawa. Lakini majibu tunayopata mpaka sasa ni kwamba *impact* ni nzuri na wananchi wamefaidika sana, lakini taarifa tutakuja kuileta rasmi baadaye. (*Makofi*)

Na. 74

Ufuatiliaji wa Viwanda na Rasilimali Zilizobinafsishwa

MHE. MARIA I. HEWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeanza kufuatilia viwanda na rasilimali zilizobinafsishwa ili kubaini wawekezaji walioshindwa kuendeleza viwanda hivyo ili wanyang'anywe:-

Je, Serikali ipo tayari kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa mpango huo?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye Hotuba yangu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, uperembaji wa Makampuni na Viwanda vilivyobinafsishwa chini ya sekta ya viwanda, biashara na masoko ulikuwa umekamilika kwa Kanda ya Mashariki inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, zoezi la uperembaji katika Kanda zilizobakia pia umekamilika.

Mheshimiwa Spika, uperembaji umebainisha kuwa kuna Makampuni na viwanda 22 vilivyowekeza zaidi ya kiwango kilichoahidiwa kwenye Mikataba ya Mauzo na viwanda 15 vimewekeza chini ya kiwango wakati viwanda 13 viliwekeza ingawaje Mikataba ya Mauzo haikuwa na vipengele vya uwekezaji. Baadhi ya viwanda hivi ni vile vilivyobinafsishwa kupitia ufilisi.

Aidha, zoezi hilo lilibainisha kuwa Makampuni saba (7) yaliyobinafsishwa kwa wafanyakazi na menejimenti (*Management and Employee Buy-Out (MEBO)*) hayakuwekeza na Mikataba ya Mauzo haikuwa na masharti ya kuwekeza kwa vile mengi hayakununua mali zisizoondosheka na yanajishughulisha na biashara (*trading*).

Pia, zoezi la uperembaji lilibainisha kuwa Makampuni na viwanda saba (7) vimebadilisha shughuli za awali. Makampuni na viwanda 29 vimefungwa. Viwanda 15 kati ya 29 vilivyofungwa viko chini ya sekta ya viwanda, biashara na masoko na viwanda 14 viko chini

ya sekta za maendeleo ya mifugo na uvuvi; maliasili na utalii na nishati na madini. Kwa upande wa ulipaji wa fedha za manunuzi, ilibainika kuwa Makampuni na viwanda 21 bado havijakamilisha ulipaji wa fedha za manunuzi kwa mujibu wa Mikataba ya Mauzo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa zoezi hilo, Waraka wa Baraza la Mawaziri wa kuwasilisha mapendekezo ya hatua za kuchukua kulingana na mambo yaliyobainishwa unaandaliwa na utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa maamuzi. Taarifa kamili ya hatua za kuchukua dhidi ya wale ambao hawajatekeleza mikataba ya mauzo itawasilishwa katika Bunge hili mara mapendekezo husika yatakaporidhiwa na Baraza la Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wavute subira hadi maamuzi yakapotolewa na Baraza la Mawaziri ambapo yatawasilishwa Bungeni hapa. (*Makofi*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nisimame tena. Kwanza niombe tu kutoa pongezi zangu kubwa kwa Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri alilolitoa lenye kujaa takwimu na mara nyingi jibu lenye takwimu huwa lina mwelekeo wa kuwa la uhakika, naomba tu nimwulize swali moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake la msingi ametumia neno uperembaji naomba kuuliza katika kuperemba huku Kiwanda cha *Nyanza Glass* kilichoko Mwanza kiko katika kundi lipi katika viwanda hivi kwa sababu Kiwanda hiki ni cha siku nyingi na kiko pale muda mrefu na hakifanyi kazi tangu kianzishwe, lakini kuna kila sababu ya ku-*operate*. Lakini mpaka sasa ni kimya. Je, Waziri anasema nini kuhusu Kiwanda hiki?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali lake naomba nishukuru sana kwa pongezi zake alizotupa na sisi tutajitahidi kuendelea kufanya kazi kwa nguvu zote ili kuwahudumia Watanzania. Kuhusu swali lake dogo kwamba *Nyanza Glass* iko wapi. *Nyanza Glass* itakuwa katika viwanda ambavyo vimeuzwa na havijashughulikiwa. Kwa hiyo, kama nilivyoahidi kwenye jibu langu la msingi na ambalo amelikubali kwamba baada ya Baraza la Mawaziri kuridhia ripoti hii tutaleta ripoti hii Bungeni kwa kuelezea kiwanda hadi kiwanda na nini hatua ya kuchukuliwa ili tuweze kudumisha na kuimarisha uchumi wa nchi yetu kupitia sekta ya viwanda.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa baadhi ya wanunuzi hawa wamekiuka mikataba ya makubaliano na hivyo kusababisha hasara kwa Taifa kwa mfano aliyenunua Kiwanda cha *TWICO Arusha* kilichokuwa kinatumika kwa ajili ya kuchakata nyara za Serikali amebadilisha na kukifanya ni karakana ya kutengeneza Mabodi ya magari na hivyo mpaka sasa hivi kuna tatizo kubwa sana kwamba ngozi zinasafirishwa zikiwa hazijachakatwa.

Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kumiliki kiwanda hiki ambacho taarifa tunaisubiri ni kuliletea hasara kwa Taifa na hivyo ni utaratibu gani unafanyika sasa kuhakikisha kwamba wale wote waliokiuka makubaliano ya mikataba mara moja wanarejesha viwanda hivyo ili kazi iendelee kama kawaida?

WAZIRI WA VIWANDA, BIAASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, niane kwa kumpongeza Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Maria Hewa kwa kuwa wamekereketwa sana na shughuli ya sekta za viwanda. Kwa ajili hiyo kama nilivyoahidi nitajitahidi sana kuona yale yanayotakiwa kwa kweli yanafanywa. (*Makofi*)

Sasa kuhusu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba, je, ni nini kitafanyika kwa wale ambao watakuwa wamekiuka mikataba ya uuzaji kwa kutokufanya zile shughuli ambazo ziko kwenye mikataba. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba baada ya kupeleka ripoti hii kwenye Baraza la Mawaziri na nina hakika tutaamua ni hatua zipo ambazo zitachukuliwa na ambazo zitakuwa na tija kwa Taifa letu. Tutalielezea Bunge lako Tukufu hatua madhubuti ambazo tutazichukua. Lakini ningependa kuchukua nafasi hii kwa wale wote ambao wamenunua viwanda na makampuni ambayo yalikuwa chini ya Mashirika na kwa kujua mikataba ambayo wameingia na Serikali ningependa sasa waone kwamba wanafanya yale yanayotakiwa ama kwa vyote vyote vile tunachukua hatua ya kuvichukua na kuvipeleka kwa wale ambao wanaweza wakawekeza na kwa manufaa ya Taifa letu.

Na. 75

Uimarishaji wa Sekta ya Mifugo

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005 imebainisha kuwa Sekta ya Mifugo itapewa kipaumbele kwa kuwasaidia wafugaji kufuga kisasa na kuvutia Viwanda vya Usindikaji wa Nyama:-

Je, hadi sasa Serikali imeweka mazingira gani na Uwekezaji wa Viwanda vya Usindikaji Nyama ukoje?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambayo inatoa mwongozo sahihi wa kusimamia na kuratibu shughuli za sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali zinazosimamia shughuli za sekta ya mifugo. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Nyama Na. 10

ya mwaka 2006, iliyoanzisha Bodi ya Nyama ambayo inaratibu na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji na usindikaji wa nyama hapa nchini. Aidha, Wizara inasimamia Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008, Sheria ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003 na Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003.

Vile vile, Bunge lako Tukufu lilipitisha “*Financial Leasing Act Cap 5*” ya mwaka 2008 ili kuwawezesha wawekezaji kupata mikopo kwa kutumia rasilimali mbalimbali na hivyo kuwezesha upatikanaji wa mitaji. Upatikanaji wa mikopo utaongeza kasi ya uwekezaji na uendeshaji wa shughuli za ufugaji na ujenzi wa machinjio/viwanda vya kusindika nyama.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuhamasisha uundaji wa vikundi vya wadau wa sekta ndogo ya nyama vikiwemo vile vya wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo na nyama. Aidha, vyama viwili vya wadau vimeanzishwa katika ngazi ya Kitaifa ambavyo ni *Tanzania Livestock and Meat Traders Association (TALIMETA)* na *Tanzania Meat Processors Association (TAMEPA)*.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapatia wafugaji soko la uhakika ndani na nje ya nchi, Wizara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindika nyama na uhamasishaji huu umewawezesha wawekezaji kutoka sekta binafsi kujenga machinjio/viwanda vya kisasa vya kusindika nyama.

Machinjio hizo ni pamoja na *Tanzania Meat* (Dodoma), *Sumbawanga Agricultural and Animal Food Industry* (SAAFI (Rukwa), *Tanzania Pride Meat* (Mvomero, Morogoro) ambazo zina uwezo wa kuchinja kati ya ng’ombe 150 – 200 kila kimoja kwa siku. Aidha, Wizara imetoa kiasi cha Tshs. bilioni 3.5 kwa ajili ya ujenzi wa machinjio kubwa katika ranchi ya Ruvu itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng’ombe 800 na mbuzi/kondoo 400 kwa siku itakapokamilika mwaka 2011.

Viwanda vingine ni vya kuchinja kuku vya *Mkuza Chicks Ltd.* (Pwani, *Interchick*) (Dar es Salaam na *Tanzania Pride Meat* (Mvomero) ambavyo vina uwezo wa kuchinja wastani wa kuku 9,000 kila kimoja kwa siku.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta hii muhimu.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Lakini pia ningependa kumshukuru Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa.

Tunafahamu kwamba katika nyama za ng’ombe tulizonazo Tanzania, *Kongwa Beef* ni *Grade One*. Hatuna kiwanda cha kati wala kidogo pale Kongwa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa ambayo ndiyo *centre* ambapo tungekuwa na Kiwanda cha namna hiyo tungepata nyama hiyo kutoka ng’ombe wa maeneo ya Gairo, Mpwapwa, Dodoma Vijijini, Kiteto, Kongwa yenyewe na ranchi ya Kongwa.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na kupatikana na kiwanda cha uwezo wa kati katika maeneo hayo kwa sababu uwekezaji wake ni ghali kidogo. Angalia tu machinjio ya Ruvu shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya machinjio peke yake, Serikali itatusaidiaje?

Lakini la pili, ngozi zetu ambazo tumekuwa tukizalisha wafugaji zina ubora duni sana. Lakini tukipata uwezesho wa vifaa husika tunaweza tukawa na ngozi ambazo badala ya kwamba tunaziua wastani wa shilingi 2,000 hivi sasa tukauza mpaka shilingi 20,000 kwa ngozi moja. Je, Serikali nayo inasemaje kuhusu kuwawezesha wafugaji ili kuweza kuboresha aina ya ngozi ambazo wanaziua kuwa na ubora wa hali ya juu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa namna anavyofuatilia suala la mifugo hapa nchini.

Mara baada ya kuteuliwa Naibu Waziri mwaka 2008 alinifuata na tukaenda naye ranchi ya Kongwa ambapo tulikwenda tukakagua ile ranchi na akaniambia matatizo ambayo walikuwa wanakabiliana na wananchi wanaozunguka ile ranchi na tuliweza kuyatatua na sasa hivi kuna uhusiano mzuri sana kati ya wananchi wa Kongwa na ranchi ya Kongwa. (*Makofi*)

Sasa kujenga kiwanda cha machinjio pale Kibaigwa. Machinjio madogo tunaweza kuweka Kongwa na wakachinja na watu wakaweza kuzipatia huduma tena huduma nzuri zaidi kuliko sasa.

Lakini kwa kiwango cha kiwanda ni lazima tukumbuke kwamba hapa Dodoma kuna machinjio ya Dodoma ambayo kiwanda hicho kilijengwa na Serikali na baadae kukabidhiwa na *NARCO* na *NICO* kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 200 kwa siku lakini hadi sasa kina uwezo wa kuchinja tu ng'ombe 70 kwa siku. Kwa hiyo badala ya kuweka tena kiwanda kingine kule Kongwa ambacho kiwanda kitajengwa na Serikali kuna umuhimu wa kuimarisha hiki cha Dodoma.

Kwa hiyo ninachotoa wito ni kwamba wananchi wa Kongwa na wanaozunguka hapa Dodoma waweze kutumia machinjio yaliyopo ambayo ni makubwa tena yanaweza kutimiza matakwa yote ya wananchi wanaokizunguka. Kwa hiyo Bucha ndogo pale tutaomba *NARCO* itaiweka pale lakini kwa kiwanda tutaomba wananchi waweze kutumia hiki kiwanda chetu cha Dodoma ambacho ni kikubwa na kina uwezo na cha kisasa kabisa.

Kuhusu ngozi ni kweli kumekuwepo na matatizo ya ngozi wananchi kuchuna vibaya ngozi wengine hata wafugaji wanatumia vyombo vya moto kuweka alama kuhakikisha kwamba ng'ombe wao wanatambulika. Tunalifahamu hilo na ambacho tumefanya tumeanzisha Kitengo cha Ngozi sasa Kitengo cha Ngozi hizo kimepita katika Wilaya tofauti kuhamasisha Halmashauri tofauti kuwahasisha wananchi.

Kwanza kabisa mwaka jana tulitoa kila Halmashauri 55 tuliweza kuipatia shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuboresha ngozi, lakini vile vile, katika hizo Halmashauri tumeshatoa visu ambavyo wananchi watatumia wakati wanachuna ngozi.

Lakini vile vile tuna ofisa ambaye tumempa pikipiki ambayo atazunguka katika eneo la Halmashauri na kuhakikisha kwamba wale wanaochinja wanawapatia elimu wale wanaochuna ngozi namna ya kuhakikisha kwamba ngozi inayochunwa inachunwa vizuri.

Lakini vile vile tunachosema ni kwamba mwaka jana tumeumia sana watu wa ngozi. Kilichotokea ni kwamba ngozi ilishuka bei kufuatana na mtikisiko wa uchumi duniani na tunachofanya sasa ni kuhamasisha wananchi kusindika ngozi na kuhakikisha kwamba ngozi yote inayosindikwa hapa nchini ili tuweze kutengeneza vitu kama viatu, mikoba na kuongeza thamani ya ngozi.

Na. 76

Takwimu Sahihi za Mifugo na Samaki Nchini

MHE. HEMED MOHAMED HEMED aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi anapojibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu Taasisi yake hutoa takwimu za mifugo ambazo hutofautiana siku hadi siku hali ambayo inatia wasiwasi katika usahihi wa takwimu hizo:-

- (a) Je, Serikali iko tayari sasa kutupa takwimu sahihi za mifugo na samaki hapa nchini?
- (b) Je, takwimu hizo zinatokana na sensa ya mwaka gani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na ya Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu za mifugo na samaki na mazao yake zinazotolewa na Serikali kwa nyakati tofauti kwa Waheshimiwa Wabunge na umma kwa ujumla ni sahihi kulingana na mifumo mbalimbali inayotumika kukusanya takwimu husika ambayo ni pamoja na sensa, ukaguzi na tafiti mbalimbali.

Kwa upande wa sekta ya mifugo takwimu hupatikana kutokana na sensa kamili na sensa ya sampuli. Sensa kamili ya mwisho ya mifugo ilifanyika mwaka 1984 ambapo idadi ya mifugo ilikuwa ng'ombe 12,500,000, mbuzi 6,400,000, kondoo 3,100,000 na nguruwe 280,000.

Sensa hiyo ilifuatiwa na sensa ya sampuli ya sekta ya kilimo ikijumuisha mifugo iliyofanyika mwaka 2002/2003 kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Takwimu (*National Bureau of Statistics*) ambapo idadi ya ng'ombe ilikuwa 16,836,217, mbuzi 11,756,527 na kondoo 3,945,266. Sensa hiyo ya sampuli ilifanyika katika vijiji 3,500 vya Tanzania Bara.

Sensa nyingine ya sampuli iliyofanyika mwaka 2007/2008 na Makadirio ya idadi ya mifugo yanafanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2003/2004 hadi mwaka 2008/2009. Kutokana na sensa hiyo ya sampuli, idadi ya mifugo kwa mwaka 2007/2008 ilikuwa ng'ombe 18,800,000, mbuzi 13,500,000 na kondoo 3,600,000. Katika mwaka 2008/2009 idadi ya ng'ombe ilikuwa 19,100,000, mbuzi 13,600,000 na kondoo 3,600,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya uvuvi, takwimu zinazotolewa na Serikali hutokana na tafiti mbalimbali zinazofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Nchini (*TAFIRI*) pamoja na savei (*frame and catch assessment surveys*) zinazofanywa na Idara ya Uvuvi.

Kwa mfano, utafiti iliyofanyika katika Ziwa Victoria mwezi Agosti, 2008 ulibaini kuwepo kwa sangara tani 227,365, daga tani 742,289 na furu na samaki wengine tani 518,359, ambapo mwezi Agosti 2009 kulikuwa na sangara tani 307,539, daga tani 786,653 na furu na samaki wengine tani 489,220.

Pia, utafiti uliofanyika kwenye Bahari ya Hindi mwaka 2004 ulibaini kuwepo kwa kambamiti tani 114.64, ikilinganishwa na tani 1,076.8 mwaka 2009. Idadi ya kambamiti iliongezeka kutokana na Serikali kusitisha uvuvi wa rasilimali hii Februari, 2008 kwa wavuvi wakubwa.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swala moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Pwani ya Tanzania kuanzia visiwa vya Unguja, Pemba, Mafia na fukwe zake kuna samaki ambaye kwa muda mrefu sasa hivi kwa kiasi kikubwa ametoweka na walikuwepo wengi sana aina ya pomboo na samaki huyo ana faida kubwa sana kwa binadamu kwa sababu ni rafiki kwa binadamu na mara nyingi sana wavuvi wanapozama samaki huyu huwa anaokoa binadamu.

Kutokana na sifa za samaki huyu mara nyingi haliwi wala havuliwi, lakini sasa hivi ametoweka.

Je, TAFIRI imefanya utafiti samaki huyu amekwenda wapi au kwa kiasi wametoweka kwa nini. Je, hizi meli zinazovua katika Pwani ya Tanzania ambazo mnazipa vibali mna uhakika gani kama samaki hawa hawaibiwi wakati meli nyingi ya meli hizi zinauza samaki moja kwa moja nje hazileti Pwani ya Tanzania? Muwe mnafanya uchunguzi huo.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa kazi ya TAFIRI ni kufanya utafiti na pale ambapo samaki anakaribia kutoweka huwa tunaweka utaratibu kwamba watu wasiwavue. Sasa kufuatana na samaki ulioniuliza ni kweli nikiri kwamba mimi huyu samaki simfahamu, na ni vizuri Mheshimiwa

nikakiri badala ya kujibu kitu ambacho nikatoa taarifa ambayo ni ya uongo. Lakini ni kwamba kama samaki huyo anatoweka nina hakika kwamba Wizara na Idara ya Uvuvi itakuwa imeweka utaratibu kwamba wasivuliwe na yoyote yule atakayepatikana kwamba anamvua lazima atachukuliwa hatua kali kufuatana na Sheria Na. 22 ya mwaka 2003 na kanuni za mwaka 2005 ambazo tunazirekebisha sasa.

Na. 77

Mikoa Inayoongoza Kwa Kilimo cha Mpunga

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Mpunga ni muhimu sana hapa nchini kwa ajili ya kupata mchele:-

- (a) Je, ni Mikoa ipi inayoongoza kwa kilimo cha Mpunga na kwa wastani wa tani ngapi kwa mwaka?
- (b) Je, Tanzania inazalisha tani ngapi za mchele kwa mwaka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Ogessa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mikoa inayoongoza kwa kilimo cha mpunga hapa nchini ni Mbeya, Morogoro, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Mikoa hii kwa pamoja huzalisha karibu asilimia 66 ya mpunga wote unaozalishwa nchini kwa mwaka. Uzalishaji wa wastani kwa mwaka kwa kila mkoa ni kama ifuatavyo:- Mbeya tani 202,313; Morogoro tani 151,000, Tabora tani 130,230; Shinyanga, tani 130,156 na Mwanza tani 110,807.
- (b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita (1998/99 – 2008/2009) Tanzania imekuwa ikizalisha wastani wa tani 717,417 za mchele kwa mwaka. Katika msimu wa 2008/2009 uzalishaji ulikuwa tani 885,614.
- (c) Kwa wastani Mkoa wa Shinyanga unazalisha tani 130,156 za mchele kwa mwaka. Kiasi hiki ni sawa na wastani wa asilimia 11.796 ya mchele wote uliozalishwa hapa nchini na hivyo mkoa huo unachukua nafasi ya nne katika uzalishaji wa nafaka hiyo.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru majibu ya Serikali yenye takwimu sahihi. Lakini nina maswali madogo ya nyongeza. Miaka ya 1970 Serikali kupitia *National Milling Corporation* kwa kuzingatia uzalishaji wa mchele wa Mkoa wa Shinyanga ilijenga kinu cha kukoboa mpunga pale

Shinyanga mjini. Lakini ni miaka karibu 30 kiwanda hicho hakifanyi kazi. Je, ni nani mmiliki na nini matumizi ya kiwanda hicho na miondombinu yake haieleweki?

Pili, kwa kuwa mchele ni chakula kikuu kwa Watanzania walio wengi kwa nini Serikali haijumuishi mchele katika hifadhi ya chakula ambapo utunzaji wa mchele na hususan mpunga ni rahisi zaidi kuliko hata utunzaji wa mahindi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vinu ambavyo vipo Shinyanga ambavyo vilikuwa vinamilikiwa na *National Milling* pamoja na vinu vingine vilivyopo maeneo mengine kama Arusha na Iringa vinu hivi vyote vitafanyiwa ukaguzi na kuonekana vile ambavyo vinafaa vitatumiwa na Bodi ya Vifaa Mchanganyiko kwa ajili ya kuhifadhi nafaka ili viweze kufanya kazi zilezile zilizokuwa zinafanywa na National Milling.

Kuhusu mpunga kuwekwa kwenye Hifadhi ya Taifa hilo ni wazo zuri na inategemea uzalishaji. Kwa hiyo, tunaweza tukalichukua tukaangalia lakini kinachotakiwa ni kuongeza uzalishaji katika maeneo hayo ili tuweze kununua, lakini wakati huo huo wananchi waweze kupata chakula cha kuweza kuwasaidia.

Na. 78

Serikali Kuwaruhusu Wakulima Kuuza Mazao Nje ya Nchi

MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. MCH. DR. GERTRUDE RWAKATARE aliuliza:-

Kwa kuwa, ukosefu wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo ni kikwazo kikubwa katika kuendeleza kilimo:-

Je, Serikali iko tayari kuwaruhusu wakulima kuuza mazao yao nchi jirani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa kuuza soko la bidhaa za Tanzania nje ya nchi likiwemo soko la mazao ya kilimo. Serikali pia inatambua umuhimu wa kuruhusu wananchi kuuza mazao yao nje ya nchi, hivyo sio sera ya Serikali kuzuia uuzaji wa mazao kwenda nje ya mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, kwa mazao ya chakula suala la usalala wa chakula kwa wananchi ni suala linalopewa kipaumbele wakati nchi inapokabiliwa na upungufu wa chakula. Ili kukabiliana na upungufu wa chakula, Serikali imeweka utaratibu

wa muda mfupi wa kuzuia uuzaji wa chakula nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na kuzuia mfumuko wa bei unaosababishwa kwa sehemu kubwa na kupanda kwa bei ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo ni kulingana na Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji wa Bidhaa nje ya nchi, Sura 381, toleo lililoboreshwa 2002 (*Export Control Act Cap 381, R.E, 2002*). Aidha zipo Sheria ndogo ndogo zilizotungwa kwa mujibu wa sheria hiyo zinazoainisha aina ya bidhaa zinazozuliwa kusafirishwa nje ya nchi. Kwa mfano, Serikali ilitoa agizo tarehe 28 Mei, 2008 la kusitisha uuzaji wa mazao ya mahindi, mchele, mtama, ngano, uwele, muhogo, viazi na maharage kwenda nje ya nchi ili kukabiliana na upungufu wa tani 860,000 za nafaka mwaka 2008 uliotokana na uzalishaji katika msimu wa 2007/2008, kutokutosheleza mahitaji ya mazao ya nafaka. Aidha, katika mwaka 2009 upungufu wa nafaka ulifikia tani 1,348,445. Kutokana na hali hiyo Serikali bado imesitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na kama nilivyotangaza yale mawili ya Nishati na Madini tutayapangia tarehe nyingine.

Matangazo; tunaanza na wageni kama kawaida yetu. Nafurahi kwa niaba yenu nyote kutambua ugeni mashuhuri wa wenzetu kutoka Bunge la Uganda taifa rafiki na ndugu zetu katika Afrika Mashariki. *Excellencies I want to recognise you when I mention your name please stand up so Members of Parliament can acknowledge you. I will start with the Hon. Rose Akoi Okulu Leader of delegation from Uganda. Wenzetu hawa wanazingatia sana mambo ya jinsia. Msafara unaongozwa na mwanamke sio vinginevyo. Hon. Med Mulumba, Hon. Jofrey Ekanya, Hon. Rose Munyira, Hon. William Okecho, Mr. Robert Tumukwasibwe and Mr. Sam Onyaka. It's a great pleasure to welcome you Members of Parliament from Uganda and your delegation we feel very much honoured and we hope that these visits contribute to the ever strengthening relation between our two countries. Thank you very much for being here.*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, hawa ni viongozi wa CHADEMA kutoka Wilaya mbalimbali. Wamekuja kusikiliza Bunge, bahati mbaya. Wapo wageni wa Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai ambao ni Ndugu Menard Swai, Mwenyekiti wa *KNCU* na Ndugu Martin Malya Mjumbe wa Bodi ya *KNCU*. Karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Wilaya ya Mpanda kwa maana hiyo ni pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Ndugu, Rose Mayaya, Mwenyekiti wa UWT Mpanda, Ndugu Getrude Kamahinda, Katibu wa UWT wa Wilaya na Ndugu Rhoda Mwakalenga, Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Wilaya ya Mpanda. Karibuni sana Wageni wetu. Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata, kutoka Taasisi ya Usalama Barabarani kwa watu wenye ulemavuambao ni Ndugu Jutoram Kabarale, Ndugu Hamis Nassor Cheni, inawezekana wamechelewa kufika.

Wapo wageni watano kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni Wahadhiri kutoka Chuo hicho. Leo wageni wetu kidogo kuna matatizo. Basi tutaendelea na matangazo ya kazi za Bunge. Nawafahamisha Wajumbe wa Uongozi *Stealing Committee* tukutane pale ukumbi wa Spika saa tano asubuhi.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) anaomba Wajumbe wote wa LAAC mkutane saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani mtakuna na watu wengi hapo. Mheshimiwa Mussa Azan Zungu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nje Ulinzi na Usalama anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane leo katika ukumbi mpya wa sherehe *basement* hapa hapa, namba 105.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira mkutane saa saba leo mchana katika ukumbi Pius Msekwa B. Nimeiruhusu Kamati ya Fedha na Uchumi ikutane saa tano kwa jambo maalum. Kwa hiyo, natangaza sasa tangazo la Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwamba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane kwa kikao saa tano asubuhi katika Ukumbi Namba 227 Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwisho wa matangazo na kulingana na shughuli inayofuata ambayo itakuwa ni Maazimio, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliuliza kama maazimio yamepita kwenye Kamati. Kamati husika imeyapitia maazimio yote kama utaratibu unavyohitaji. Kwa hiyo, sio kweli kama yanakuja moja kwa moja. Limekuja tangazo sasa hivi na kwa upendeleo maalum ambalo mtauelewa tu kwa sababu tangazo hili limeletwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo. (*Kicheko*)

Ingawa nilitangaza muda wa matangazo umekwisha, lakini wakubwa hawa wanapokwambia jambo inakubidi kutii. Kwa hiyo, kuna mgeni wa Wazira wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, naye si mwingine ni Mama Mariam Mwafisi, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, karibu sana. Basi kwa kuendeleza shughuli zinazofuata na kuniwezesha na mimi niendeleo na Kikoa cha Kamati ya Uongozi nimemwomba Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, aje aendeleze shughuli za Bunge. (*Makofi*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tuendeleo. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Kulinda
Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mimea
(*International Convention for the Protection
of New Varieties of Plants*)**

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu kwa mwaka huu wa 2010 naomba nichukue fursa hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bunda kuwapongeza na kuwatakieni Wabunge wote kheri na fanaka kwa mwaka 2010 hasa kwa kuwa ni mwaka wa lala salama.

Aidha nachukua fursa hii kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Vita Kawawa na Watanzania wote kwa ujumla kwa kifo cha Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa. Tunaomba Mwenyenzi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa nitoe hoja kuwa Mbunge lako Tukufu liridhie Mkataba wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa mwaka wa 1991 (*The International Convention for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*).

Mheshimiwa Mwenyekiti awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Gidion Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa kujadili Mkataba huu kwa kina na kutoa mapendekezo ambayo yamezingatiwa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio linalowasilishwa na Serikali hapa Bungeni lina lengo la kuliomba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, likubali Tanzania liridhie Mkataba wa Kimatifa wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*The International Convention for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*). Na hatimaye kuiwezesha kuwa mwanachama wa Chama wa Shirika la Kimatifa ya kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za Mimea. (*The International Union for the Protection of New Varieties of plants (UPOV)*). Kutokana na faida ambazo taifa letu litapata hususani katika uendelezaji wa sekta ndogo ya mbegu na sekta ya kilimo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuiwezesha Tanzania kujiunga na Shirika la Kimataifa la *UPOV* ni moja ya juhudi zinazotekelezwa na Serikali za kuimarisha mazingira ya sera na sheria za Sekta ya Kilimo ili ziweze kuvutia sekta binafsi kuwekeza zaidi katika utafiti wa mbegu bora za mazao na teknolojia mpya za kuendeleza kilimo nchini. Mazingira hayo yataiwezesha Tanzania kunufaika na teknolojia za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutoka nchi mbali mbali zenye maendeleo ya kilimo. Kwa kuwa yataruhusu kulindwa kwa haki miliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutoka nje watakaowekeza katika uzalishaji wa mbegu mpya hapa nchini.

Aidha, mazingira hayo yatahamasisha watafiti wa ndani na nje kufanya ugunduzi wa aina mpya za mbegu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Azimio. Ili kuhamasisha Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea nchini na kuwawezesha wachangie zaidi katika uzalishaji wa mbegu bora na maendeleo ya kilimo kwa ujumla mwaka 2002 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na kuweka utaratibu wa usambazaji wa mbegu hizo unaozingatia hakimiliki zao.

Hata hivyo, Tanzania imeshindwa kunufaika na teknolojia mpya zinazogunduliwa na Watafiti wa nje na pia imekuwa ikikosa misaada ya kimataifa kuwezesha mfumo wa kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa hapa nchini kuendeshwa kwa

ufanisi. Aidha, Wagunduzi binafsi wa nje na wa ndani wamekuwa wakisita kutumia fursa ya sheria yetu ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu kutokana na Tanzania kutokuwa mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*International Union for the Protection of New Varieties of Plants (UPOV)*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 nchi kadhaa za Ulaya zilitia saina Mkataba wa Kimataifa wa kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mbegu za Mimea (*International Convention for the Protection of New Varieties of Plants*) na hatimaye kuanzisha Shirika la UPOV. Mkataba huo uliboreshwa mwaka 1972, 1978 na 1991. Mojawapo ya malengo makuu ya Mkataba huo ni kuhakikisha kuwa nchi zinazouridhia zinakuwa na utaratibu wa kutoa na kulinda hakimiliki unaofanana na hivyo kuziwezesha kushirikiana katika kulinda hakimiliki katika nchi wanachama, ikiwa ni pamoja na kuendesha majaribio yanayomwezesha mgunduzi kukubalika na hivyo kupewa hakimiliki katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na faida na mafanikio yaliyopatikana kwa nchi wanachama, idadi ya nchi wanachama imekuwa ikiongezeka na sasa inajumuisha nchi nyingine zilizo nje ya Ulaya ikiwa ni pamoja na nchi za Bara la Asia kama vile China, Japan, Korea Kusini na Vietnam na nchi nne za Bara la Afrika, ambazo ni Kenya, Afrika ya Kusini, Morocco na Tunisia. Nchi jirani zilizo wanachama wa *UPOV* zimekuwa zikinufaika kwa kupata aina za mbegu zenye teknolojia mpya na ambazo zinakubalika katika masoko ya kimataifa kwa kuwa Wagunduzi wa nje wana imani na mfumo wa kutoa na kulinda hakimiliki za nchi hizo.

Aidha, utafiti unaonyesha kuwa Tanzania inaweza kunufaika zaidi na teknolojia mpya kutoka nchi zilizoendelea kutokana na kuwa na hali nzuri zaidi ya *agro-ikolojia* kwa uzalishaji wa mbegu bora, ikilinganishwa na nchi hizo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuridhia mkataba. Kuridhia mkataba huu na kujiunga na Shirika la *UPOV* kutakuwa na matokeo yafuatayo kwa Taifa letu:-

- (i) Teknolojia za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutoka nchi mbali mbali zenye maendeleo ya kilimo zinazoletwa nchini zitaongezeka;
- (ii) Tanzania itakuwa na haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi ya kimataifa juu ya kanuni na taratibu zinazosimamia utoaji na ulinzi wa hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;
- (iii) Imani ya Wagunduzi wa nchi mbalimbali katika mfumo wa Tanzania kuhusu utoaji na ulinzi wa hakimiliki itaongezeka na hivyo kuchochea uwekezaji zaidi katika utafiti wa mbegu bora zilizo na masoko kimataifa na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu;
- (iv) Tanzania itaruhusiwa kunufaika na matokeo ya majaribio ya hakimiliki yaliyokwishafanyika katika nchi nyingine wanachama, hususan kwa mazao yanayohitaji ujuzi na mazingira maalum ya utafiti;

- (v) Tanzania itapata nyaraka muhimu na miongozo mbali mbali ya kitaalaam juu ya uendeshaji wa majaribio ya uchunguzi kwa ajili ya utoaji wa hakimiliki;
- (vi) Tanzania itakuwa mwanachama wa Shirika la *UPOV* na itakuwa na haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele muhimu vya mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mkataba unazitaka nchi wanachama kuweka utaratibu wa kisheria wa kutoa hakimiliki unaokidhi masharti ya mkataba huo [Ibara ya 2 & Ibara ya 30].
- (ii) Mkataba unazitaka nchi wanachama kuweka masharti sawa ya utoaji na ulinzi wa hakimiliki kwa wagunduzi wa mataifa yote yaliyo wanachama wa *UPOV* [Ibara ya 4] & [Ibara ya 5]
- (iii) Mkataba unatoa upendeleo maalumu kwa wakulima kuzalisha na kutumia tena mbegu zilizolindwa ili mradi wasifanye biashara ya kuuza mbegu bila kupata kibali cha mgunduzi husika [Ibara ya 15 (2)]
- (iv) Mkataba unazitaka nchi wanachama kulipa michango yao ya mwaka kulingana na uwezo wao [Ibara ya 29 (1) - (4)]. Kwa sasa kiwango cha chini ni uniti zisizopungua 0.2 ambazo ni Faranga za Uswisi (*Swiss Francs*) 10,728.8 sawa na TSh. 10,800,000.00.
- (v) Mkataba unazitaka nchi wanachama kutoa mchango wa mara moja kwa ajili ya Mfuko wa Uendeshaji (*Working Capital Fund*) ambapo kiwango hutegemeana na idadi ya uniti za mchango wa mwaka. Kima cha chini cha kuchangia mfuko huu ni Tsh. 1,700,000.
- (vi) Mkataba unazitaka nchi wanachama kutoweka mashaka/masharti (*reservation*) juu ya hakimiliki zilizotolewa na nchi hizo, isipokuwa tu kama mashaka yanatokana na hatua zilizochukuliwa na nchi husika kwa mujibu wa mkataba wa awali wa mwaka 1978 [Ibara ya 35].
- (vii) Mkataba unaruhusu mwanachama yeyote kujitoka katika uanachama. Hata hivyo, kujitoka huko hakutafuta hakimiliki zilizokwishatolewa [Ibara ya 39].

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kujiunga. Utaratibu wa kujiunga na mkataba huo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Nchi inayotaka kujiunga itawajibika kuomba Baraza la *UPOV* lipitie sheria yake inayosimamia hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kuona kama inawiana na vipengele vyote vya mkataba.

(ii) Nchi ambayo haikusaini Mkataba, kama ilivyo Tanzania, ili iwe mwanachama itapaswa kuwasilisha Hati za kuuridhia (*Ratification Instruments*) kwa Katibu Mkuu wa *UPOV* ambaye atazijulisha nchi wanachama pamoja na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho. Kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo juu Serikali inapendekeza Tanzania iwe mwanachama wa Shirika la *UPOV* kwa kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mimea (*International Convention for the Protection of New Varieties of Plants*) wa mwaka 1991.

Kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohitaji kuridhiwa, hivyo naomba kuwasilisha AZIMIO la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa mwaka 1991 (*International Convention for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*) kama ifuatavyo:-

KWA KUWA nchi mbalimbali ulimwenguni zilikubali kupitisha na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*International Convention for the Protection of New Varieties of Plants*);

NA KWA KUWA, lengo la kuanzishwa kwa mkataba huo ni kuhakikisha kuwa nchi zinazoridhia mkataba huo zinakuwa na utaratibu wa hakimiliki unaofanana na hivyo kuziwezesha kushirikiana katika kulinda haki miliki na hasa katika majaribio yanayomwezesha Mgunduzi kupata hakimiliki;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo hazijaridhia Mkataba wa Kimataifa wa kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea;

NA KWA KUWA, mkataba huo unazitaka nchi zinazoridhia kuweka utaratibu unaokubalika kimataifa wa kutoa na kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;

NA KWA KUWA, kwa kuridhia Mkataba huo nchi yetu itaongeza imani katika mfumo wetu wa utoaji na ulinzi wa hakimiliki za Wagunduzi na hivyo kunufaika na teknolojia za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea wa nchi nyingine wanachama;

NA KWA KUWA Mkataba unatoa upendeleo maalum kwa wakulima katika kuzalisha na kutumia mbegu mpya zilizolindwa ili mradi wasifanye biashara ya kuuza mbegu bila kupata kibali cha Mgunduzi husika;

NA KWA KUWA Mkataba huo utaiwezesha nchi yetu kuwa mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*International Union for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*) na itakuwa na haki ya:-

- (i) Kushiriki maamuzi na kupata nyaraka za kitaalamu juu ya uendeshaji wa majaribio ya kiuchunguzi kwa ajili ya utoaji wa hakimiliki; na
- (ii) Kupata au kuuziwa matokeo ya majaribio kwa ajili ya utoaji wa hakimiliki yaliyokwishafanyika katika nchi nyingine mwanachama, hasa kwa mazao yanayohitaji ujenzi wa mazingira maalumu ya utafiti.

HIVYO BASI, Bunge hili katika Mkutano wake wa kumi na nane, na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*International Convention for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. SAID J. NKUMBA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*International Convention for Protection of New Varieties of Plants, 1991*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 15 Januari, 2010, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kujadili taarifa ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*International Convention for Protection of New Varieties of Plants, 1991*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alieleza umuhimu wa nchi yetu kuridhia mkataba huo kwa kuwa imekuwa ikikosa fursa mbalimbali kutokana na kutokuwa mwanachama wa chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu bora ni miongoni mwa mahitaji muhimu ya kilimo chenye tija na chenye uwezo wa kuchangia katika kukua kwa sekta ya kilimo na uchumi wa nchi

kwa ujumla. Hivyo basi, ipo haja ya kuhakikisha kwamba wagunduzi wa mbegu mpya za mimea wanalindwa, wanapewa haki miliki na wanafaidika na ugunduzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu na faida za kuridhia mkataba, nchi yetu ilitunga Sheria ya Kulinda Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu mnamo mwaka 2002. Hata hivyo, nchi imeshindwa kunufaika na tekinolojia mpya zilizogunduliwa na watafiti kutoka nje kutokana na kutokuwa mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (*International Convention for Protection of New Varieties of Plants, 1991*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea wa nje ya nchi, wamekuwa wakisita kutumia fusra zinazotolewa na sheria yetu kwa kuwa Tanzania siyo mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Kulinda Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*International Union for the Protection of New Varieties of Plants*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuridhia mkataba huu, nchi yetu itakuwa mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Kulinda Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na kwa hiyo, kufaidika na fursa nyingi zinazotolewa kwa wanchama wa chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba unazitaka nchi wanachama kuwa na utaratibu madhubuti wa kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea unaofanana na ule ulio katika nchi nyingine wanachama ili kuwa na utaratibu mmoja wa kulinda haki miliki za wazalishaji wa aina mpya za mbegu. Utaratibu huo utaweka vigezo vitakavyoweza mgunduzi kukubalika na hivyo kupewa hakimiliki katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuridhia Mkataba huu, nchi yetu itakuwa na haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi ya Kimataifa juu ya kanuni na taratibu zinazosimamia utoaji na ulinzi wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Aidha, nchi yetu pia itapata nyaraka muhimu na miongozo mbalimbali ya kitaalaam juu ya uendeshaji wa majaribio ya uchunguzi kwa ajili ya utoaji wa hakimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa kuridhia Mkataba huu, itaongeza imani ya wagunduzi wa nchi wanachama na hivyo kuchochea uwekezaji katika utafiti wa mbegu bora zilizo na masoko kimataifa na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, inaipongeza Wizara kwa kuwasilisha Azimio hili lenye nia ya kuendeleza sekta ya kilimo kwani inatambua umuhimu wa Mkataba huu na inaamini ili dhana ya KILIMO KWANZA iweze kufanikiwa tunahitaji kuwa na mbegu bora za mimea, hivyo kuna kila sababu ya kuridhia Mkataba huu ili wagunduzi wa aina mpya za mimea waendeleo kufanya utafiti na kugundua aina mpya za mbegu na zenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba Bajeti ya Utafiti inatengewa fungu la kutosha ili kufanikisha azma hii ya ugunduzi kwa kuwapatia vitendea kazi muhimu watafiti na kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua umuhimu wa matokeo ya utafiti na inashauri Wizara iweke utaratibu utakaohakikisha Matokeo ya ugunduzi yanawafikia walengwa ambao ni wakulima, kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza Wizara ihakikishe Huduma za ugani zinatolewa kwa wakulima wote nchini ili waelewe umuhimu wa kutumia mbegu bora zinazotoa mavuno mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iweke mfumo utakaoweza Mbegu bora kuzalishwa kwa wingi na kusambazwa kwa wakulima kwa utaratibu mzuri katika maeneo yote yanayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuhakikisha wagunduzi wa aina mpya za mimea wanafaidika na ugunduzi wao kwa kuweka utaratibu wa kutoa Tuzo kwa wagunduzi wa mbegu bora ili kuendelea kuwatia moyo na kuongeza ushindani wa ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu wa kulinda vinasaba vya mimea vinavyopatikana humu nchini ili kuhakikisha kwamba vinatumia kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kuwatambua wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili na hatimaye kutoa na ushauri. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti.

Wengine ni Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah na Mheshimiwa Said J. Nkumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. David M. David (Mb), Katibu Mkuu, Ndg. Mohamed Muya, Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Sophia Kaduma pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha vyema Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah, kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha Taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati, Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Angumbwike Lameck Ng'wavi, kwa kuihudumia Kamati vizuri wakati wote na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. Aidha, napenda niwashukuru kwa namna ya pekee wananchi wa Jimbo langu la Sikonge kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge hili Tukufu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu kuridhia mkataba wa Kimataifa wa wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa mwaka 1991 (*Internationa Convention for the Protection of New Varieties of Plants, 1991*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama kwa kuchangia, napenda nitoe shukrani za mwaka mpya wa 2010, kwa Watanzania wote na hasa kwa wapiga kura wa Jimbo langu la Chambani, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiniipatia katika kutimiza majukumu yangu ndani ya Bunge na nje ya Bunge kipindi chote toka waliponipa ridhaa yao ya kuwawakilisha katika chombo hiki kikubwa cha kutunga sheria mwaka 2005. Napenda kuahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia na kuwatumikia na kuwatumikia hadi hapo watakaposema basi inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe salaam za pole kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla waliofiwa na ndugu na jamaa zao. Namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika wakati huu mgumu unaowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusiana na kataba huu, sekta nzima ya wagunduzi wa mbegu za mimea (*plant breeders*) katika nchi hii ilikuwa imesahaulika na imekuwa ikiwakatisha tamaa wataalam wetu wanaofanyakazi katika vyuo vya utafiti. Aidha, wataalam hao wamekuwa wakifanyakazi katika mazingira magumu sana na kazi zao zimekuwa haziwanufaishi wao wala familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli huo uko wazi kwani wataalam katika Chuo cha Kilimo Ilonga Mkoani Morogoro, kwa mfano; wamekwishagundua mbegu za mahindi zinazostahamili hali ya hewa ya maeneo mengi hapa nchi. Lakini mbegu zao zimeshindwa kuwafikia wakulima kutokana na kukosa msukomo katika soko na badala yake mbegu zinazozalishwa na kusambazwa na makampuni ya nje ndizo zinazouzwa kwa wakulima wetu. Aidha, kuna aina mbalimbali za Maharage zimezalishwa Chuo Kikuu cha Kilimo Morogoro- SUA na kupewa jina la SUA 90, halikadhalika Chuo cha Mafunzo na Utafiti Uyole Mbeya lakini cha ajabu wagunduzi pamoja na asasi zilizoshirikiana nao hazikunufaika na ugunduzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia ugunduzi wa mbegu mpya ambao umekubalika, kunahitajika ufuatiliaji wa karibu na kuangalia kila badiliko linalojitokeza. Kazi hii inachukua muda mrefu sana na inahitaji nyenzo nyingi, jambo ambalo kwa nchi yetu limekuwa ni kikwazo hivyo kuwakatisha tamaa Wagunduzi wetu na kuwafanya wale wote wanaotaka kuingia katika tasnia hiyo kuwa na mtazamo hasi. Kwa utaratibu huo, unatufanya sisi kama nchi kuendelea kuwa tegemezi kwa kazi zinazofanywa na wenzetu miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Azimio hili limechelewa kuletwa kwani vijana wengi wapya wamekwishaingia katika fani zingine baada kuona kuwa fani ya “*plant breeding*” hailipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudumaa kwa tasnia nzima ya ugunduzi wa mbegu za mimea kwa njia moja au nyingine imesababishwa na wanasiasa, kwani wao hawaelewi vigezo vya mbegu bora, wao wanaelewa kigezo kimoja tu cha mavuno mengi, lakini kigezo cha kuhimili magonjwa na muda wa kuiva na vigezo vingine wao hawavielewi na kwao vigezo vingine si kipaumbele. Kambi ya Upinzani inawataka wanasiasa wabadili mtazamo na kuwaachia wataalam kushughulikia masuala yanayohusu taaluma zao. Sambamba na hilo, Serikali inashindwa kutoa fedha za kufanya utafiti kwa muda muafaka kwa visingizio mbalimbali. Jambo hilo linavunja moyo kwa wataalam katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaunga Mkono Mkataba huu kwani utaiwezesha nchi yetu kuwa mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*International Union for the Protection of New Varieties of Plant-UPOV*), kwani ni ukweli ulio wazi kuwa Tanzania inathamini Wagunduzi wa mitambo mbalimbali lakini ugunduzi unaosababisha Taifa kushiba na kuondokana na utapia mlo hauthaminiwi na kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi sio tu Bunge hili kuridhia mkataba huu, bali ni kutengeza mazingira na kuwatafuta wale wote waliokwisha kata tamaa na kuwarudishia matumaini ya kumalizia kazi zao kwa kuwapa nyenzo na motisha zitakazowafanya nao wajione kuwa wanathaminiwa katika Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Waheshimiwa Wabunge, kwa Azimio hili, katika orodha niliyo nayo, nina mchangiaji mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Charles Keenja ambaye sasa nitamwita ili aweze kuanza kuchangia.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kuipongeza sana Wizara ya Kilimo, kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kuleta Azimio hili hapa Bungeni ili liridhiwe. Tanzania ni nchi ya kilimo, tunategemea sana kilimo, uchumi wetu unategemea kilimo kwa asilimia 26, asilimia zaidi ya 90 ya chakula tunachokula kinatokana na kilimo na malighafi nyingi tunazotumia katika viwanda zinatokana na kilimo. Kwa hiyo, jambo lolote ambalo litawezesha kuboresha kilimo chetu, kwetu sisi ni jambo la msingi na ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu ni suala muhimu sana kwetu. Kwa hiyo, ni vizuri tukaridhia haraka mkataba huu ili tujiunge na chombo hiki ambacho kina manufaa kama ambayo yameelezwa hapa na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Wizara na hata Kambi ya

Upinzani. Kwa hiyo, mimi naunga mkono Azimio hili moja kwa moja na naomba nilihimiza Bunge lako lifanye hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa kwanza kabisa kufaidika na Azimio hili, ni Serikali yenyewe. Utafiti mwingi unaofanywa katika nchi hii, uzalishaji wa mbegu unaofanyika katika nchi hii, unafanywa na Serikali yenyewe katika Vituo vya Kilimo vya Utafiti ambavyo ni pamoja na Uyole, Ukiliguru, Seliani n.k. matokeo ya utafiti unaofanywa ni mali ya Serikali, kwa hiyo, Serikali ndiyo ya kwanza kabisa itakayofaidika kuwa na Haki Miliki ya matokeo ya utafiti unaofanywa katika vituo vyake. Hiki ni kivutio cha kutosha kabisa kwa Serikali kuona umuhimu wa kushughulikia suala hili na kulishughulikia kwa umakini na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii niwapongeze sana Watafiti wetu wa aina mbalimbali za mbegu ambazo wamezalisha ambazo zimeboresha sana kilimo katika nchi hii, wamefanya hivyo katika mazingira magumu sana, wakati mwingine bila vitendea kazi, kwa fedha kidogo sana zinazopatikana na bila vifaa wanavyohitaji ili waweze kufanya kazi hii kwa ukamilifu. Nawapongeza sana Watafiti wetu na nawaomba waendeleo kujitahidi kufanya kazi zao kwa umakini na kwa bidii kama ambavyo wamefanya kazi katika mazingira magumu, hasa katika siku zinazokuja chini ya Kilimo Kwanza, tunategemea watapewa pesa nyingi zaidi za kuwawezesha kuzalisha kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuikumbusha Wizara mambo mawili; la kwanza, usimamizi wa utafiti katika nchi hii una matatizo hasa kutokana na mabadiliko yaliyofanyika ambayo yanaweza yakawa na madhara katika sekta hii. Tumewahi kuomba hapa Bungeni kwamba Wizara ilete Sheria Maalum itakayosimamia utafiti wa kilimo katika nchi hii na itakayosimamia matokeo ya utafiti huo. Kwa sasa hivi, hizi taasisi mbalimbali zilizoanzishwa, kwa mfano Taasisi ya Kahawa, ya Tumbaku n.k. zimeanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni na *actually* wanaweza wakafanya jambo lolote na matokeo ya utafiti ambayo yanaweza yakawa hayana manufaa makubwa sana kwetu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali izingatie hili na ihakikishe kwamba yanafanyika marekebisha. Sina hakika kama Wizara inaweza ikaleta Muswada Bungeni hapa kabla ya uchaguzi wa mwaka huu, lakini wafanye bidii kuhakikisha kwamba mapema iwezekanavyo, sheria hiyo inapatikana, unawekwa utaratibu madhubuti wa kusimamia shughuli za utafiti katika nchi hii na kusimamia matokeo ya utafiti huo. Hili ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mbegu nyingi sana zinazotumika hapa nchini zinatoka nje. Kiasi tunachozalisha sisi wenyewe kupitia katika vituo vyetu na mashamba yetu ya kuzalisha mbegu ni kidogo sana, hakizidi tani 30,000 kwa mwaka. Hizo mbegu zinazozalishwa nje hazizingatii mazingira ya nchi hii. Kwa hiyo, ni lazima tuchukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba wazalishaji wa mbegu wanafanya hivyo ndani ya nchi. Wa kwanza ni vituo vyetu wenyewe, lakini wa pili ni watu binafsi ambao wana uwezo wa kuzalisha mbegu wanaotoka nje ambao kutokana na vivutio mbalimbali vitakavyowekwa hasa baada ya kupitisha Azimio hili, watakuja kuzalisha mbegu humu humu nchini, kuzisambaza humu nchini na mbegu hizo zitakuwa zinazingatia mazingira yetu na kwa hiyo zitakuwa na manufaa makubwa zaidi kwetu kuliko mbegu zinazozalishwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikuwa Arusha na tulitembelea moja ya mashamba yanayozalisha mbegu. Shamba lile linaajiri wafanyakazi

1500, linazalisha mbegu ambazo zinauzwa nje na wanaanza kuzalisha mbegu ambazo zitasambazwa humu humu nchini. Walituambia mbegu moja ya nyanya (mbegu moja, siyo gramu moja) ina thamani ya EURO moja (karibu shilingi 2000). Kwa hiyo, mbegu zina gharama kubwa sana. Ni vizuri tukahakikisha kwamba tunazalisha humu humu nchini ili kwanza, kupunguza gharama yake, lakini pili ili kuhakikisha kwamba zinaendana na mazingira ya nchi yetu. Hawa wanaozalisha Arusha ni watu kutoka nje, wamekuja nafikiri kwa kuvutiwa na Sheria yetu ya mwaka 2002 na watavutiwa zaidi tutakapokuwa tumejiunga na chombo hiki cha kusimamia hakimiliki kimataifa kwa sababu watakuwa na hakika zaidi kwamba kumbe wanachofanya kitakuwa ni chao na hakitakuwa na matatizo ya kuingiliwaingiliwa na watu wengine kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendeleze utaratibu huu na tuendeleze kuhimiza haya mashirika mbalimbali yanayozalisha mbegu ili yaje yafanye kazi hiyo humu humu nchini. Ardhi tunayo, maji tunayo, hali nzuri ya hewa tunayo, nina hakika tuna mazingira mazuri kuliko nchi nyingi, jitihada zifanyike kuhakikisha kwamba tunazalisha mbegu na kulinda hakimiliki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, ningependa vile vile tukumbuke kwamba watumishi wetu wanaozalisha mbegu hizi wanastahili na wao kufaidika na ugunduzi wao, kwa hiyo tuweke utaratibu utakaohakikisha na wao wanapata vivutio vya kuwafanya waendeleo kufanya kazi hii kwa bidii zaidi. Najua Wizara ya Kilimo inawapa bakshishi kiasi fulani wanapokuwa wamezalisha aina za mbegu. Suala hili liangaliwe na liwekewe utaratibu rasmi, isiwe ni jambo tu ambalo linafanyika bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo limegusiwa na Kamati nalo ni hili suala la wizi wa vinasaba katika nchi yetu. Katika nchi hii tuna utajiri mkubwa sana wa vinasaba vya mimea mbalimbali kutokana na kuwa na mimea mingi sana. Kutokana na teknolojia iliyoko duniani hivi sasa, inawezekana mtu akaja Tanzania akachukua mmea wenye vinasaba fulani, akaenda akatumia teknolojia hiyo akazalisha mimea mingine na akadai vinasaba vile ni vyake na akavisajili na kwa hiyo akapata hakimiliki ya vinasaba hivyo. Tusipokuwa makini, tunaweza tukajikuta katika mazingira magumu ambayo yatatufanya tushindwe hata kutumia sisi wenyewe vinasaba vile ambavyo vinapatikana nchini mwetu. Kwa hiyo, ninaomba Wizara, katika kuweka utaratibu wa kusimamia masuala haya, tuweke utaratibu vile vile wa kulinda maliasili hii tuliyonayo katika Taifa letu na kuhakikisha kwamba inatumika kwa manufaa yetu na siyo kwa manufaa ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni muhimu sana na ni lazima sheria yetu ya kulinda Wagunduzi wa aina mpya za mbegu ilingane na mahitaji ya mkataba huu. Kwa hiyo, tungeomba Wizara haraka sana iende ikaangalie, ikapitie upya ile sheria na kuhakikisha kwamba inaendana na mkataba huu na kwa kufanya hivyo, kuhakikisha kwamba tunajiunga mapema iwezekanavyo na hiki chombo na tunaanza kufaidika na yale yanayotolewa na chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Nami naunga mkono hoja ya Waziri ya kudhibiti na kuandikisha wagunduzi wa mimea Tanzania

na naunga mkono yote aliyosema ndugu yangu Mheshimiwa Charles Keenja, kwanza kwa sababu yeye ni mzoefu wa suala hilo, lakini vile vile kwa sababu ni ukweli mtupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la wizi wa vinasaba ni kubwa sana. Kuna habari kwamba wako watu wa nje wanaokuja kwenye nchi zetu kama watafiti, wanapokaa kule wanagundua au wanashiriki na kushirikishwa kwenye ugunduzi unaoendelea kwenye maabara hizo za vituo vyetu vya utafiti na baadaye wanachukua zile siri, wanakwenda kuziandikisha mapema, wanazifanya ni zao. Nilikuwa nasoma wakati mmoja kwamba jambo hili linafanyika sana hasa kwenye vituo vya utafiti vya Kenya. Kwa hiyo, ni kweli kwamba hata kwenye vituo vyetu vya utafiti tuwe waangalifu sana tunapofanya tafiti za namna hii ili wageni wasije wakatuwahi na kuchukua ugunduzi wa watu wetu na kuufanya kuwa wao na kufaidika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma vile vile habari za mimea miwili; mti unaoitwa Mwarobaini na mbegu zake na mchele wa Basmati. Hii ni habari ya kweli, kulitokea kwamba wako watu Amerika na Ulaya waliochukua mchele wa Basmati, wakaenda wakauandikisha kwao Ulaya na Amerika wakasema ni wao. Kumbe mchele ule asili yake ni India, lakini Wahindi walikuwa hawajauandikisha kwamba ni mchele wao, kwa hiyo ikaonekana Basmati ni mchele wa Ulaya na ni mchele wa Amerika, nadhani Carlifonia. Wahindi walikwenda Mahakamani kusema asili ya mmea huu ni India. Amerika walishinda, India hawakushinda na hata kushinda kwao ni kwa baadhi ya vipengele, siyo vyote. Kwa hiyo, ni jambo lisilo la kawaida kwamba mchele au mpunga wa Basmati ni wa India lakini pia ni wa Ulaya au wa Amerika na wanaofaidika sasa ni wale waliokwenda kuwahisha kuandikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari nyingine za mmea huu wa Mwarobaini. Vivyo hivyo watu walichukua mbegu zake wakaenda wakaandikisha, mmea ule ukawa ni wa Ulaya na vile vile Amerika. Wahindi wakaenda Mahakama za Kimataifa kusema mmea huu ni wa India, wakashinda kesi, lakini *again siyo a hundred percent*, kiasi kikaitwa cha India, kiasi kikaitwa chao kwa sababu hizi alizokuwa anaeleza Mheshimiwa Charles Keenja kwamba wajanja wanachukua, wanafanya *modification* kidogo tu kwa hiyo haifanani mia kwa mia na ile mbegu asilia. Kwa hiyo, inakuwa ni yao kwa maana kwamba wamefanya ukarabati kidogo wa hapa na pale lakini ukweli Mwarobaini ni mmea wa India na mchele wa Basmati ni wa India, kwa hiyo tuwe wangalifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nililisoma vilevile ni kwamba kuna watu wanaokuja huku kwetu na hasa hao wanaotafiti mambo ya mazingira, mambo ya misitu, wanaokota mimea, wanachukua. Wanakwenda kule kwao kufanya *modification* za namna fulani na kwa hiyo sasa wanafanya mmea unakuwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mmea mmoja, jina nimelisahau, unaitwa USAMBARANSIS jina la Kilatini yaani ni mmea wa Usambara uliochukuliwa kwenye misitu ya

Usambara; ni mmea wa dawa. Wakachukua zile dawa wakaziandikisha wakasema ni zao na ule mmea wakauandikisha wakasema ni wao lakini mmea upo hapa katika misitu ya Usambara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kweli kabisa kwamba watu watakuja hapa kuiba siyo tu zile mbegu ambazo zinagunduliwa kwenye Maabara za vituo vyetu vya utafiti lakini hata hivi hivi zilivyo, wakishajua mti huu una maana fulani au mbegu hii ina maana fulani, wataichukua, wataenda kuandikisha mmea wa Usambara, unapachikwa jina la Kilatini na mmea wa mahali popote pale hata kama ni Tanzania unapitishwa na mvumbuzi anapatikana ni Mzungu si Mtanzania si Msambaa wala siyo Mmasai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, liko eneo kubwa kabisa, sisi wengi tunaotumia dawa za kienyeji na waganga wengi wa dawa za kienyeji wale wanaotumia mitishamba na vitu vya namna ile kujiandikisha, la sivyo siku moja dawa zote hizi zitakuwa ni za Wazungu na Wazungu ndiyo watakao kula ile *royalty* ya uvumbuzi na ya ugunduzi. Kwa hiyo, najua hili siyo la Wizara hii lakini kwa sababu Serikali ni moja na Waziri Mkuu namwona yuko hapa nilitaka niliseme hilo kwamba eneo hili ni kubwa, ni pana na nadhani kama Taifa hatujalifanyia kazi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuandikisha ile mimea ambayo tunajua kimila ina manufaa fulani kama dawa au kama chakula labda jambo moja ambalo pengine hatulifahamu na ni vizuri Waziri pia alifuatilie ni kuwa jambo moja lililoko hapa Tanzania ni kwamba kule kwenye *Commission for Science and Technology Dar es salaam* na *BRELA* ambapo *BRELA* wanashughulikia haya mambo ya uvumbuzi na uandikishaji wa vumbuzi mbalimbali, *BRELA* akishirikiana na *Commission for Science and Technology*, wana kituo ambacho kiko kule *Commission for Science and Technology* ambacho unaweza ukaandikisha vitu kama hivi vya Azimio hili kwamba hata kama ingechukua muda, au kama unadhani watu wanaweza wakakupora utalamu wetu kijanja bila sisi kujua unaweza leo ukajiandikisha pale Sayansi na Teknolojia na ile ikatambuliwa Duniani kote. Kwa hiyo, hiyo *facility* kwa kweli ipo na ina kama mwaka mmoja au miwili hivi kwa umri lakini ipo na tunaweza kuitumia hasa tunapoweza kuandika vumbuzi ambazo tunaamini ni za Tanzania au kuandikisha mimea au mbegu tunazodhani zina manufaa na ni za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonaldo ni kwamba watu wengi nadhani wanaogopa au wanaona hili jambo si la manufaa sana kwa hiyo wanaacha na watu wa nje wanakuja wanatupora. Wanachukua utalamu wetu au ujuzi wetu kama nilivyokuwa nimejaribu kueleza. Mimi naunga mkono jambo hili ni jema, limechelewa kama alivyosema Msemaji wa Upinzani na ni vizuri tuliharakishe kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Basil Mramba. Sasa nitamwita mtoa hoja ili aweze kuhitimisha kwa kujibu hayo machache yaliyojitokeza. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika!

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kuwashukuru wote ambao wamechangia hoja hii na kwa kweli sitakuwa na maelezo mengi sana kwa sababu mimi nakubaliana na ushauri wote ambao

umetolewa. Ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ambaye tumeshirikiana naye na Kamati yake katika kuutazama Mkataba huu na ushauri wa mwisho ambao ameutoa tutauzingatia ili kuona kwamba tunaboresha zaidi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru rafiki yangu Khamis ambaye naye amechangia kwa kueleza kwamba suala hili limechelewa na kutoa maelezo mengi mengine ambayo ni ya kweli kwamba tumechelewa katika jambo hili na si jambo zuri sana lakini lazima tukiri kwamba maendeleo wakati mwingine hayaendi *speed* kama wote tunavyopenda. Kwa hiyo, tumeleta hoja hii na nia yetu ni njema kabisa kutaka tuboreshe zaidi utafiti pamoja na umiliki wa matokeo, kwamba tunao watafiti ni kweli siyo kwamba tulisahau mambo ya utafiti lakini mimi nadhani sekta nzima ya kilimo hatukuwekeza vya kutosha katika miaka mingi na ndiyo maana tumetoa dhana ya Kilimo Kwanza ambayo kusema kweli hii tunayoelekea sasa ndiyo itakuwa bajeti ya kwanza tangu tulipotoa ile kauli ya Kilimo Kwanza. Naamini tutazingatia masuala haya ya utafiti katika bajeti zinazofuata ili kusaidia zaidi kazi nzuri sana ambayo inafanywa na Watafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitakuwa sikuwatendea haki Watafiti kama sitatumia fursa hii, kuwapongeza sana kwa kazi nzuri sana wanayofanya, hatuwapi *resources* za kutosha kwa sababu ya matatizo yetu ya kibajeti lakini kwa kweli tunao Watafiti mahiri sana katika Tanzania, nenda katika vituo vyetu na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge niwakaribishe mkipata nafasi muwatembelee Watafiti, utaona mazingira si mazuri lakini matokeo ni makubwa. Niliwahi kwenda Naliendele, utakuta kuna matokeo mengi sana ya zao la Korosho, Ufuta ambayo yametokea kutokana na kazi nzuri ya Watafiti wetu pale, ukienda Uyole utakuta hali ni ile ile, ukienda Salieni hali ni ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba utafiti umekuwa unaendelea lakini hatuupi fedha za kutosha lakini kazi ambayo imekuwa inafanyika ni nzuri sana. Mimi lazima niwapongeze na niwatie moyo kwamba *spirit* hii ya Kilimo Kwanza itaendelea. Mimi naamini na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa kwamba tutenge angalau asilimia moja ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya vituo vya Utafiti siyo vya Kilimo lakini Utafiti kwa ujumla, nadhani utafiti katika kilimo utanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri Kivuli, rafiki yangu Khamis alizungumzia juu ya Azimio limechelewa, tunasema ndiyo limefika sasa na sasa tutaenda kwa *speed* zaidi katika kuhakikisha kuwa utafiti huu unawatia moyo Wagunduzi kwa sababu sisi siyo Kisiwa tukifanya Utafiti ambao hauhusishi *brain* ya nje, tutakuwa tumejifunga. Kwa hiyo, Azimio hili linafungua pazia kwamba sisi tunaweza kupata matokeo ya utafiti unaofanyika nchi nyingine na vilevile sisi tutaweza ku-*register* matokeo yetu katika Shirika hili la Kimataifa na kwa hiyo yale aliyokuwa anasema Mheshimiwa Mramba ya kuibiwa yanaweza yakapungua kama tumewahi ku-*register* kwa sababu ukisha-*register* mtu mwingine hawezi aka-*register the same*, hili nalo tutalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khamis alisema Wanasiasa wasiingilie masuala ya utaalumu, tuwaachie wataalamu na mimi nasema sisi hatuingilii utalaamu. Kwanza mimi siujui kabisa siwezi kuwa *Breader* lakini kazi kama Mwanasiasa ninayesimamia sekta ya kilimo ni kuwatia moyo *Breaders* wafanye kazi yao huku wakijua kwamba Serikali ambayo

inaendeshwa na Waniasia inawaunga mkono na kuwatia moyo. Hiyo ndiyo *role*, tunagawana wao wanafanya *Breeding* sisi tunawatia moyo, kwa hiyo nilidhani hata Mheshimiwa Khamisi anakubali kwa sababu maneno aliyosema alikuwa anakusudia hivyo nadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea masuala aliyoyasema Mheshimiwa Keenja. Kwanza tunamshukuru sana ameunga mkono na amesema Watafiti tuwape moyo na mimi nakubaliana naye kabisa. Amesema tutazame uwezekano wa kuwepo Sheria maalumu ambayo inasimamia utafiti, tutalitazama jambo hili ingawa pengine halitawezekana katika kipindi hiki cha uhai wa Bunge hili lakini ni wazo zuri ambalo nadhani itabidi tulitazame katika siku zinazokuja ili tuwe na Sheria maalumu inayosimamia utafiti nk.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile amezungumzia juu ya mbegu zinazotoka nje na kwamba tunatumia mno mbegu za nje badala ya kutumia mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Mheshimiwa Keenja anafahamu vizuri tu kwamba tunazo aina nyingi za mbegu ambazo zimegunduliwa hapa nchini, udhaifu wetu ulikuwa katika kuzizalisha (*multiplication*) lakini aina za *breeders seeds* ziko nyingi. Sasa kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kwamba wakati Watafiti wanaendelea kutafiti, sasa tunaingia katika hatua ya pili ya kuzizalisha yaani *multiplication* kwa hiyo uwekezaji mwingi sasa tunauelekeza katika utafiti lakini pia katika uzalishaji wa mbegu zenyewe ili ziweze kumfikia mkulima kwa sababu haitoshi tu ku-*bread* halafu unabaki na mbegu ambayo haifiki kwa mkulima na ile *breeders seed* haiwezi kwenda kwa mkulima lazima itengenezwe katika mfumo unaoitwa '*the foundation seed*' halafu ukitoka *foundation seed* ndiyo uende kwenye *multiplication*. Ie ambayo ni *multiplied* ndiyo sasa inaingia moja kwa moja kwa mkulima. Kwa hiyo, maelezo ya Mheshimiwa Keenja ninayaunga mkono na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya mazao ya bustani kama aliyoonna kule Arusha ni jambo ambalo linatupa matumaini makubwa *actually* labda nitumie fursa hii kusema kwamba Tanzania ni *sleeping giant* katika masuala ya *horticulture* na nchi hii inaweza kabisa ukabadili uchumi wake kabisa kwa kutumia *horticulture* kwa sababu mazingira yote yanaruhusu tena sehemu kubwa ya nchi yetu mazao haya yanastawi kwa mfano Kaskazini mwa Tanzania sasa watu wengi kwa sababu ya upungufu wa ardhi *horticulture* inaanza kuwa ni zao kuu ambalo wanalima na unaweza uka-*process* au ukasafirisha mpaka katika masoko ya nje. Kwa hiyo, uzalishaji wa mbegu hizi za *horticulture* na yenyewe tunaipa umuhimu. Maeneo ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania, hata Mikoa ya Ziwa hali ya hewa iliyoko kule yote inavutia zaidi *horticulture*. Kwa hiyo, unaweza ukalima mazao haya na kwa kutumia viwanja vya ndege vilivyopo Dar es salaam, Mwalimu Julius Nyerere au Songwe kule Mbeya kikimalizika au Mwanza kikipanuliwa unaweza ukapata mazao ya *horticulture* na ukauza katika masoko ya nje na ukaweza kukuza uchumi wa Tanzania, kwa hiyo suala hili tutalipa umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwatie moyo wazalishaji wa mbegu, ninakubali na sasa tutaanza kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mbegu. Haya yalikuwa maelezo ya Mheshimiwa Keenja.

Vilevile Mheshimiwa Mramba ameunga mkono maelezo hayo na ametupa mfano na kutahadharisha juu ya wizi wa vinasaba vya mimea, hili ni jambo kubwa. Kama yeye alivyosema na sisi tutalitazama kwa mazingira ya ukubwa wake. Lakini kwa suala linalohusiana na mbegu,

vinasaba vya mimea inayotokana na utafiti wa kilimo huko kwenye mipaka, tumeweka watu na tunazo sheria ambazo zinazuia uvushaji wa aina zozote za mimea na uingizaji vilevile hapa nchini lakini naamini labda hiyo ni hatua kubwa ya kuweza ku-*deal* na matatizo kama yale aliyokuwa anaeleza Mheshimiwa Mramba kama yale ya kuibiwa kwa MWAROBAINI au mchele wa aina ya BASMATI, hayo mambo yote ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ku-*register* vinasaba, kama inavyofanyika pale *COSTEC* hili ni jambo zuri. Lakini vilevile halijawa kubwa sana kwa sababu ya mazingira ya uchumi wetu lakini ukienda katika nchi nyingine, kuna Benki kabisa benki ya aina mbalimbali ya vinasaba vya mimea, tuliwahi kutembea na Mheshimiwa Waziri Mkuu kule India ambako tulijionea mahali ambapo mimea ya aina mbalimbali imehifadhiwa na nchi yoyote ile inaweza ikapeleka mimea yake kule ikaihifadhi ika-*register* na ikaichukua wakati wowote inapoihitaji. Nadhani hiyo hatua inayofanywa na *COSTEC* ni mwanzo mzuri ambao unastahili kuungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wote kwa kweli waliochangia, hawakuwa wengi, Mheshimiwa Keenja ameleta vilevile maelezo mengine kwa maandishi ambayo nayo tutayazingatia yalikuwa yanaongezea yale ambayo tumeshayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mwisho nimalize kwa kuwashukuru tena wachangiaji, sikutaja majina kwa sababu ndiyo hao hao niliowataja, ni Kamati, ni Keenja, ni Basil Mramba na mimi nahitimisha pamoja na Khamis, kwa hiyo nawashukuruni sana na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na kwa maana hiyo Bunge limepitisha Azimio hili na ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kulileta kwa wakati na kuweza kulipitisha na kuungwa mkono na Bunge zima.

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Mwaka 1991 (International Convention for Protection of New Varieties of Plants, 1991) liliridhiwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Tunaendelea, sasa nitamwita tena Mheshimiwa Waziri kwa Azimio lingine ili aweze kutuwasilishia hapa Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 yaani *The Internatinal Coffee Agreement ICA, 2007*, karibu Mheshimiwa Waziri.

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka 2007
(*International Coffee Agreement-Ica, 2007*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la kukubali Kuridhiwa Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa shukrani nyingi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa kujadili Mkataba huu kwa kina na kutoa mapendekezo ambayo tumeyazingatia. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Wazalishaji na Watumiaji wa Kahawa Duniani (*International Coffee Agreement - ICA*) tangu mwaka 1962 Umoja huo ulipoanzishwa na imeridhia marekebisho katika Mkataba huo yaliyofanyika mwaka 1983 na 2001 kutokana na umuhimu na manufaa inayoyapata katika biashara na maendeleo ya zao la Kahawa ambalo hutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa kila mwaka. Kahawa huchangia asilimia 33 ya mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa na huajiri asilimia kubwa ya wakulima katika Mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Kagera, Ruvuma, Kigoma na Mara. Aidha, kwa mujibu wa Mkakati wa Kuendeleza Zao la Kahawa wa 2010, kilimo cha Kahawa kitapanuliwa kujumuisha Mikoa ya Rukwa, Iringa, Morogoro, Tanga, Mwanza na Manyara na hivyo kuwanufaisha wakulima wengi zaidi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa ulifanyiwa marekebisho yenye malengo ya kuimarisha sekta ndogo ya Kahawa duniani na kuwezesha upanukaji endelevu wa masoko katika mazingira ya soko huria ili kunufaisha washiriki wote, hususan wakulima wadogo, kuongeza uwazi kwenye biashara ya Kahawa kimataifa na kuondoa vikwazo vya kibiashara ya Kahawa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio litakalojadiliwa linakusudia kuiwezesha Tanzania kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 (*International Coffee Agreement - ICA, 2007*) ili kuwezesha nchi inufaike na fursa zinazotolewa ndani ya Mkataba huo ambao una madhumuni ya kuimarisha sekta ndogo ya Kahawa duniani na kuwezesha upanukaji endelevu wa masoko ya Kahawa duniani kwa manufaa ya wadau wote katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhiwa kwa Mkataba huo kutaleta faida na matokeo yafuatayo kwa Taifa letu:-

(a) Kuongeza masoko ya Kahawa ya Tanzania. Marekebisho ya mwaka 2001 yaliwezesha masoko ya Kahawa kupanuka kutoka yale ya asili ya nchi za Ulaya na kwenda kwenye masoko ya Japan na Marekani, jambo lililoongeza ushindani na bei kwa mkulima na kufanya bei za Kahawa ziongezeke na ziwe zenye kumpatia mkulima faida kutokana na mikakati iliyowekwa na *ICO* ya kuongeza ubora wa Kahawa. Marekebisho ya mwaka 2007 yanayolenga kutangaza duniani kote ubora wa Kahawa ya wakulima wadogo kutoka nchi zinazoendelea yatawezesha Kahawa ya Tanzania kuuzika katika masoko mapya ya Urusi na China;

(b) Tanzania kupata fedha za kuendeleza wakulima wadogo. Marekebisho ya mwaka 2007 yanaanzisha chombo maalum kitakachoshughulikia masuala ya fedha na takwimu na kuipa mamlaka Umoja wa Kimataifa wa Kahawa (*International Coffee Organization - ICO*) kufadhili

miradi ya wakulima wadogo inayolenga katika kuongeza ubora wa Kahawa na kufuatilia mnyororo wa uzalishaji (*value chain analysis*);

(c) Tanzania kunufaika na miradi inayofadhiliwa na Umoja wa *ICO* ya kuongeza thamani na kuhimiza uuzaji wa Kahawa iliyosindikwa. Kwa mfano, kutokana na kutia saini Mkataba wa 2007 Tanzania hivi sasa inanufaika na Mradi wa Kudhibiti Ugonjwa wa Mnyauko Fisari wa Kahawa ya Robusta (*Robusta Coffee Wilt Disease*) unaofadhiliwa na Umoja wa *ICO*;

(d) Kuwezesha wakulima wadogo wa Kahawa wa Tanzania kunufaika na mafunzo yatakayotolewa na Umoja wa *ICO*; na

(e) Kuwezesha Tanzania, hususan, sekta ndogo ya Kahawa kupata taarifa zinazohusu maendeleo ya zao la Kahawa duniani zitakazokuwa zinatolewa na Umoja wa *ICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa 2007 utakuwa na matokeo ya kuwaongezea kipato wakulima wadogo wa Kahawa wa Tanzania na hivyo kuchangia katika kuwapunguzia umasikini na hivyo katika utekelezaji wa malengo ya *ASDP* na **MKUKUTA**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele muhimu vya Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 ni kama vifuatavyo:-

i. Majukumu ya Wanachama – Sura ya III. Wanachama wanapewa majukumu ya kushirikiana ili kuwezesha utekelezaji wa Mkataba, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa zitakazoratibiwa na *ICO* zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji;

ii. Mamlaka ya Usimamizi ya *ICO* kuongezwa – Sura ya V. Shirika la Kimataifa la *ICO* lililoanzishwa na Mkataba wa 1962 linaongezewa majukumu mapya ya uratibu na usimamizi, ikiwa ni pamoja na kufadhili miradi mbalimbali ya kuendeleza zao la Kahawa;

iii. Ukuzaji na Uendelezaji wa Masoko – Sura ya IX. Mkataba unatoa msukumo mpya katika suala la kukuza na kendeleza soko la Kahawa duniani. Mabadiliko makubwa yamefanyika katika Ibara za 24, 25, 26 ili kuondoa vikwazo vya kufikia masoko, kutangaza Kahawa ya nchi wanachama katika masoko mapya na kuhimiza uongezaji wa ubora; na

iv. Takwimu na Upatikanaji wa Taarifa – Sura ya XII. Katika Ibara za 32, 33 na 34 *ICO* imeimarishwa ili iweze kushughulikia taarifa na takwimu mbalimbali zinazohusu maendeleo ya zao la Kahawa kwa manufaa ya wanachama wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Ibara za 40 na 41 za Mkataba, Mkataba ulikuwa wazi kuanzia tarehe 1 Februari, 2008 hadi 31 Agosti, 2008 kwa ajili ya nchi wanachama kuutia saini kulingana na taratibu za kisheria za nchi husika. Aidha, nchi zilizotia saini zilitakiwa ziwe zimeridhia Mkataba huo kabla ya tarehe 30 Septemba 2009. Hata hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 41, nchi inayotarajia kuridhia Mkataba huo, ingeweza wakati wowote kutoa taarifa kwa Msajili kwamba itatumia Mkataba huo kwa muda, wakati inakamilisha taratibu zake za kisheria za kuuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu za kisheria za nchi yetu, Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inalipa Bunge mamlaka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohitaji kuridhiwa. Hivyo baada ya taratibu zote za kisheria kufuatwa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge lifuatalo la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka 2007 (*International Coffee Agreement, 2007*):-

KWA KUWA Tanzania ni nchi Mwanachama wa Umoja wa Wazalishaji na Watumiaji (*Producers and Consumers*) wa Kahawa Duniani, Umoja ulioanzishwa mwaka 1962;

NA KWA KUWA kutokana na mabadiliko ya Sera za Uchumi Duniani, mkataba unaotumika na Umoja huo umekuwa unafanyiwa marekebisho kila inapobidi na marekebisho makubwa yamefanyika mwaka 1983, 2001 na 2007;

NA KWA KUWA kwa kusaini na kuridhia na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2001 Tanzania iliweza:

a) Kupanua masoko yake ya Kahawa kutoka nchi za Ulaya na kwenda kwenye masoko ya Japani na Marekani.

b) Kuuza Kahawa yake yote inayozalishwa kwenye soko la kimataifa bila kikwazo tofauti na hapo awali ambapo kila nchi ilikuwa inapangiwa kiwango cha Kahawa cha kupeleka sokoni (*quota*).

NA KWA KUWA tarehe 28 Septemba 2007 kwa Azimio namba 431 la Baraza la Kimataifa la Kahawa (*International Coffee Council-ICC*) katika kikao chake cha 98 lilipitisha Mkataba wa 2007 kwa lengo la kufanyia marekebisho mkataba wa 2001;

NA KWA KUWA aya muhimu zilizoongezwa kwenye mkataba wa 2007 zinahusu maeneo yafuatayo:

a) Maswala ya maendeleo ya Kahawa kuanzia hatua za uzalishaji, usindikaji, masoko na ugharamiaji miradi ya maendeleo ya Kahawa;

b) Kuondoa vikwazo kwenye biashara ya Kahawa, kutangaza na kuendeleza masoko ya Kahawa na kutia kipaumbele katika usindikaji wa Kahawa; na

c) Uanzishwaji wa chombo cha majadiliano kuhusu masuala ya fedha katika sekta ya Kahawa (*Consultative Forum on Coffee Sector Finance*).

NA KWA KUWA pamoja na mambo mengine malengo makuu ya Mkataba wa 2007 ni kuimarisha sekta ndogo ya Kahawa duniani na kuwezesha upanukaji endelevu wa masoko katika mazingira ya soko huria kwa ajili ya manufaa ya washiriki wote katika sekta hiyo;

NA KWA KUWA kwa kusaini tu mkataba wa mwaka 2007 Tanzania imekwishaanza kunufaika na mkataba huo kwa kufadhiliwa kwa miradi mbalimbali inayohusu Kahawa, kwa mfano, Mradi wa Kuangamiza Ugonjwa Hatari wa Mibuni ya Robusta (*Robusta Coffee Wilt*)

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa mkataba wa mwaka 2007 kutainufaisha Tanzania katika nyanja tofauti ikiwa pamoja na:

a) Kupata masoko ya Kahawa nje ya nchi wanachama wa Umoja wa Kimataifa wa Kahawa (*International Coffee Organization - ICO*) kwa kuhamasisha unywaji wa Kahawa hasa nchi za mashariki za China na Urusi;

b) Kufanya bei za Kahawa ziwe nzuri, zenye kumpatia mkulima faida kutokana na mikakati iliyowekwa na Umoja wa Kimataifa wa Kahawa (*International Coffee Organization - ICO*) ya kuongeza ubora wa Kahawa;

c) Uwezekano wa kuongeza thamani kwa kuongeza mauzo nje ya Kahawa iliyosindikwa; na

d) Uwezekano wa kupata fedha kupitia Umoja wa Kimataifa wa Kahawa (*International Coffee Organization - ICO*) za kugharamia miradi ya maendeleo ya sekta ya Kahawa kwa nchi wanachama.

NA KWA KUWA Tanzania ni nchi mojawapo iliyotia saini Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 tangu mwaka 2008, Mkataba ambao umefanyiwa marekebisho Mkataba wa Kahawa wa mwaka 2001 ambao vilevile ulisainiwa na Tanzania tarehe 26 Januari 2001 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI Bunge hili katika mkutano wake wa kumi na nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, linaazimia Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 (*International Coffee Agreement – ICA, 2007*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nachukua nafasi hii kumuita tena Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mwenyekiti wake au kama kuna msemaji, ahsante Mheshimiwa Hilda Ngye atamwakilisha Mwenyekiti wa Kamati.

MHE. HILDA C. NGOYE (K.N.Y. MHE. GIDEON A. CHEYO –MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka wa 2007 (*The International Coffee Agreement, 2007*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana katika Ofisi ndogo ya Dar es salaam, tarehe 15 Januari, 2010, kuchambua Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka wa 2007 (*The International Coffee Agreement, 2007*), lililowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Dkt. David M. David, Mb, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa niaba ya Waziri wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa mwanachama wa Umoja wa Wazalishaji na Walaji wa Kahawa Duniani tangu umoja huo ulipoanzishwa mnamo mwaka 1962. Aidha, kutokana na mabadiliko ya Sera za Uchumi Duniani, Mkataba wa Umoja huo umekuwa ukifanyiwa marekebisho kila inapobidi, kwa mfano, marekebisho makubwa yalifanywa mwaka wa 1983, 2001 na 2007 yakiwa na nia ya kuongeza fursa mbalimbali kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kahawa ni moja kati ya mazao ambayo yamekuwa yakiliingizia Taifa fedha za kigeni na hivyo kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi. Zao la Kahawa pia huchangia asilimia 33 ya mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili linakusudia kuiwezesha Tanzania Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka wa 2007 (*The International Coffee Agreement, 2007*) ili kuiwezesha nchi kunufaika na fursa zinazotolewa ndani ya Mkataba huo ambao pia una lengo la kuimarisha sekta ndogo ya Kahawa duniani na kuwezesha upanukaji endelevu wa masoko ya Kahawa kwa manufaa ya wadau wote wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yaliyofanyika mwaka wa 2007 yalilenga kutangaza duniani kote ubora wa Kahawa ya wakulima wadogo kutoka nchi zinazoendelea; jambo ambalo linaipa nchi yetu fursa ya kuuza Kahawa yake katika masoko mapya ya China na Urusi. Aidha, marekebisho hayo ya mwaka wa 2007 yalianzisha chombo maalum kitakachoshughulikia masuala ya fedha na takwimu na yalioupa mamlaka Umoja wa Kimataifa wa Kahawa yenye lengo la kuongeza ubora wa Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuridhia Mkataba huu, nchi yetu itanufaika na miradi inayofadhiliwa na Umoja huo, kwa mfano, mpaka sasa Tanzania inanufaika na Mradi wa Kudhibiti Ugonjwa wa Mnyauko Fusari wa Kahawa ya Robusta (*Coffee Wilt Disease*). Aidha, Tanzania itanufaika na mafunzo yanayotolewa na Umoja wa Kimataifa wa Kahawa (*The International Coffee Organization*) na pia kuiwezesha sekta ndogo ya Kahawa kupata taarifa za maendeleo ya zao hilo zinazotolewa na umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na maudhui ya Azimio hili kwani lina faida kubwa sana kwa nchi yetu, hasa katika kipindi hiki ambacho nchi imeamua kukipa Kilimo kipaumbele cha kwanza. Kwa mantiki hiyo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu ilikubali kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba baada ya kuridhiwa kwa Marekebisho ya Mkataba huu, nchi yetu iweke mkakati wa kuiwezesha kutumia fursa zilizopo ili kuhakikisha:-

(a) Sekta ya Kahawa inakua kwa kuongeza tija ya uzalishaji na kupanua maeneo zaidi yanayolima Kahawa;

(b) Kahawa inayozalishwa ni ya ubora wa juu; na

(c) Kunapatikana masoko mapya na endelevu ya zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kwamba, kuwepo na usimamizi madhubuti wa kilimo cha Kahawa utakaohakikisha kwamba kanuni za kilimo bora cha zao hilo zinazingatiwa na elimu iendeleo kutolewa kwa wakulima ili kuhakikisha Kahawa yenye ubora wa juu inazalishwa ambayo itapata masoko yenye bei nzuri. Aidha, huduma za ugani ziboreshwe na ihakikishwe zinawafikia wakulima wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokuwa na viwanda vya Kahawa vya kutosha nchini, Kamati inaishauri Serikali iweke vivutio maalum vitakavyowashawishi wawekezaji kujenga viwanda vya kusindika Kahawa hapa nchini ili kuhakikisha Kahawa inauzwa nje baada ya kusindikwa na kwa hiyo kuongezewa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ni vyema Serikali iendeleo na utaratibu wa kuwapatia wakulima ruzuku ya madawa ya Kahawa ili kuhakikisha sekta hii ndogo inakua kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano wao waliouonyesha wakati wa kupitia Azimio hili. Napenda kuwatambua wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na mimi Cynthia Hilda Ngoye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa Dkt. David M. David, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Katibu Mkuu, Mohamed Muya, Naibu Katibu Mkuu, Sophia Kaduma pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa na kuwasilisha Azimio hili kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kasilillah, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi. Napenda pia kuwashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inaandaliwa na kukamilishwa kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 (*The International Coffee Agreement (ICA) 2007*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niendeleo kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah, kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Kuridhia Mkataba wa Mimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 (*The International Coffee Agreement (ICA) 2007*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 86 (6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu Azimio hili, Kahawa ni zao la kwanza kwa ukubwa kwa kulingizia Taifa letu fedha nyingi za kigeni lakini pia ni zao ambalo limekuwa likipambana na matatizo mbalimbali yakiwemo ya magonjwa, kuzeeka kwa miche ya Kahawa, lakini kubwa zaidi ni bei ya Kahawa katika soko la dunia imekuwa na ushindani mkubwa kutoka nchi mbalimbali, hasa zile za Latin America na hivyo bei yake kuwa inapanda na kushuka mara kwa mara jambo ambalo limekuwa likileta athari ya moja kwa moja kwa wananchi na kuwavunja moyo wakulima wa Kahawa kama ilivyotokea wakati wa mtikisiko wa kiuchumi duniani bei ya Kahawa ilishuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, zao hilo limekuwa likishambuliwa na magonjwa kutokana na kutokuwa na aina ya mbegu ambayo inaweza kustahimili magonjwa mbalimbali yanayosababishwa na kushuka kwa ubora wa Kahawa inayozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli uliowazi kuwa, hivi sasa Kahawa ndiyo zao la biashara hapa nchini linaloongoza kwa kulimwa katika Mikoa mingi na kwa kulinganisha na zao la biashara lolote hapa nchini. Kulingana na takwimu za Waziri ni kwamba zao hili huchangia asilimia 33 ya mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya Kahawa itakuwa na bahati sana hapa nchini kwanza kwa sababu ni wakulima wadogowadogo ndiyo wanaojishughulisha na kilimo hiki, lakini pili mikakati mingi iliyopo na ijayo yote inalenga kuinua kilimo hiki, hivyo basi vyanzo vingi vya fedha vitakuwa vinachangia katika kuinua kulifanya zao la Kahawa kuwa linazalishwa

na wakulima kwa kutumia njia bora za kisasa jambo ambalo michango ya fedha kutoka ndani na nje inaweza kutoa mwanya kwa wajanja wachache kujineemesha kwa fedha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kuhusiana na udhibiti mzima wa fedha hizo, hivyo inamtaka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alihakikishie Bunge hili Tukufu imeandaa mkakati gani wa kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na kulifanya Taifa la Tanzania kupitia zao la Kahawa kuwa kiongozi katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la dunia, Kahawa yenye bei nzuri ni ile inayozalishwa bila kutumia kemikali ya aina yoyote, *Organic Produced Coffee* hivyo basi Serikali baada ya kuridhia mkataba huu haina budi kuwahamasisha wakulima wetu kuzalisha kwa kutumia mbolea zetu za asili na kuzidi kufanya tafiti za kutumia madawa yanayotokana na mimea katika kutibu magonjwa yanayoshambulia zao la Kahawa na pia tafiti itakayotupatia aina mpya ya Kahawa inayostahimili magonjwa, mfano ugonjwa sugu wa Kahawa hapa Tanzania *coffee berry disease* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la dunia la Kahawa katika mnada unaofanyika katika soko la Moshi, Kahawa inayouzwa ni ile ambayo haijasindikwa na kuwa katika bidhaa inayotumika kwa mlaji wa mwisho, ili kuweza kuwa na wigo mpana katika soko hilo ni bora tukainua utalaamu wetu katika kutengeneza aina nyingi za Kahawa kwa mahitaji ya wateja katika pande zote za dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Mkataba huu; Ibara ya 6(2) cha mkataba kinachosema *the city of the organisation shall be in London*, kama inavyoeleweka Uingereza siyo wazalishaji wa Kahawa, wao ni watumiaji tu wa zao hili kama zilivyo nchi mbalimbali katika bara la Ulaya na kwingineko duniani. Hivyo basi ingekuwa ni bora mikutano na makao makuu ya Jumuiya hii yawe yanazunguka katika Kanda za nchi ambazo ni wazalishaji wa Kahawa kwa lengo kuu kuwa Wajumbe wa waweze kutembelea uzalishaji wa Kahawa na hivyo waweze kupata matumizi halisi ya fedha zitolewazo kwa maendeleo ya Tasmania ya Kahawa kwa nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imetoa pendekezo hili kwa sababu mara unapokuwa mwanachama wote tunakuwa sawa na hakuna mwanachama aliye na kura ya veto kwa kumzidi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkataba hauonyeshi ni kwa vipi unaweza kuwaingiza watumiaji wakubwa wa Kahawa kama vile nchi za Asia na Uarabuni katika kusaidia uzalishaji wa zao hili na wakati inapotokea majanga yatokanayo na athari za uzalishaji kwani tunaamini kuwa mchango wa nchi hizo ni muhimu kama ulivyo kwa nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mkataba huu, Kambi ya Upinzani imeridhika kuwa mkataba huu ni wa manufaa makubwa kwa tasnia nzima ya Kahawa hasa kwa wakulima wadogowadogo wa Kahawa ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa zao hili hapa Tanzania. Hivyo basi, haina sababu yoyote ya kutokukubali na kuridhia Azimio hili la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Salim Hemed Khamis kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji watatu tu ambao kwa kweli watatuhitimishia asubuhi ya leo. Kila mmoja atatumia muda wake ipasavyo na kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri atakuja kuhitimisha hoja hii jioni, niwataje kabisa ili waanze kujiandaa kuchangia. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi na tutamalizia Mheshimiwa Basil Mramba.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Azimio hili muhimu linalohusu zao la Kahawa, zao ambalo linalimwa sana katika Jimbo la Mbinga Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja hii na ingekuwa ajabu sana nisiunge mkono wakati hata Wapinzani wenyewe wameunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mkataba hapa, nimeusoma na nimeelewa, maudhui yake ni mazuri sana na ndiyo maana yanamilazimisha niunge mkono, kwamba na sisi Tanzania tuwe wamojawapo kati ya wale ambao tunatia saina katika mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda pia hasa kumpongeza mzawa mmoja kule Mbinga ambaye ana Kiwanda cha Kukoboa Kahawa anaitwa Danny Komba. Yeye ni Mtanzania Mwanambinga ambaye amejenga kiwanda kikubwa sana cha kukoboa pale Mbinga na hili Azimio pia linahamasisha katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda vingi vya namna hiyo. Pia ninapenda kuchukua nafasi hii kuwaalika wengine waweze kwenda mbele zaidi ya kukoboa lakini tuendelee katika mazao mengine yanayohusu Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze wakulima wa Mbinga ambao wamejitahidi sana kulima zao hili kwa muda mrefu na katika shida nyingi na niwape pole wakulima wa kata za Mkumbi, Litembo, Kitura, Myangayanga kwa sababu Kata hizo sasa zimeingiliwa na ugonjwa ambayo unaitwa Mdudu Ng'ata toka mwaka 2008 na mpaka sasa anaendelea kuwepo na kasi yake ya kuendelea kuwepo kule inaongezeka. Mimi leo nimefurahi Serikali imeleta mbele yetu Azimio hili, ni Azimio ambalo linaongelea juu ya uzalishaji zaidi lakini pia utunzaji bora zaidi wa ile miche na unywaji zaidi wa Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba wakati tunakubaliana na Azimio hili huku ndani tumejipangaje ili kuhakikisha kwamba Kahawa yetu inakuwa bora, tunapata nyingi zaidi na inakuwa bei nzuri zaidi, hili ndiyo tatizo letu kubwa. Hili Azimio ni zuri mno lakini sisi kama Serikali na Watanzania tuna-*take advantage* namna gani juu ya Azimio hili? Hii inaonekana wazi kwa wananchi wa Mbinga ambao wamelalamika kwa muda mrefu, nashukuru Naibu Waziri juzi alijibu kwamba atapeleka Wataalam kushughulikia tatizo hili la wadudu, huu kule ni msiba na hata Wanambinga sasa wamesema kule Mbagala Kuu Mabomu yalikopigwa, Serikali ilikwenda ikalia na wale wananchi, kule Kilosa yametokea mafuriko, zimetafutwa *billions of billions*, kwa nini Mbinga maana wanategemea Kahawa ikifa hawana chakula na hawana fedha lakini hatuoni hatua zinazofanana na hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kuwaomba waweze kuchukua hatua za dharura kuweza kuokoa janga hili. Jana nimesikiliza televisheni, Afisa wa Kahawa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, anasema kule Mbeya na Rukwa pako salama, mimi sina hakika kule Mbinga tulianza na Kata moja Mkumbi lakini imeenea katika Kata zingine na inaendelea kuenea. Uzalishaji wa Kahawa msimu wa 2007/08 ilikuwa tani elfu kumi na saba, uzalishaji wa Kahawa msimu wa 2008/09 umeshuka mpaka kufikia tani elfu tano, sababu mojawapo ni kwamba katika Kata hizi ambazo ni karibu hekari elfu mbili hazikuzalisha. Mimi kama Mbunge na mwakilishi wa wananchi sijaona hatua madhubuti zikichukuliwa, kweli Mheshimiwa Waziri alifika kule, walituma Wataalamu wakaleta mapendekezo lakini waliishia hapo tu katika mapendekezo, hawakuishia katika kutoa vitendea kazi na nyenzo za fedha ili kuwawezesha wale wananchi kuondokana na janga hili. Kwa hiyo kule tunayo msiba mkubwa sana wa jambo hili na *it is not a joke*, ningeomba Serikali ilitilie maanani jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunazo pia Sheria za Kahawa za mwaka 2000/01 ambazo mpaka leo utekelezaji wake ni mdogo sana. Hawa wakulima wetu wa Kahawa ili waweze kufanya vizuri, wanatakiwa wakopesheke na tukitaka wakopesheke ni lazima mashamba yao yaandikishwe na Sheria inasema hivyo na jukumu la kuwaandikisha ni la Bodi ya Kahawa lakini Bodi ya Kahawa mpaka leo haijachukua hatua, kwa nini kwa sababu uwezo wao kibajeti ni mdogo mno, wanataka kufanya mambo mengi lakini wameshindwa kwa sababu bajeti yao ni ndogo sana. Kwa hiyo, hili pia halifanyiki kwa hiyo tunapongea juu ya ubora wa Kahawa isiwe ni maneno, iwe ni vitendo zaidi na moja ya kitendo kizuri kitakachowakomboa wakulima hawa ni kuandikisha mashamba yao ili watambulike, nani Mbinga analima Kahawa nani Kilimanjaro analima Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la usafirishaji, kuna Sheria zinazotawala usafirishaji wa Kahawa, hizi Sheria haziangalii pia Kahawa inasafirishwa kwenye vumbi jingi lakini pia lipo tatizo la miundombinu. Nafurahi kwamba katika *Article 31* ya makubaliano haya inazungumzia kipengele cha fedha na ni mategemeo yangu kwamba Serikali itachukua *advantage* hiyo pia kuweza kutafuta fedha za kuongeza miundombinu ya barabara hasa katika maeneo yanayozalisha Kahawa. Kwa mfano eneo la Maguu na Langiro ambako Kahawa inatoka na Litembo barabara zake ni za vumbi, mimi nafikiri ingekuwa rahisi kuziweka lami ili tukapata zao lililobora zaidi. Kama lami inapita katika maeneo ambayo si ya uzalishaji sana kwa nini katika maeneo ya uzalishaji tusiweze kupitisha lami, tusiweze kuweka umeme ili waweze kutumia umeme huo katika kuanzisha kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unapopita katika baadhi ya maeneo unashangaa kwa nini umeme umepita hapa badala ya kupita sehemu ambazo kwa kweli zingeweza kuzalisha, sisemi kwamba wale wananchi hawastahili lakini *in terms of priority and economics* ndivyo zinavyotawala. Kwa hiyo, mimi ni tegemeo langu kwamba katika nyanja hizi za miundombinu sisi Tanzania kwa ndani tungeweza kuliwekea jambo hili mkazo na tuka-*take advantage* sasa ya Maazimio haya ili kuweza kupata *finance* ya kuweza kuendeleza miradi hii. Zipo fedha za *STABEX* lakini zamani zilikuwa zinasaidia sana katika barabara lakini sasa hivi hazipo kabisa, lakini *funding* zingine nasikia zipo, kwa hiyo tunayo matatizo kama hayo ambayo tunaweza tukayachukulia na tukasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana, ninaunga mkono Azimio la Serikali lakini ninaomba sana Waziri hapa aangalie ule msiba unaowapata Wanambinga sasa, kama zile tani zimefika tani elfu tano, mimi sijui msimu ujao zitafika tani ngapi, lakini la msingi ni wale watu wanakosa fedha, wanakosa chakula, ningepomba sana ahadi ya Naibu Waziri ambayo naiheshimu iweze kutekelezwa haraka sana, pengine hata kabla hatujamaliza Bunge hili ili na Wanambinga waweze kuonekana kwamba na wao ni sehemu ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo kufuatia Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 kama ulivyowasilishwa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze masikitiko yangu kwamba Azimio muhimu kama hili mpaka Waziri karibu anaanza kusoma taarifa hizi ndipo tunaanza kugawiwa. Mimi nadhani hili siyo jambo zuri sana kwa sababu hatupati nafasi ya kuyasoma haya Maazimio vizuri na kwa maana hiyo kutoa mchango wetu vizuri. Mimi naomba kwa baadaye Maazimio haya na taarifa nyingine za Serikali, Wabunge wapate mapema ili waweze kujiandaa kwa maana ya kutoa mchango unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo na mimi naomba niungane na wasemaji wa Kamati lakini pia na mwenzangu Kayombo kumpongeza sana Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Azimio hili na mimi sidhani kama kuna sababu kulikataa kwa sababu kimsingi ni jambo ambalo tulishaliridhia ni kwamba tunafanya hivi kwa sababu tu ya mabadiliko ambayo yameendelea katika sekta hii ya Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nami niseme mambo machache sana, Azimio ni zuri na mimi naomba niseme mwanzoni kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za Azimio hili, kwanza ni kuongeza masoko ya Kahawa duniani, jambo hili ni jema kwa sababu unapokuwa na soko kubwa maana yake kuna uwezekano pia mkubwa wa kupata bei nzuri ya Kahawa. Lakini hapa nataka nieleze wasiwasi wangu kwa wanunuzi wakubwa wa Kahawa duniani hasa wale watumiaji wakubwa, mara nyingi jambo ambalo mimi naliona wanapanga au wanakula njama, sijui neno zuri la Kiswahili lakini kuna kitu kinaitwa *syndicate*, wanajiunga pamoja kuhakikisha kwamba wanahujumu bei za zao la Kahawa hasa kwa nchi maskini kama zetu. Kwa hiyo, mimi nataka niombe Serikali wakati Azimio ni zuri na linasomeka vizuri, lakini nchi na wanunuzi wakubwa mara nyingi wanakula njama za kuhakikisha kwamba bei ya Kahawa inakwenda chini kwa maana hiyo kutomfaidisha mkulima. Ni kweli Azimio linaweza likawa limeandikwa vizuri lakini njama hizo kama tusipokuwa makini bado tunaweza tusishindane nazo kwa maana hiyo uzuri wa Azimio lote unaweza usionekane hasa kwa mkulima mdogo, kwa hiyo hilo lilikuwa angalizo kwa Serikali ili waweze kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nizungumzie na kama mkataba unavyosema na Waziri alivyosema ni suala linalohusu kuongeza ubora wa Kahawa. Kuna mambo kadhaa ili tuongeze ubora wa Kahawa; ni lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa na

Maafisa Ugani wa kutosha, hili ni jambo muhimu sana. Kuna mambo ambayo wakulima kama wakulima hawajashauriwa vizuri, bado uzalishaji wa zao la Kahawa hautakuwa mzuri. Mimi naomba niseme Waziri amekuwa anatuambia mara kwa mara, zipo jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba tunakuwa na Maafisa Ugani wa kutosha lakini mpaka leo kule Mbozi hasa Mashariki ambako tunalima Kahawa bado Maafisa Ugani wako wachache sana. Mbali ya kwamba wapo wachache, hata hawa ambao wapo wengine wanasoma fani mchanganyiko, unaweza kuona yupo Afisa Kilimo au Bibi Shamba au Bwana Shamba lakini bado siyo mtalaamu wa zao la Kahawa na wakati mwingine inashangaza unakuta mtu kasomea Korosho au mwingine kasomea chai, lakini yupo kule ambako wanalima Kahawa, kwa vyovyote vile ushauri wake kwa wakulima wa Kahawa unaweza usiwe mzuri sana lakini wakati tunafanya jitihada hizo tuangalie watalaamu ambao tunawapeleka kwenye kushauri zao la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa pia nilizungumzie ni lile linalohusu ubora wa Kahawa, leo tumeruhusu soko huria na mimi nimetafsiri soko huria kama soko holela, kwenye Kahawa leo ukienda kule Mbozi bila shaka na maeneo ambayo yanalima Kahawa, wanunuzi wameruhusiwa jambo ambalo ni zuri tu, ndiyo upanuzi wa soko lenyewe, lakini kuruhusu watu kununua Kahawa ghafi kumesababisha ubora wa Kahawa kwenda chini. Mtu anachuma Kahawa anaenda kuuza yule anayenunua hana utaalumu wa kahawa, hivyo maandalizi hayawi mazuri. Lingine tumesababisha wizi mashambani. Watu wanakwenda kuchuma Kahawa za wenzao mashambani au leo wewe umechuma Kahawa yako unaweka pale labda katika utaratibu wa kuikoboa kuna watu wengine wanaiba hili ni tatizo kubwa. Nashauri Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kukabiliana nalo, mimi sioni umuhimu wa kuruhusu ununuzi wa Kahawa ghafi kwa mazingira kama ya kwetu, sioni kama inasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nishauri, ni suala la miche bora. Tunazungumzia kuongeza ubora wa Kahawa, hebu tuwasaidie hawa wananchi ili waweze kupata miche bora. Mimi nina Kituo cha Kuzalisha Miche Bora pale Mbimba lakini uwezo wa kile kituo kwa ujumla ni mdogo, lakini pia tumeziambia Halmashauri za Wilaya zisaidie katika kuzalisha miche hii na kuuza kwa wakulima, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbozi inafanya hivyo, lakini bado uwezo wa Halamshauri ni mdogo kuweza kuzalisha miche ya kutosha kwa ajili ya kupeleka kwa wakulima. Kwa hiyo, naomba na hilo pia Serikali ijitahidi kuwapatia wananchi miche bora ili waweze kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nizungumzie ni uanzishwaji wa vituo vya kukoboa Kahawa na swali liliulizwa nadhani wiki iliyopita, Mheshimiwa Naibu Waziri Mathayo alilijibu. Mimi ninapenda nishauri zaidi lazima Serikali ihakikishe kwamba tunakuwa na Vituo vya Kisasa vya Kukoboa Kahawa na hili pamoja na kwamba limeanza, uwezo wa wakulima wetu wengi sio mkubwa sana. Zile mashine nyingi bado zinouzwa bei kubwa hivyo wananchi wetu wanashindwa kumudu kufanya manunuzi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ione kwamba na hilo tunaweza tukasaidia ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata hizo mashine na kwa maana hiyo kuanzisha vituo vya kukoboa Kahawa na hivyo kuongeza ubora wa Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mkataba tumezungumzia suala la kuongeza thamani ya Kahawa yenyewe, kwa maana ya kwamba badala ya kuuza Kahawa ghafi nje, basi tujitahidi hiyo Kahawa tuisindike hapa nchini ili Kahawa iweze kuongezwa ubora na kwa maana hiyo

kuweza kupata bei nzuri. Sasa hili mimi nilipenda niishauri Serikali najua haifanyi biashara, lakini ni vizuri pia Serikali ikalisimamia na kuwahamasisha wawekezaji wengi kujenga viwanda vingi vya Kahawa katika nchi hii ili iweze kukobolewa, iweze kukobolewa na kusindikwa na kwa maana hiyo inapouzwa nje, basi iuzwe ikiwa imesindikwa kuliko tunazalisha sana Kahawa lakini yote tunayoiuza nje inakwenda kuwa *processed* baadaye inarudi tunauziwa sisi ambao tulima. Mimi nadhani jambo hili Serikali ilitilie maanani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nilizungumzie ni suala la kuwaongezea wananchi kipato. Katika utaratibu wa sasa wa soko huria tunawaongezeaje wananchi hawa kipato wakati wanunuzi wanakula njama na kupanga bei? Mwananchi wa mwisho anayelima na kuiuza, anapata tabu sana kwa sababu kama makampuni yako kumi yote yanakula njama kwenye bei ya Kahawa. Kwa hiyo, ninaomba hili kwa sababu nia hapa ni kuwaongezea wakulima hawa wadogo kipato, kama hatuwezi kusimamia kule kwa mkulima, bado mkulima huyo ataendelea kuumia na watakaofaidika ni wanunuzi wa kati ambao ndio wengi wanakwenda kuuza Kahawa kule Moshi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilianganalie hilo kama tunasema mkataba huu una nia kwa kweli kuongeza au kupanua uzalishaji wa Kahawa kwa wakulima wadogo wadogo lazima Serikali ilisimamie hilo vinginevyo tutakuwa hatuwezi kuwasaidia wakulima wetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia ni suala la kuisisitiza matumizi ya mbolea kama alivyosema Msemaji wa Upinzani na wasemaji wengine, sisi kule Mbozi huwezi kulima Kahawa bila kutumia mbolea, haiwezekani hata kidogo. Lakini imekuwa bahati mbaya sana sisi wengine tuko humu ndani kwa sababu ya Kahawa lakini huyu mkulima kimsingi hajasaidiwa sana, kwa sababu bei ya mbolea ni kubwa na kule Mbozi mbolea ambayo tunaitumia ni mbolea aina ya *CAN*, ninajua kuna mazao mengine ya biashara ambayo wamepewa ruzuku ya mbolea nadhani wenzangu kwenye korosho wanapewa ruzuku ya mbolea, mimi nasema kama kuna mazao mengine ambayo wanapewa ruzuku ya mbolea kwa nini tusifikirie kuwapa wananchi wanaozalisha Kahawa ruzuku ya mbolea ili waweze kuzalisha kwa wingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hapa tunazungumzia kumpa huyu mwananchi uwezo wakati tunazungumzia kumpa uwezo lazima tuangalie je, hii bei iliyopo leo mwananchi anaiweza na tuchukulie mfano tu Mwenyekiti, kama unalima hekta tano, ukahitaji kutumia mbolea mifuko mitano ya *CAN* au mifuko kumi kwa maana ya hekta tano, mkulima huyu anahitaji kwenye mbolea pekee yake si chini ya milioni moja kwa sababu katika utaratibu wa Kahawa lazima uweke walau mbolea mara mbili, sasa mkulima yupi anaweza kama asiposaidiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wakati mwingi tumekuwa tunasema kwamba uwezo wa Serikali ni mdogo ndio sababu tunatoa ruzuku kwenye mazao pengine ya chakula. Lakini tuangalie hata huku kwa sababu mazao haya ndio yanayochangia pato kubwa la Serikali na kama Waziri alivyokiri zao la Kahawa linachangia asilimia 33 katika pato la Taifa, kwa hiyo lazima tuweke mazingira mazuri kwa mkulima huyu anayelima zao la Kahawa ambalo linaingiza Taifa hili fedha nyingi sana za kingeni. Kama hilo likitekelezwa tutakuwa tunawasadia wakulima na tutakuwa tunaenda na *spirit* ya Azimio lenyewe ambalo linalenga kumwongezea uwezo mkulima

huyu mdogo ili aweze kuzalisha Kahawa hii vizuri zaidi na kwa maana hiyo ili tuweze kuchangia pato la Taifa kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niseme na kama nilivyotangulia kusema naunga mkono Azimio hili ili liweze kupita na liweze kutufaidisha kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametueleza, nakushuru sana. (*Makofi*)

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze tena kwa kuunga mkono Azimio hili na nazungumza kutokana na uzoefu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro na hususani Wilaya ya Rombo na niseme mimi ni mkulima mdogo wa Kahawa. Kwa hiyo, ninazungumzia jambo ninaloishi nalo na nimeishi nalo toka nizaliwe mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopitia lilikuwepo swali hapa la mambo ya Kahawa ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti nilipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nataka sasa nitumie fursa hii kufafanua zaidi msingi wa lile swali langu la nyongeza ambalo nilijibiwa vizuri na Naibu Waziri kwa kusema wanalichukua wazo lile ambalo nilikuwa nimelisemea kwenye swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Desemba, *RCC* ya Mkoa wa Kilimanjaro ilikutana kutafakari pamoja na mambo mengine uendelezaji wa zao la Kahawa. Inavyoonekana, pamoja na juhudi zote ambazo zimefanywa bado zao la Kahawa haliendelei kwa kasi inayotakiwa katika Mkoa ule. Malengo tuliyokuwa tumepeana kwa kweli hatuyafikii. Tulikuwa tumepeana kitaifa, mtakumbuka wakati ule Mheshimiwa Lowassa akiwa Waziri Mkuu aliita Wakuu wa Wilaya za wakulima wa mazao mbalimbali na kuwapa malengo. Sisi kwenye Kahawa tulipewa lengo lakini hatujalikaribia hata kwa nusu na nataka nisaidie kidogo kwa nini hatujafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza habari ya kwenda kuuza Kahawa na wanachama wengine wa *ICO* lakini tutauza nini sisi, Kahawa yetu haijaongezeka sana na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Mbinga, janga linalonyemelea kule Mbinga likiendelea itakuwa bahati mbaya kabisa tena itakuwa mbaya kwa Tanzania maana yake ni kwamba Kahawa Tanzania itazidi kuteremka; kiasi cha uzalishaji kitazidi kuwa chini na kama mdudu yule naye angehamia Mbozi ndio kabisa tutakuwa tumekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kupendekeza namna tunavyoweza kutumia zaidi hili soko litakalopatikana kutokana na uanachama wetu kwenye *ICO* na ndivyo Mkoa wa Kilimanjaro tulivyoamua kupendekeza Serikalini na sasa nalisema rasmi kwa niaba ya wenzangu wa Mkoa na kwa niaba yangu mwenyewe kama mkulima mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kazi nzuri imefanyika kule *TACRI* kuzalisha mbegu bora au miche bora lakini wanalalamika sana hawana miche ya kutosha. *TACRI* wamesambaza utaaalam kwa wakulima wadogo ngazi ya Wilaya. Kule kwetu tumeanzisha bustani ndogo ndogo za wakulima fulani fulani pamoja na vituo kama vile vya Makanisa ili tutoe mbegu kwenye vituo hivyo vidogo vidogo na kupeleka kwa mkulima mmoja mmoja. Tulimuonyesha Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka juzi alipotutembelea akaona mwenyewe na akatoa maagizo fulani fulani. Tatizo la agizo lile la Waziri Mkuu ni kwamba tukazanie sana kutumia *DADPs* kupanua zao hili, hata *DADPs* nazo ni *limited*; huwezi kuwa na *DADP* ya kila kijiji, kila mwaka inaonekana, hapo

napo kuna tatizo na tatizo ni bajeti ya Wizara; labda sasa bajeti ya Wizara iongezeke. Kwa hiyo kuna upungufu mkubwa kabisa kabisa, ni *crisis* ya miche na kama huna miche huwezi kuendelea. Kwa hiyo, tumekwama. Kwanza hatuna miche, mimi ilibidi niende kuomba wafadhili wanisaidie tuweze kupanua vitalu hivi ili tupate miche zaidi. Lakini wafadhili wangapi watafanya jambo hilo. Labda nishukuru Kampuni ya Bia Tanzania ilitupa fedha kwa ajili hiyo na nataka niishukuru rasmi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ambalo ni kubwa kabisa mche ule unauzwa mmoja shilingi 1500, shilingi 2000, 2500 mkulima hawezi kununua miche mingi kwa sababu hana fedha, mkulima mdogo huyu. Kwa hiyo, ni lazima miche hii iwe *subsidized* kama tunataka ku-*break through*, miche hii iwe *subsidized* au itolewe bure kabisa au itolewe kwa mkopo wa masafa marefu yaani alipe baada ya miaka mitano, mmea wenyewe utakapoanza kuzalisha. Lakini lazima tutafute jibu la hii bei ya miche hata kama ingepatikana kwa wingi lakini bei ni kubwa sana kwa mkulima wa kawaida hawezi. Mche ule kwa teknolojia ya sasa na aina mpya ya kahawa kutoka *TACRI* kwa bahati nzuri matumizi ya dawa sio makubwa kama ilivyokuwa kwa ile aina ya Kahawa ya zamani ni kidogo zaidi lakini bado bei ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunahitaji ku-*subsidize* vitu viwili yaani mbolea na madawa na mimi naunga mkono na kule Mkoani tumeliona hilo katika *debate* hiyo ya kutafakari hatima ya zao la Kahawa; tuliona kwamba Kahawa inakubaliana sana na samadi. Bahati mbaya sisi kule sio wafugaji wakubwa kwa hiyo hatuna hata samadi. Sisi Rombo huwezi kuamini tunaagiza samadi kutoka Kenya; tatizo ni (*transport cost*) gharama ya usafirishaji, kwa hiyo samadi ile ikifika kijijini ni ya ghali, mkulima mdogo hawezi kulipa gharama hiyo ingawa bado ni nafuu kuliko mbole za chumvi chumvi. Kwa hiyo, sasa wengine tunaanza kutumia Minjingu *Phosphate* na kidogo samadi tunachanganya hivyo hivyo lakini hatuna uhakika wa mbolea na kama huna uhakika wa mbolea ndio hivyo umeshakuwa mkulima ambaye hujakaa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunahitaji ili tuweze kuwa sawasawa kabisa ni mashine zile ndogo ndogo za kumenya Kahawa. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu tulimuonyesha baadhi ya mashine zile pamoja na banda lake na chekecheke zake zile; sio chini ya shilingi milioni 10 au 15, kwa kutegemea saizi. Hizi zinanunuliwa kwa sasa hivi kwa utaratibu wa kuibua miradi kupitia *TASAF* au *DADP* lakini ni kidogo sana yaani ni tone. Kwa hiyo, tunahitaji Serikali *some how* au kwa utaratibu huu au kwa utaratibu wa kukopa fedha benki au programu maalum. Tunahitaji mashine hizi hata kama hamuwezi kutupa bure tupeni mkopo basi kupitia *SIDO* au kupitia ule mfuko wa *JK directed* kabisa kwa Kahawa ili kusudi tujue kwamba kwa kupitia *SIDO*, kwa sababu *SIDO* wana uzoefu mkubwa wa mambo wa *hire purchase*, kukopesha na kulipa kidogo kidogo basi wakipitisha kule sisi tunaenda kuomba mikopo, tunasaini halafu tunalipa kidogo kidogo labda baada ya miaka mitano au miaka fulani.

Lakini sasa hivi kuna upungufu mkubwa hata ile Kahawa ya zamani tu tunaendelea kuimenya kizamani ambapo bei inakuwa ni ndogo na kila mtu kule anajua kwamba Kahawa nzuri ni ile iliyomenywa *kwenye central pulperies* mimi naita *village pulperies* ndogo ndogo. Ukifanya makubwa mno tena watu watabeba mizigo kichwani kwenda kilomita saba kwenye *pulpery* haifai lazima wamenyee karibu karibu. Kwa hiyo, tunahitaji *village pulperies* na hizi hazitengenezwi huku nchini lakini zingeweza zikatengenezwa, hazina maajabu zile *pulperies*, ni suala la kutafuta Makalasinga na watu wengine watazitungeneza tu hizi. Kwa sasa hivi

zinaagizwa kutoka Brazil, zinaagizwa kutoka Kenya na mimi nafikiri humu humu ndani ya nchi tungeweza tukazitengeneza kwa sababu hazina *complications* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa tutahitaji vikundi kwani Serikali/Wizara haiwezi kushughulikia mkulima mmoja mmoja, kwa hiyo, tunahitaji vikundi. Kule kwetu bado vile Vyama vya Ushirika vya zamani vipo na tunavitumia kuuzia Kahawa hiyo ya *grade* nzuri hata ile ya *grade* hovyoyovyoyo bado tunauzia huko kwenye *cooperative*, wao wanajua jinsi ya ku-*grade*. Lakini vilevile *Farmers Associations*, kule kwetu tumeweza kuanzisha vikundi vinavyoitwa *Special Coffee Farmers Associations*. Niko kwenye *association*, niko kwenye *cooperative* na ziko tofauti za bei lakini hizo sio za hapa; hiyo tusizungumze hapa lakini wakulima waanzishe *associations* kule ambako ushirika una matatizo na mimi najua maeneo mengi ya wakulima wa Kahawa ushirika bado una matatizo. Lakini kule Kilimanjaro bado ushirika uko kwenye damu yetu; lakini tunahitaji kusaidiwa sasa ili tuweze kuzalisha kwa wingi ili vyama hivi navyo viweze kuwa *viable*. Pale wasipotaka ushirika tungeweza kuanzisha *Special Coffee Farmers Associations* na zikasaidiwa kwa utaratibu wa *extension* na zikaweza kutoa Kahawa nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote haya maana yake ni nini? Yote haya niliyosema maana yake ni kwamba tunahitaji *a special program*, programu maalumu ya wakulima wa Kahawa, *specially funded* kwa *item* zote hizo nilizozungumza na ambazo kwa kutumia *Extension Officers*, tunaweza basi tukaongeza uzalishaji kwa wingi tena uzalishaji wa Kahawa bora, Kahawa ya kisasa na wakulima wakaweza kuongeza kipato. Tusipofanya mambo haya kama ni *intergrated program*, kuzungumza habari za kuongeza zao la Kahawa na ubora wa Kahawa na kuingia huku *ICO* kutakuwa hakuna maana kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo rai yangu na rai ya wakulima wa Kahawa Tanzania nadhani lakini kwa vyovyote vile Kilimanjaro, ni hiyo kwamba kila Mkoa wenye Kahawa kuwe na programu inayolingana na mazingira ili tuweze kuongeza uzalishaji wa zao hili kama tulivyoelekezwa na Serikali miaka mitatu minne iliyopita ili tuweze kuongeza kipato cha mkulima wa kawaida, mkulima mdogo wa Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii na nafikiri Waziri amenisikia, haya ndiyo nilitaka kusema wiki iliyopita nikakosa muda. Kama anataka tuzungumze zaidi mimi nina muda kabisa wa kuzungumza zaidi ili mradi tupate hiyo programu. Kama hakuna huko kwenye bajeti tukope hata fedha kwa sababu Kahawa ndilo linalotuletea fedha za kigeni kuliko zao lingine lolote. Nchi hii fedha za kigeni zinatoka kwenye Kahawa na korosho na sisi sasa kwa sababu ndio ng'ombe wetu wa maziwa lazima tumtunze vizuri, aendelee kutoa maziwa kwa wingi, lakini ukimkondesha ng'ombe wa maziwa sasa utakunywa maziwa gani? Naomba kuunga mkono hoja na nashukuru kwa fursa hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Waziri amekusikia.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na timu yake yote, kwa kuleta *Protocol* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kuunga mkono na kusisitiza juu ya tatizo linalowakabili wananchi wa Mbinga juu ya ugonjwa wa Kahawa aina ya Arabika inayopatikana Mbinga. Tunacho kituo cha utafiti TACRI, wanajitahidi lakini tatizo hili la ugonjwa ni tishio na nadhani ni sawa na janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *traceability*, tunashukuru *TIRDO* waliweza kutoa mafunzo ya awali juu ya mfumo huo. Kwa kuwa zao hili limeanza kulimwa siku nyingi, yawezekana inahitajika utafiti wa kina katika kutatua matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia Wizara kila la kheri na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, michango yenu kwa kweli ilikuwa mizuri sana, nitampa muda Waziri ili aje ahitimishe hoja jioni na kwa kuwa muda tulionao pia hamruhusu mchangiaji mwingine yoyote kuendelea, naomba nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 06.56 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Job Y.Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Wasira.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii tena ili niweze kuhitimisha hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusiana na Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kahawa wa Mwaka 2007. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii ya Azimio ya Kuridhia Mkataba wa Kahawa. Wabunge waliochangia hoja hii, wako sita, kwanza amechangia Mwenyekiti au mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, Mheshimiwa Hilda Ngoye, halafu Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Basil P.Mramba, Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na Mheshimiwa Stella Manyanya amechangia kwa maandishi. Hao ndiyo waliochangia kwa maandishi na hoja ambazo zimezungumzwa katika mjadala huu, zote zimeunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kazi yangu itakuwa ni kutoa ufanunuzi wa masuala kadha ambayo yameongelewa. Liko suala kubwa ambalo limezungumzwa na Wanakamati likiwakilishwa na Mheshimiwa Hilda Ngoye, vile vile Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Basil Mramba, wote wamezungumzia sana suala la mkakati wa kukuza na kuendeleza zao la Kahawa. Ninapenda niseme tu kwamba tumepokea ushauri wao, lakini maamuzi ya kutengeneza mkakati na programu ya kuendeleza zao la Kahawa kwa miaka mitano

ijayo, yaani mwaka 2010 - 2015 ulipitishwa katika kikao cha wadau kilichofanyika Arusha tarehe 30 Novemba na tarehe 1 Disemba mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya mkakati huo yameanza sasa kwa kuzingatia malengo ambayo yaliwekwa na kikao hicho. Malengo yaliyowekwa, kwa kweli na kikao hicho cha wadau, ambacho kilikuwa cha kwanza kabisa tulipopitisha sheria inayowapa wadau mamlaka maalum ya kusimamia zao linalowahusu ni pamoja na kukuza na kuendeleza zao la Kahawa katika Mikoa inayolima Kahawa kwa sasa ni Mikoa sita mipya yaani Manyara, Tanga, Morogoro, Iringa, Rukwa na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao hiki cha wadau ambacho mimi mwenyewe nilipata fursa ya kuhudhuria, kiliwaleta wadau kutoka katika maeneo mbalimbali na kwa kweli walifika mahali wakayazungumza na kukubaliana kujaribu kadri inavyoweze kuanza kuongeza tija ya uzalishaji wa mibuni kutoka wastani wa kilo mia nne za sasa hadi kufika kilo elfu moja, huo ni mkakati. Lakini vile vile mkakati wa pili ilikuwa kubadilisha miche ya zamani na kupanda miche mipya inayofanyiwa utafiti na TAKRI zenye ukinzani wa magonjwa na yenye kutoa mavuno kwa kiwango kikubwa na vile vile kupeleka huduma za bodi karibu na wakulima kwa kufungua ofisi za bodi katika kanda mbalimbali ambako zao hili linalimwa na kuongeza ubora wa Kahawa kwa kuzingatia mnyororo wa uzalishaji. Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo yameamuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Basil Mramba kama mkulima mwenyewe amesema ni mkulima mdogo, lakini siamini kama atakuwa mdogo hivyo, kwa hiyo ninamshauri tu kwamba bado hoja iko wazi tu, tunamkaribisha sisi Wizarani aweze kutoa ushauri wake zaidi kwa masuala yoyote yale ambayo yeye anafikiri tukiwachukua au kuyatekeleza, yatasaidia kuongeza uzalishaji wa zao la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoweza kusema ni kwamba Serikali tunataka kuona zao la Kahawa linaongezeka kwa namna peke yake ya kuongeza uchumi wa nchi yetu kupitia kilimo na vile vile kusaidia kupunguza umaskini katika jamii ya watu wanaolima Kahawa, ni kuwasaidia wakulima hawa waweze kuongeza uzalishaji kwa hekta badala ya kutegemea upanuzi tu wa mashamba yao. Kwa hiyo, suala hili tunalipa kipaombele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile naliunganisha na suala zima la Kilimo Kwanza kwamba tunao mfumo sasa hivi wa *ASDP* na *DADPs* katika ngazi ya Wilaya. Mahali ambapo mimi nimetembelea kwa mfano kule Mbinga na Kigoma, katika Wilaya ya Kibondo, nimekuta mahali ambapo fedha za *DADPs* zimetumika kuweka mashine hizi ndogondogo za kukoboa Kahawa ili kuongeza thamani na mimi naamini fedha hizi zikitumiwa na kama Kahawa ni zao la umuhimu wa pekee katika Wilaya inayohusika, hakuna sababu kwa nini fedha hizo zisielekezwe katika kuwasaidia wakulima katika kuongeza uzalishaji wa miche ili waweze kupata miche ya kutosha na waweze kuongeza uzalishaji wa zao la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yalikuwa ni mawazo mazuri ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Basil Mramba, Godfrey Zambi ambaye alikuwa anahoji tunafanya nini, tumejipanga vipi katika kufikia azma ya kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Salum Khamis Salum alihoji mambo kadha ambayo kwanza, alizungumzia juu ya Kahawa inashambuliwa na magonjwa na hili vile vile limezungumziwa kwa nguvu sana na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, aliyekuwa anazungumzia ugonjwa; yeye nitaeleza hoja yake maalum kwa ajili ya Mbinga wakati unaofuata baada ya kumaliza kuzungumzia hoja za Mheshimiwa Khamis au nitalijibu hilo pamoja na la Mheshimiwa Kayombo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bei kushuka na kupanda, hii nadhani tunajua kwamba sisi ni wazalishaji wa mazao ambayo yanauzwa kwa kutegemea utashi wa soko na kwamba soko likiwa na Kahawa nyingi zaidi *tendency* huwa ni bei kushuka lakini Kahawa ikiwa kidogo na hasa ikitokea madhara katika nchi zinazozalisha Kahawa kwa wingi kwa mfano Brazil, basi bei kwa kawaida inapanda. Lakini faida moja tunayopata kwa kuridhia hoja hii, ni kwamba sasa soko la Kahawa litapanuka, nchi kama Urusi na China ambazo zilikuwa haziko katika soko la kawaida la Kahawa, sasa zitaingia chini ya mpango huu na hiyo maana yake ni kwamba mahitaji, yaani *demand* itaongezeka na *demand* ikiongeeka bei zinaweza ku-*stabilise* kutokana na wingi wa watumiaji wa zao la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano China, kama mnavyojua kuna watu zaidi ya bilioni moja ...

MBUNGE FULANI: Trilioni.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Bilioni moja sio trilioni, trilioni ni wengi maana dunia nzima haina watu trilioni, bilioni moja, sasa ikiwa Mchina mmoja ataingia kwenye soko na akanywa kikombe kimoja tu cha Kahawa, naamini hapatakuwa na Kahawa ya kutosha duniani. Maana hawa ni watu wengi sana kwa kweli na ni soko ambalo linatazamwa na watu wengi. Kwa hiyo, makubaliano haya yanatuingiza kwenye soko la Urusi na China, hiyo peke yake ni hatua ambayo inatusaidia kuwa na uhakika kidogo juu ya hali ya bei katika siku zinazokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na mbegu ambazo zinastahimili magonjwa, labda hili ni suala ambalo limefanikiwa sana kutokana na utafiti ulioendeshwa na kituo chetu cha TAKRI. Utafiti huu umechukua muda mrefu, lakini hatimaye tumeweza kupata mche wa Kahawa ambao unastahimili magonjwa na ambao hauhitaji matumizi makubwa sana ya madawa kama ilivyokuwa kwa ile mbegu yetu ya zamani. Kwa hiyo, nadhani maelezo yake yapo na kwa kweli miche ndiyo pungufu, lakini miche inayostahimili magonjwa ndiyo hii ambayo imepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba fedha za Kahawa zilindwe ili zimfikie mkulima, hili ni jambo tunalikubali, lazima tuchukue hatua ya kuhakikisha kwamba fedha zinazotoka *ICO* kwa ajili ya maendeleo ya zao la Kahawa, lazima zitumike kwa makusudi yaliyokusudiwa. Mara nyingi fedha hizi, huwa zinakuja kwa miradi. Miradi imejulikana na fedha kiasi gani zinajulikana, zinapelekwa kwa walengwa, kwa ajili ya kutimiza azma iliyokuwa imekusudiwa,

lakini ni jambo jema kukumbushana kwamba fedha za umma zinazolingia kwa ajili ya kazi maalum zitumike kwa kazi hiyo kwa manufaa ya waliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kahawa *organic* ni zuri na sasa soko la *organic* linaendelea kukua hatua kwa hatua, lakini kama ulivyomsikia Mheshimiwa Basil Mramba, Kahawa inahitaji mbolea, yeye anasema kule wanatoa mbolea kutoka Kenya, sasa ukisema *organic everywhere* unaweza kweli ukashusha *production* badala ya kuipandisha. Kwa hiyo, sisi tunachosema ni kwamba kule ambako wanaweza kulima Kahawa bila kutumia *chemicals* na wakatoa Kahawa ambayo ni *organic*, tunawatia moyo kufanya hivyo, kwa sababu soko la *organic* linaendelea kukua, lakini bado soko la kawaida la Kahawa ni la Kahawa zote na kubwa zaidi ni *non-organic* kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti wa magonjwa na tatizo la *CBD*, hili tatizo la *CBD* ni la kutumia madawa na utafiti uliyofanyika wa kupata miche mipya ndiyo jibu kwa *CBD*. Tutakapokuwa tumeweza kueneza miche yote ya Kahawa, hii mipya, basi tutakuwa tumeshaondokana na tatizo la ugonjwa huu wa *CBD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la Kahawa ni la Kahawa ghafi na sio inayosindikwa. Kwa sasa hivi Kahawa nyingi inayouzwa ni ile ambayo ni ghafi na hili ni jambo ambalo ndiyo hali halisi ya sasa, huko mbele ya safari basi tutajua kitakachotokea.

Mheshimiwa Khamis alihoji kwa nini Makao Makuu yawe London na kwa nini mikutano isiwe inazunguka. Kwanza unajua umoja wa *ICO* ni wa walaji na wakulima; na walaji sio watu wadogo sana kama unavyowafikiria. Kwa hiyo, waliamua sasa Makao Makuu yatakuwa London lakini mikutano yote haifanyiki London, kwa mfano mkutano wa mwaka huu 2010 utafanyika huko Amerika ya Kusini, mkutano wa mwaka kesho utafanyika *Ivory Coast*, Afrika. Kwa hiyo, mikutano ile ina-rotate, lakini Makao Makuu yanakuwa yako pale pale Uingereza na hakuna athari yoyote ya kuwa na Makao hayo hapo Uingereza, maana yako hapo na wote tunayatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Gaudence Kayombo ambalo vile vile liliandikwa na Mheshimiwa Stella Manyanya kwa maandishi, linahusu ugonjwa wa vidung'ata ambao umeanza kuonekana katika eneo lile la Mbinga. Ninapenda kusema tu kwamba huu ugonjwa sio mpya, uliwahi kutokea tena mwaka 2006 na *TACRI* pamoja na wataalamu kutoka Wizara yangu, walishirikiana katika kushughulika na ugonjwa huu na ukatoweka mwaka ule wa 2006. Sasa umerudi tena na hivi tunavyoongea wataalam wa Wizara yangu na wataalamu wa *TACRI* wako Mbinga kufuatilia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda kusema tu kwamba tatizo ambalo wataalamu wanatuambia ni hakika, ni kwamba ule ugonjwa unaweza ukaisha ikiwa kila mkulima itazingatia kanuni za kilimo bora cha Kahawa na hata hali ilivyo katika maeneo yale ambayo yameshikwa na ugonjwa huu, ukienda ukikuta mkulima ambaye anazingatia kanuni za kilimo bora unakuta shamba lake liko sawa lakini ukienda kwa yule ambaye hakuzingatia ndiyo unaukuta huu ugonjwa. Kama wakulima wote wangezingatia kanuni za kilimo bora huu ugonjwa unatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli kazi ambayo iko mbele yetu pale ni kuwashauri wakulima wa Mbinga na kwingine kote kule ambako ugonjwa huu unaweza ukafika maana unaweza ukafika mahali popote, wazingatie kanuni ya kilimo bora. Yako mambo yanafanyika huko si mazuri sana hata kueleza, kwa mfano mkulima anafikiri anaweza kupunguza gharama kwa kutumia madawa ya pamba kunyunyuzia Kahawa. Sasa akifanya hivyo anavunja kwa kweli kanuni ile na wakati mwingine anauwa wadudu ambao ni adui wa wale wanaoeneza ule ugonjwa baadala ya kuwahifadhi ili wasaidie kupunguza tatizo. Jambo hili tunawatuma wataalamu wetu kwenda Mbinga huko, wako tayari kule na tutaendelea kufuatilia hatua ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kayombo alizungumzia juu ya miundombinu, nadhani alikuwa anazungumza juu ya barabara za vijijini, hii nadhani ni mambo ambayo yanashughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia *DADPs* na kutumia programu za kawaida za Serikali za Mitaa juu ya kupambana na ugonjwa huo. Lakini sisi tukipata fedha za Kahawa ambazo zinaweza zikasaidia katika Wilaya fulani kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya barabara, hatutasita kusaidiana na Halmashauri ya Wilaya katika kuendeleza barabara za vijijini na kuhakikisha kwamba mazao ya wakulima yanafika kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zambi alisema Serikali ihimize uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda vya kukoboa na kusindika Kahawa, tunakubaliana naye na Serikali tunaendelea na kazi hii, lakini vile vile tunaomba wakulima waanze kutumia mashine zile ndogondogo za kukoboa ambazo zinasaidia kuwapa soko zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi itekelze sheria na kwamba *i-register* wakulima, tunakubalina na Mheshimiwa Kayombo na tunaanza kazi hii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya zote zinazolima Kahawa ili tujue ni nani hasa analima Kahawa na nani halimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na hoja kwamba watu wananunua Kahawa mbichi na kukawa na hoja ya kutaka wapigwe marufuku. Mimi nadhani, marufuku yake ni kuwafanya wakulima wawe na zile mashine za kukoboa, kwa sababu watakuwa wanachuma, wanakoboa na wao wenyewe watagundua kwamba kwa kufanya hivyo bei na thamani ya zao lao linaongezeka. Kwa hiyo, hii inaweza ikawa ni *policy* nzuri zaidi kuliko kusema tunapiga tu marufuku kwa mdomo, kinachotakiwa ni hatua zitakazomfanya mkulima huyu aone kuna *incentive* ya ku-*process* na kupata bei nzuri kwa zao lake.

Mheshimiwa Basil Mramba nimeshaeleza programu ambayo imeandaliwa na wadau na nimeshasema kwamba tunamkaribisha aweze kutupa mawazo zaidi ikiwa yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabla ya mwisho ni la miche, miche inayozalishwa *TACRI* haitoshelezi mahitaji na kwamba bei ya hiyo miche ni kubwa, labda nisema tu kwamba Serikali tunatoa fedha kwa *TACRI* kwa nia ya kutaka wazalishe miche mama ya kutosha ili kutoka hapo kwenye mashamba ya miche mama ya *TACRI* vikundi mbalimbali vipate miche vikazalishe miche kwa ajili ya wakulima hivyo ndivyo tunavyofanya na kwa kweli wanaopata miche kutoka kwa *TACRI* wanaipata kwa bei ya nafuu kwa sababu ya *subsidy* ya Serikali kule *TACRI*. Lakini labda tulichojifunza sio hapa tu ni kwamba wale wanaochukua hii miche halafu wanaenda kuanzisha bustani mara nyingi wanapandisha bei sasa inakuwa kama biashara hivi huko Kilimanjaro, Mheshimiwa Mramba anasema inafika shilingi 2500 na

nilishapata habari kwamba kule Mara kwa sababu ya matatizo ya ukosefu wa maji inafika mpaka shilingi 3500. Mimi ninapenda kusema kwamba jambo hili hatuwezi kulipatia majibu hapa leo lakini tumelipokea na tunaitisha wadau wengine wanaohusika na kazi hii wakiwemo *TACRI*, Bodi ya Kahawa na sisi Wizara tukae tuone ni kitu gani tunaweza tukafanya ili miche iongezwe lakini vile vile bei ishuke, ili wakulima wengi zaidi waweze kuipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema kilimo cha Kahawa tunakipa umuhimu mkubwa na vilevile bei hizi ambazo tunazisema hapa zinaweza zisiwe tatizo kubwa sana ikiwa wakulima wetu watazingatia kanuni na wakazalisha Kahawa ya daraja la juu sana. Kwa sababu hata bei ya Kahawa ilipoanguka mwaka jana ile Kahawa ya *high quality* haikuanguka na ilikuwa inapata bei nzuri sana. Ndugu zangu wa Kigoma, kule wanaelewa wao wanazingatia kanuni, wana *process* na wanauza katika masoko maalum na wanapata bei nzuri tu na ya kwao haikushuka na wako wakulima katika Mikoa kama Arusha, *specilized* ambao wanafanya kazi hii na wenyewe wanapata bei nzuri na bei haitikisiki sana ukilinganisha na bei ya Kahawa ya kawaida ambayo inazalishwa bila kuzingatia sana ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninachoweza kusema ni kwamba Azimio hili tunalolipitisha hapa pamoja na masuala mazima ya kusimamia programu za uzalishaji wa Kahawa, ni programu za uzalishaji kwa kuzingatia kanuni yote, kwa pamoja yatatuongezea ubora na wingi wa Kahawa na hiyo itakuwa ni shabaha nzuri. Lakini hoja hii ambayo inaridhiwa, itaridhiwa na Bunge lako Tukufu muda sio mrefu ujao, itatusaidia kwa sababu inapanua soko la Kahawa ambalo ni jambo muhimu sana katika suala zima la biashara ya Kahawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge vizuri na umetoa hoja na hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo naomba kutangaza rasmi kwamba Bunge hili limeridhia Azimio linalohusu Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 2007 (*The International Coffee Agreement Act 2007*). Tunawatakiya kila kheri Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, tukiamini kabisa kwamba Azimio hili litatusogeza mbele zaidi kuhakikisha kwamba kilimo chetu cha Kahawa, wakulima wetu na biashara nzima ya Kahawa katika nchi yetu na Kimataifa inatufaidia zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa, tunasema ahsante sana. (*Makofi*)

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka 2007*
(*International Coffee Agreement-Ica, 2007*) liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Sasa baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge mkiangalia *Order Paper* yetu ya leo kinachofuata ni Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC ya mwaka 2008, *SADC Protocol*

on Gender and Development. Moja kwa moja, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta atusomee Azimio lenyewe.

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya
ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) wa Mwaka 2008
(SADC Protocol on Gender and Development)**

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hoja ya Azimio la Tanzania Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu Jinsia na Maendeleo la Mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mwaka huu wa 2010, kabla sijawasilisha hoja yangu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha siku ya leo. Nawatakia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti, na Waheshimiwa Wabunge wote, kheri ya mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na Watanzania wote, kwa kuondokewa na kiongozi wetu aliyetoa mchango mkubwa katika Taifa letu, marehemu Mzee Rashid Mfaume Kawawa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amen. Pia nawapa pole Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na wazazi, ndugu na jamaa zao. Poleni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeweza kusimama kutoa hoja hii siku ya leo kutokana na maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuhusu itifaki hii na ufuatiliaji wa karibu wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii, kuwashukuru kipekee wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, kwa uchambuzi wa kina wa itifaki hii na hivyo kuniwezesha kuiwasilisha siku ya leo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwanasheria Mkuu na ofisi yake kwa kazi kubwa iliyowezesha kukamilika kwa itifaki hii. Namshukuru kipekee Mwandishi Mkuu wa Sheria (CPD), Bwana Casmir Kyuki, kwa juhudi zake za makusudi zilizowezesha kukamilika na kuwasilisha kwa itifaki hii. Asante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri wa Maendeleo Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Katibu Mkuu Bi. Mariam Mwafisi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa ushirikiano na msaada mkubwa walioutoa. (*Makofi*)

Baada ya utangulizi huo, naomba sasa kutoa muhtasari wa masuala yaliyomo katika itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *SADC* na imekuwa ikishiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu jumuiya hiyo. Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchini za Kusini mwa Afrika *SADC* ya mwaka 2008, inatokana na Azimio la Wakuu wa nchi au Serikali za *SADC* lililowekwa saina huko Blantyre nchini Malawi mwezi Desemba, 1997 pamoja na nyongeza yake ya uzuiaji na utokomezaji ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto iliyowekwa saina nchini Botswana na wakuu wa nchi mwaka 1998, Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya *SADC* iliyowekwa saina mjini Johannesburg, Afrika ya Kusini, tarehe 17 Agosti, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii inatekeleza makubaliano ya nchi wanachama wa *SADC* na wajibu wa nchi kuhusu utekelezaji wa mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa aina zote za Ubanguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Azimio na ulingo wa Beijing, Azimio la *SADC* la Jinsia la Maendeleo la mwaka 1997 na nyongeza ya mwaka 1998 kuhusu Kuzuia na Kuondoa Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto. Vilevile ni utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Mataifa, namba 1325 kuhusu wanawake, amani na usalama, Itifaki ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Wanawake ya mwaka 2003 na Azimio la Usawa wa Jinsia la mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Itifaki hii ni kuwepo kwa makubaliano ya kisheria na kuziba upungufu wa kijinsia, kwa kuweka malengo yenye vipimo katika shughuli zote za maendeleo ambayo awali hayakuhusishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya *SADC* imezingatia masuala muhimu katika kuleta usawa wa jinsia na yamegawanyika katika Ibara 36 kama ifuatavyo:-

Ibara ya 1 - 3 ya Itifaki hii inahusu tafsiri ya maneno yaliyotumika. Vilevile inaeleza kanuni za msingi na madhumuni ya Itifaki hii, ambayo pamoja na mambo mengine ni kuweka ahadi ya Nchi Wanachama, kukubali kutekeleza wajibu wao kuhusu kuleta na kuweka usawa wa kijinsia katika nchi zao, kuainisha muda mahususi wa utekelezaji, kuweka namna bora ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na kubadilishana uzoefu wa mifano bora baina ya Nchi Wanachama ikiwemo kuboresha uhusiano wa kikanda.

Ibara ya 4 - 11 inahusu Katiba na Sheria. Ibara hii inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba, Katiba zao zinazingatia usawa wa jinsia na kuhakikisha kwamba, Katiba inaheshimiwa na hakuna sheria za kimila zinazopingana na Katiba. Vilevile inaelekeza kufutwa au kurekebisha kwa sheria zote zinazombagua mwanamke na kuhakikisha kwamba, mipango, sera na sheria, zinatoa fursa sawa katika kupata haki za msingi pamoja na haki za kifamilia kwa watoto, wanawake na wasiojiweza.

Ibara ya 12 - 13 inahusu uwiano katika nafasi za Uongozi, Ibara hii inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha uwakilishi wa wanawake katika ngazi za maamuzi unazingatiwa katika

Taasisi za Umma na Binafsi. Inasisitiza Nchi Wanachama kutumia mabadiliko ya Kikatiba na Kisheria, pamoja na Utashi (*Affirmative Action*). Inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kuwa zinakuwa na sera, mikakati na programu za kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika hatua zote na ngazi zote za uchaguzi kwa kuwajengea uwezo na kuwapa msaada unaostahili ili kufikia lengo hilo.

Ibara ya 14 inahusu elimu na mafunzo. Ibara hii inasisitiza fursa sawa ya kupata elimu kwa wanawake na wanaume kuhakikisha kwamba, wanawake wanawezeshwa kuendelea na kuhitimu masomo yao. Vilevile inaelekeza umuhimu wa kushughulikia utokomezaji wa mawazo mgando (*stereotypes*), kwenye taasisi za elimu na kuondoa aina zote za ukatili wa kijinsia.

Ibara ya 15 - 19 inahusu uzalishaji, ajira na uwezeshwaji wa kiuchumi. Ibara hii inazungumzia umuhimu wa kuwashirikisha wanawake katika utungaji na uandaaji wa sera za kiuchumi, pamoja na utekelezaji wake. Ibara hii ina vipengele vinavyozitaka Nchi Wanachama kuwawezesha wajasiriamali kupata mikopo, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wajasiriamali wadogo wanawake kuweza kuomba na kushindania *tender* mbalimbali za manunuzi Serikalini na katika Taasisi zake, ikiwemo nafasi sawa katika kupata na kumiliki rasilimali pamoja na ajira.

Ibara ya 20 - 25 inahusu ukatili wa kijinsia. Ibara hii ina vipengele vinavyozitaka Nchi Wanachama kutekeleza mikakati mbalimbali, ikiwa ni pamoja na utungaji wa sheria na urekebishaji wa sheria zilizopo ili ziweze kukidhi vigezo na viwango vya usawa wa jinsia na kufuta sheria zote zinazoendeleza ubaguzi kwa misingi ya jinsia, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa sheria zilizopitishwa au kurekebishwa ili kuondoa aina zote za ukatili wa kijinsia, pamoja na biashara ya binadamu (*trafficking*). Vilevile Itifaki hii inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba, sheria zinazohusu ukatili wa kijinsia zinatoa wajibu kwa wahusika ili kuendesha usimamizi na tathmini ya utekelezaji utakaohakikisha utokomezaji wa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Ibara hii pia inaelekeza Nchi Wanachama ziruhusu kuwepo na sheria ya kuruhusu kutoa mimba. Kwa upande wa nchi yetu, Sheria ya Jinai (Sura Na. 16), inazuia utoaji wa mimba isipokuwa kwa sababu maalum tu za usalama na uhai wa mtoto na mama.

Ibara ya 20(2)(a) ya Itifaki hii, inatoa haki ya kutoa mimba kinyume cha Sheria za Nchi yetu, Kifungu cha 219 cha Kanuni ya Adhabu (*The Penal Code, Cap. 16 R.E. 2002*). Kufuatana na hali hii, Mkataba wa Vienna wa Mwaka 1980 unaelekeza ni kwa namna ipi Nchi Wanachama wanavyoweza kutekeleza au kutotekeleza masharti ya Mikataba ya Kimataifa. Kwa mujibu wa Mkataba huo wa Vienna, pamoja na Kanuni za Sheria za Kimataifa, nchi inaporidhia Mkataba huo bado hailazimiki kutekeleza kila jambo lililomo ndani ya Mkataba. Ni rai ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuwa, Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki ya *SADC* kuhusu Jinsia na Maendeleo ya Mwaka 2008, lakini isitekeleze masharti yaliyomo kwenye Ibara ya 20(2)(a), kwa kuwa yanaenda kinyume na imani, mila, utamaduni na Sheria za Nchi yetu. Masharti yanakinzana na maadili yetu, yanayoitaka kila Nchi Mwanachama kuhakikisha kwamba, ifikapo mwaka 2015 ziweke utaratibu wa kisheria utakaoruhusu au kuwezesha wahanga au waathirika wa vitendo vya ubakaji waruhusiwe kutoa mimba.

Ibara ya 26 inahusu Afya. Ibara hii inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba, zinaandaa na kutekeleza Sera na Programu za Afya, kwa kuzingatia hali zote za kimaumbile, kiakili na kijamii kwa wanawake ili kuhakikisha zinaboreshwa na kupatikana kwa uhakika katika sehemu zote ili kupunguza vifo vya akinamama na watoto.

Ibara ya 27 inahusu VVU na UKIMWI. Ibara hii inahusu masuala ya kinga, tiba na matunzo kuhusu VVU na UKIMWI. Vilevile inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha upatikanaji wa kinga, tiba na matunzo kwa waathirika unaozingatia usawa wa jinsia, kwa kujumuisha wanawake, wanaume vijana na wasichana bila ubaguzi.

Ibara ya 28 inahusu ushirikishwaji wa wanawake wakati wa mazungumzo ya kutafuta amani. Ibara hii inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba, zinaweka utaratibu unaowezesha usawa wa uwakilishi wa wanawake na wanaume wakati wa mazungumzo ya utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa Azimio Namba 1325 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Ibara ya 29 - 31 inahusu Vyombo vya Habari, Taarifa na Mawasiliano. Ibara hii inazitaka Nchi Wanachama kuzingatia usawa wa jinsia katika upatikanaji wa taarifa na mawasiliano. Katika Sera na Sheria ya Habari, Itifaki inazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba, kuna uwakilishi sawa wa wanawake na wanaume katika maeneo yote na ngazi zote katika vyombo vya habari. Aidha, wanawake na wanaume wapewe fursa sawa katika vyombo vya habari. Itifaki inazitaka Nchi Wanachama kuongeza vipindi vya uelimishaji kuhusu haki za wanawake na usawa wa jinsia, kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mawazo mgando na athari zake kwa maendeleo ya wanawake na jamii katika vyombo vya habari.

Ibara za 32 – 36 hii zina vipengele vinavyozitaka Nchi Wanachama kuandaa bajeti zenye kuzingatia usawa wa kijinsia, pamoja na kutenga rasilimali za kutosha, kuandaa mpango mkakati wa nchi wa utekelezaji wa Itifaki hii na ukusanyaji wa takwimu. Itifaki pia inazitaka Nchi Wanachama kuwasilisha ripoti ya kina kwa sekretarieti ya SADC kila baada ya miaka miwili ikionyesha hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa Itifaki na maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii kabla ya kuwasilishwa hapa Bungeni, Wadau mbalimbali wameshirikishwa katika kuipitia, hususan wakati wa maandalizi na kabla ya kuweka saina. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imehusishwa kikamilifu katika kupitia na kuandaa taratibu ili iweze kuridhiwa kwa mujibu wa Sheria na taratibu za Nchi.

Kuridhiwa kwa Itifaki kutawezesha kuandaliwa kwa mkakati wa utekelezaji wake. Mkakati huo utaelekeza sekta na wadau mbalimbali, namna ya kuziba mapengo ya kijinsia katika shughuli za kisekta na hivyo kuwezesha sekta kuwa na nguvu za kisheria katika kuboresha mifumo ya huduma, kutunga sheria mpya, kurekebisha au kufuta sheria kandamizi kijinsia, kuandaa au kudurusu sera, mikakati na mipango mbalimbali ya kisekta. Aidha, itatoa fursa sawa ya ushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo bila ubaguzi wa kijinsia na uonevu. Itifaki hii itawezesha pia wananchi wote kulinda utu, heshima, uhuru na usalama bila woga.

Pamoja na kuwekwa sahihi kwa Itifaki hii na kabla ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu, Tanzania imekuwa ikitekeleza mambo mengi yaliyo katika Itifaki ikiwemo kuongeza nafasi za wanawake katika nafasi za uongozi, kutunga sheria au kufanya mabadiliko ili kuzingatia usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizotia sahihi Itifaki hii ni kumi na tatu kati ya kumi na tano ambazo ni Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Lesotho, Madagascar, Mozambique, Malawi, Namibia, Afrika ya Kusini, Swaziland, Tanzania, Zambia, Zimbabwe na Seychelles. Nchi ambazo zimesharidhia ni Namibia na Zimbabwe. Botswana na Mauritius hazikuweka sahihi.

Aidha, nchi nyingine kwa mujibu wa sheria za nchi zao, zikishasaini moja kwa moja zinakuwa zimeridhia; kwa mfano Botswana. Kwa mujibu wa Ibara ya 41 ya Itifaki hii, Itifaki itanza kuwa na nguvu ya kisheria siku thelathini baada ya theluthi mbili ya Nchi Wanachama kuwasilisha Hati za Kuridhia kwa Katibu Mtendaji wa SADC. Nchi ambazo ziko kwenye mchakato wa kuridhia ni Namibia, Afrika ya Kusini, Swaziland na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hii kutawezesha kuandaliwa kwa mkakati wa utekelezaji wake; na kwa kuwa Mkakati huo utatatekelezwa na wadau mbalimbali; ni dhahiri kwamba, Itifaki hii itakapoanza kutekelezwa, kutakuwepo na gharama za utekelezaji. Kwa msingi huo, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa wito kwa kila sekta, kuingiza gharama za utekelezaji wa Itifaki hii kwenye bajeti ya shughuli zao kwa ajili ya utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, lipitie, lijadili na liriidhie Itifaki hii kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani SADC la Mwaka 2008.

KWA KUWA Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama wa SADC zimeziridhika kuwa usawa wa jinsia ni mojawapo ya nguzo muhimu za haki za binadamu;

NA KWA KUWA Tanzania imedhamiria kuondoa aina zote za unyanyasaji na kuwa na haki sawa kijinsia katika mipango na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa mujibu wa Sheria, Sera, Mipango na Miradi;

NA KWA KUWA masuala ya jinsia yameingizwa katika program na mipango ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, nchi wanachama hazina budi kuendeleza masuala ya jinsia katika programu na mipango ya kimaendeleo katika nchi zao;

NA KWA KUWA masuala yanayohusiana na utoaji mimba yamehusishwa katika Itifaki hii katika Ibara ya 20(ii)(a) kwa namna ambayo inapingana na utamaduni na imani, mila na sheria za nchi yetu;

NA KWA KUWA Sheria ya Jinai, Sura ya 16 inazuia utoaji wa mimba isipokuwa kwa sababu maalum tu za usalama na uhai wa mtoto na mama;

NA KWA KUWA Ibara ya 20(ii)(a) ya Itifaki hii inatoa haki ya kutoa mimba kinyume cha sheria za nchi, kifungu 219 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 na marekebisho yake ya mwaka 2002;

NA KWA KUWA nchi wanachama wa *SADC* wanalo jukumu la kutekeleza Maazimio, Mikataba na Itifaki za Kimataifa na Kikanda zinazohusu jinsia na maendeleo inawapasa kuwa na mikakati ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia pamoja na masuala mtambuka kama janga la UKIMWI, usafirishaji haramu wa watu hasa wanawake na watoto na kupiga vita umaskini;

NA KWA KUWA nchi wanachama wa *SADC* zilikubali kuingia na kutia sainsi Itifaki ya Jinsia na Maendeleo yaani *SADC Protocol on Gender and Development* tarehe 17 mwezi Agosti, 2008 mjini Johannesburg, Afrika ya Kusini;

NA KWA KUWA hatua ya Tanzania kuridhia Itifaki hii ikiwa ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika itawezesha Watanzania kupata faida katika kuleta na kuimarisha usawa na maendeleo ya kijinsia katika nyanja zote za maisha.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia mkataba wa Kimataifa unaohusu mikataba na Itifaki za Kimataifa yaani *The Viena Convention on the Law of Treaties* ya mwaka 1980 na kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya kuridhia Itifaki ya *SADC* kuhusu Jinsia na Maendeleo kwa Taifa letu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Sura ya 2. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kumi na Nane, sasa inaazimia Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Jinsia na Maendeleo ya mwaka 2008 isipokuwa Tanzania isitekeleze masharti yaliyomo kwenye Ibara ya 20(ii)(a) yaani *SADC Protocol on Gender and Development* ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunakushukuru sana kwa kutusomea Azimio na kutoa hoja na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Msemaji wa

Kamati, ambaye ni Mwenyekiti Mwenyewe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ya Mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, naomba sasa kwa heshima yote niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ya Mwaka 2008 (*The SADC Protocol on Gender and Development*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bunge hili linakutana sasa kipindi ambacho muda mfupi tu uliopita tumempoteza Kiongozi Mashahuri, aliyekuwa mwadilifu sana na zaidi ameitumikia nchi yetu katika nyadhifa mbalimbali ikiwemo kuongoza shughuli za Serikali Bungeni, Hayati Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa; kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kutoa pole nyingi kwa familia ya marehemu na Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amen*.

Vile vile kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua nafasi hii kuwapa pole waathirika wote wa majanga mbalimbali katika nchi yetu, ambayo yametukumba toka tulipomaliza Mkutano uliopita mpaka kipindi cha Mkutano huu. Mwenyezi Mungu, atawapa faraja na basi yote yatakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilikutana na kuanza kupitia Azimio la Kuridhia Itifaki hii ya Jinsia tarehe 13 na tarehe 19 Januari, 2010, ambalo liliwasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margret Sitta, Mbunge, ili kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mwanachama katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, yaani *SADC*; na kwa kuwa Nchi Wanachama wa *SADC* zimeridhika kuwa sasa usawa wa jinsia ni mojawapo ya nguzo muhimu ya haki za binadamu; na kwa kuwa Tanzania ipo tayari kukomesha unyanyasaji na kuwa na haki sawa ya kijinsia katika mipango na utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo kwa mujibu wa Sheria, Sera, Mipango na Miradi; na vile vile kuhakikisha masuala ya jinsia yameingizwa katika Programu na Mipango ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Nchi Wanachama; ni budi masuala hayo yapewe kipaumbele katika maendeleo katika nchi yetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano ya kina na Wajumbe kuridhishwa na maelezo ya utangulizi ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kamati

inaliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuridhia pendekezo la Serikali kuhusu Itifaki ya Jinsia ya Maendeleo ya Nchi za SADC, isipokuwa Ibara ya 20(2)(a), ambayo nitaelezea hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe maoni na mapendekezo ya Kamati yangu. Ukiangalia kwa ujumla pamoja na Azimio hili kujikita katika suala zima la jinsia na maendeleo, kwa kweli sehemu ya pili ya Itifaki imesisitiza sana Nchi Wanachama kushirikiana kwa pamoja katika kukusanya rasilimali ili kufanikisha utekelezaji wa Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, Kamati imegundua nchi yetu pia katika kuridhia Itifaki hii, itajiweka katika nafasi nzuri sana ya kushiriki katika kujipatia ama kutumiwa na wananchi wake kushiriki kufaidi huduma za kiufundi, kifedha na rasilimali watu katika utekelezaji wa Itifaki yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5 ya Itifaki hii inazungumzia juhudi za makusudi (*Afemative Action*). Nchi Wanachama zinatakiwa kuchukua hatua za makusudi ili kusaidia kumjengea mwanamke mazingira bora ya kushiriki katika mambo yote yawe ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ni ya uzito wa namna ya pekee, hasa ukizingatia kuwa inamtaja mwanamke kwa jinsi yake na kusisitiza apewe mazingira ya kumwezesha kushiriki katika mambo mbalimbali. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne katika nchi yetu ya Tanzania, kwa kutambua mchango wa wanawake katika nyanja zote zikiwemo kilimo, siasa, uchumi na hata uongozi. Kamati yangu inatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofi*)

Ibara ya 6 ya Itifaki inazungumzia kwamba, ifikapo mwaka 2015, Nchi Wanachama zihakikishe zinaondoa dhana ya kumkandamiza mwanamke, lakini zinatambua usawa wa jinsia katika kupata haki sawa mbele ya Sheria. Kamati inakubaliana na Azimio hili, kwani ukweli ni kuwa, mahusiano bora katika ya mwanamke na mwanamume ndiyo msingi mkubwa kabisa wa kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7 ya Itifaki inazungumzia Nchi Wanachama kutunga sheria na taratibu zitakazohakikisha usawa kwa wanawake unaonekana na kupatikana katika mienendo ya kesi kwa kufuata sheria zote nchini; ziwe za kimila, ziwe za jadi na nyingine zote, hasa katika umilikaji mali, mirathi na mikopo na kutengeneza huduma za kufikika za kisheria. Sehemu hii pia inaitaka jamii kuwawezesha wanawake katika kupigania haki zao kisheria. Wanawake wawezeshwe kushiriki au kuwakilishwa kikamilifu katika vyombo vya sheria vya kimila vya kiserikali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Kamati yangu inaipongeza Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama vile NOLA, WILAC, TAMWA, TGNP na mengine mengi tu, kwa kuanza kutekeleza sehemu hii ya Azimio, kwani wanawake wengi wamekuwa wakipoteza haki zao za kimsingi katika vyombo vya maamuzi ya kisheria ama tu kwa kushindwa kujieleza au kwa kukosa elimu ya kutosha.

Kamati inashauri kuwa, pamoja na kuwepo kwa mazingira na baadhi ya sheria zinazoweza kumsaidia mwanamke katika eneo hili, bado upo umuhimu wa kuziangalia sheria zetu katika mazingira ya uendeshaji wa mashtaka na hasa kama mdai ni mwanamke na namna bora ya kutekeleza eneo hili la Azimio kama ilivyoelekezwa katika Itifaki yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi na hasa waishio vijijini, hawajui haki zao. Huu ni ukweli usiopingika, kwa kuwa eneo hili linahusu pia kutoa elimu. Tunashauri sana kupitia Kamati yangu, vyombo vya habari vijikite katika kuwaelimisha wanawake na hasa wanawake waishio vijijini kuhusu Azimio hili na hasa Sheria na haki zao za kimsingi. Kamati inaendelea kuyaomba Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Serikali na hata Sekta Binafsi, kuendelea kuongeza nguvu katika eneo hili la kuwasaidia wanawake kwenye nyanja ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8 ya Itifaki inazungumzia haki sawa kwa mwanamume na mwanamke hasa katika kuweka sheria zitakazowafanya wote wafurahie na wawe washiriki sawa katika ndoa. Sehemu hii inasisitiza kutoruhusu kuolewa kwa mtoto wa kike chini ya miaka 18, isipokuwa kwa kibali maalum na iwe pia masuala ya ndoa ni maridhiriano huru ya mwanamume na mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Itifaki inasisitiza na kushauri ndoa zote iwe za kimila, iwe za kidini, iwe za kiserikali, zifanyiwe usajili kulingana na sheria za nchi. Kamati inakubaliana na kifungu hiki na kuisisitiza, suala la tabia isiyo njema ya kimaadili ya akina baba wengi wenye mazoea ya kuwaharibu watoto wadogo chini ya miaka 18 kwa kisingizio cha kutaka kuwaoa ikomeshwe mara moja. *(Makofi)*

Kamati pia inawakemea sana akina mama wenye tabia ya kuwarubuni watoto wadogo wa kiume wa chini ya miaka 18 kimapenzi, kwani nchi yetu sasa imeshatekeleza sehemu ya Itifaki hii kwa kutunga Sheria ya Mtoto na Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana. Kamati inaishauri Serikali iamue kufanya elimu ya sekondari kuwa elimu ya lazima kama ilivyo elimu ya msingi ili watoto wote waendeleo na masomo katika umri chini ya miaka 18. Serikali ipitie sheria zake na kuhakikisha kuwa, inawalinda wanandoa katika maamuzi yao ya ndoa na kuwaruhusu kuchukua uraia wa mwenzi wake kama ndoa hiyo siyo jozi ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9 inahimiza kuwepo kwa sheria zitakazowalinda walemavu na kuwasaidia kupata haki zao shirikishi. Kamati inaunga mkono eneo hilo na kwamba, Serikali ihakikishe kila sheria itakayotungwa yenye kuhusiana na suala la ulemavu, basi pawepo kipengele cha kuzingatia kuwalinda walemavu katika maeneo yote muhimu yahusyo walemavu kama Itifaki inavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 10 inahusu haki za wajane na wagane. Nchi Wanachama zinatakiwa kuhakikisha kuwa, wajane na wagane hawanyanyasiki katika suala lolote. Wajane na wagane waendeleo kupata haki zao katika kila jambo; mfano mirathi, kazi, ajira na kadhalika. Kamati inakubaliana na sehemu hii na inaendelea kuishauri Wizara na Serikali ikiwezekana kuingiza madawati ya jinsia katika maeneo yote ya kazi, kufuatilia suala zima la kuwasimamia wajane na wagane ili kuhakikisha wanaendeleo kupata haki zao. Suala la haki za wajane na wagane linaonekana kukosa usimamizi wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 inazungumzia ulinzi na usalama wa watoto wote wa kike na wa kiume. Eneo hili linataka Nchi Wanachama kuwa na sheria zitakazowalinda watoto kutokana na aina zote za unyanyasaji na hasa watoto wa kike; kumlinda mtoto wa kike kutokana na mazingira hatarishi ya mila na desturi, kumtumikisha, kumfanyisha mtoto kazi za kiuchumi, biashara na ukatili mwingine wa kijinsia, yaani *economic exploitation and trafficking and sexual abuse*.

Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa watoto wetu wa jinsi zote wapo katika mazingira hatarishi, mfano; madawa ya kulevya, utumikishwaji, ajira ngumu, unyanyasaji na kadhalika; watoto wa kike hutumika katika madanguro, huchukuliwa na kupewa ajira za unyanyasaji; na kwa kuwa tayari Bunge limepitisha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu (*Anti Trafficking in Persons Act No. 6 of 2008*) na Sheria ya Mtoto; tunaona angalau Serikali yetu ilishaanza kutekeleza ajenda hii. Sasa ni wakati muafaka Sheria hizi zifanyiwe tafsiri ili watoto na jamii yote ya Tanzania wapate nafasi ya kuzitambua na hivyo utekelezaji wake uonekane hadharani. Kamati inakemea sana vitendo hivyo vinavyokiuka maadili ya nchi yetu kwa kunyanyasa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara za 12 na 13, zinazungumzia Uwakilishi na Ushiriki wa Wanawake katika vyombo vya maamuzi. Azimio linataka Nchi Wanachama kuhakikisha ifikapo mwaka 2015, angalau nchi hizo ziwe zimefikia asilimia 50 ya Uwakilishi katika vyombo vya maamuzi, bila kusahau kutumika kwa *affirmative action* kama njia ya kufikia hapo. Katika Ibara ya 13, Azimio linaisisitiza nchi hizo wanachama ziwe na Sheria Maalumu na Mipango ya kuleta ushiriki sawa kati ya wanaume na wanawake katika mwenendo wa uchaguzi, kwa kuwajengea uwezo wanawake katika kushiriki shughuli zote za uwakilishi katika vyombo vya maamuzi, kutengeneza mpango maalumu wa kuwawezesha kufikia hapo na kuangalia upya mila na desturi zinazozuia kufikia uwakilishi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuongeza wanawake katika vyombo vya maamuzi ni jambo jema tena lenye umuhimu. Katika uchaguzi wa mwaka 2005, ulifanyika wakati Viongozi wa Nchi za SADC waliazimia kuwa ifikapo mwaka 2005, kila nchi iwe imefikia angalau asilimia 30 ya Wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi hasa Ubunge. Katiba yetu kabla ya mabadiliko ya mwaka 2005, ilikuwa na kipengele kifuatacho; ninanukuu: “Wabunge Wanawake idadi inayoongezeka kuanzia asilimia 20 ya Wabunge walitajwa katika aya ya (a), (c), (d); (kuchanguliwa Spika, kama siyo Mbunge, wawakilishi watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Wateuliwa na Rais kumi na Mwanasheria Mkuu). Idadi itakayotajwa mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi kwa taarifa iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali baada ya kupata kibali cha Rais.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za kushughulikia suala hilo, mwaka 2005 mabadiliko ya Kikatiba yaliyoletwa yakiwa tayari yamewekwa sahihi yalionesha kukosekana kwa maneno yafuatayo; nanukuu: “Itakayotajwa mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi kwa taarifa iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali baada ya kupata kibali cha Rais” yakawa hayapo. Hivyo, ikaonesha kuwa idadi ya wanawake ingekuwa chini ya asilimia 30 na hivyo Tanzania ambayo ilikuwa inasifika kwa mtazamo wake juu ya ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za maamuzi ingekuwa chini sana. Azimio hili linawataka Nchi Wanachama,

ziwashirikishe wanaume kwa kuwapatia elimu kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali na hasa Mheshimiwa Rais, kwa kuanza kuteua wanawake katika vyombo vya maamuzi kabla hata ya Bunge kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 – 2010, kifungu cha 120 (a) kinazungumzia ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi, nanukuu: *“(a) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi, kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kama ilivyokwisha azimiwa na Umoja wa Afrika.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa, ili kukamilisha adhima hii, Kamati inapendekeza Uchaguzi wa 2010, uwiano wa wanawake katika siasa uanze kwa kuchukua 40% ya Wabunge wote wa Majimbo na wale wa Kundi Maalumu ambao watatupelekea kuwa na asilimia 30.5 ya Viti Maalumu; hivyo ili kufikia asilimia 50, wanawake wengi wanatakiwa wasimame katika Majimbo kutafuta asilimia 20 iliyobaki. Hii inawezekana tu endapo mambo yafuatayo yatafanyika:-

Kwanza, kuwepo na utashi wa makusudi wa kisiasa katika vyama vya siasa kuteuwa wanawake kugombea katika Majimbo ya Uchaguzi na kuwasimamia washinde.

Pili, Serikali kupitia vyombo vyake na pia sekta binafsi, itoe elimu kwa umma kuhusu kusudio jema la kushirikisha wanawake ili kuchaguliwa katika vyombo vya maamuzi.

Tatu, Serikali na sekta binafsi ielimishe jamii kuachana na mila potovu zinazomfanya mwanamke ashiriki kuchaguliwa katika uchaguzi.

Nne, wanaume kwa wanawake wapeane ushirikiano ili dhamira hii itekelezeke. “Wanawake wasiogope, wanaume wasihofu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 inaozungumzia usawa wa kijinsia katika elimu na kwa kuwa hatuna Sheria inayomlinda mtoto anayepata ujauzito awapo shuleni; Kamati inashauri:-

Kwanza, Serikali itoe tamko rasmi la kumrudisha shuleni mwanafunzi aliyepata ujauzito mara baada ya kujifungua, wakati sheria ya kumrudisha mwanafunzi aliyepata ujauzito shuleni ikisubiriwa.

Pili, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza na kutenga magari maalum kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa kike na wa kiume wanaosoma shule za kutwa hasa za mijini, ili kuepukana na unyanyasaji kwenye daladala na kuepukana na watu wazima (mafataki), wanaowarubuni watoto hao kwa lifti na kuwatia mimba za utotoni na kuharibu maadili ya watoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16 inahusu suala zima la kutambua majukumu mazito ya kazi za mwanamke. Nchi Wanachama zinatakiwa mpaka kufikia 2015, ziwe zimefanya utafiti wa kutambua kazi za wanawake na mchango wao katika maendeleo ya jamii pia kurahisisha utendaji wao wa kazi.

Kamati inashauri Serikali sasa iangalie uwezekano wa kutunga sera itakayoruhusu uchambuzi wa mchango wa kazi zinazofanywa na mwanamke katika Pato la Taifa. Vile vile kwa kuwa mwanamke ndiyo mwenye majukumu mazito katika jamii ya sasa ya Mtanzania:-

(a) Serikali iweke Sera na Kanuni mahususi zitakazompunguzia mwanamke mzigo alionao katika jamii. Kwa mfano, kumfundisha teknolojia rahisi kama *Power tiller* na pembejeo za kilimo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vocha.

(b) Serikali itenge mikopo ya makusudi ya riba nafuu kwa nia ya kumwinua mwanamke kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ibara ya 18 ya Itifaki inamruhusu Mwanamke kumiliki mali, ikiwa ni pamoja na ardhi; Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Kuwepo na kipaumbele kwa wanawake katika mambo yote yanayohusu umilikaji na upatikanaji wa rasilimali.

(b) Wizara ya Kazi, Ajira na Mendeleo ya Vijana ifanye utafiti kujua Fedha za J. K. ni kwa kiasi gani zimewafikia wanawake kwa kulinganisha na wanaume.

(c) Serikali iweke utaratibu utakaomsaidia mwanamke anayetaka kutumia ardhi kama dhamana ya mkopo aweze kufanya hivyo bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ibara ya 19 ya Itifaki hii inampa mwanamke fursa sawa na wanaume katika kufanya kazi. Kamati inawataka waajiri wote kuwapatia wanaume na wanawake haki sawa katika kupata ajira. Vile vile Itifaki inawakumbusha wanaume na wanawake kukumbuka kuchukua likizo ya uzazi pale inapotokea kwani ni haki ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20(2)(a) ya Itifaki hii, pamoja na mambo mengine ya kimsingi, inazungumzia suala nyeti la utoaji mimba kwa dharura, kwa namna ambayo inapingana na utamaduni, imani, mila na Sheria za Nchi yetu. Sheria ya Jinai (Sura ya 16), inazuia utoaji wa mimba isipokuwa kwa sababu maalum tu za usalama na uhai wa mtoto na mama. Ibara hiyo ya 20(2)(a) ya Itifaki hii inatoa haki ya kutoa mimba kinyume na Sheria za Nchi, kifungu cha 219 cha Kanuni ya Adhabu (*The Penal Code, Cap. 16R E. 2002*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa SADC, wanalo jukumu la kutekeleza Maazimio, Mikataba na Itifaki za Kimataifa na za Kikanda, zinazohusu jinsia na maendeleo na hivyo nchi zinapaswa kuwa na mikakati ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia pamoja na masuala mtambuka kama janga la UKIMWI, usafirishaji haramu wa watu hasa wanawake na watoto na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hatua ya Tanzania kuridhia Itifaki hii, kunapelekea Watanzania kupata faida katika kuleta na kuimarisha usawa wa maendeleo ya jinsia katika nchi yetu. Pamoja na hayo, Kamati baada ya kuona tatizo la Ibara ya 20(2)(a) na kwa kuzingatia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Mikataba na Itifaki za Kimataifa (*Vienna Convention on the Law of Treaties 1980*), pamoja na kuzingatia wajibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa na wajibu wa Kikatiba wa Kuridhia Itifaki (Ibara 63(3)(e) ya Katiba yetu); Kamati inaiomba Serikali isitekeleze masharti yaliyomo kwenye Ibara ya 20(2)(a) yahasuyo utoaji mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 22 inatoa ufumbuzi wa matibabu kwa mtu aliyebakwa. Kwa kuwa kuna dawa anazopewa mtu aliyebakwa kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI, Kamati inaishauri Serikali kutoa dawa hizo kwa watu wote watakaogundulika wana maambukizi katika hatua za mwanzo, badala ya dawa hizo kupewa wale waliobakwa peke yao ili kupunguza maambukizi ya UKIMWI yanayozidi siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ibara ya 29 ya Itifaki inafafanua namna ya kuondokana na udhalilishaji kwa wanawake na watoto, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa kufungia vyombo (Magazeti), yanayotoa picha na habari za kudhalilisha wanawake katika jamii. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa, vyombo vya habari haviitumii taaluma yake kuchafua na kudhalilisha makundi fulani katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, pamoja na Wataalam wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mariam Mwaffisi, kwa ushirikiano wao waliutoa kwa Kamati. Vile vile kwa namna ya pekee, Kamati inapenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Wasaidizi wake, kwa ushirikiano waliotoa kwenye Kamati yangu na hatimaye Kamati kukubali pendekezo hili la Serikali la Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo, isipokuwa Ibara ya 20(2)(a). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, napenda sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili la Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub S. Masoud - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Dora Herial Mushi, Mheshimiwa Dkt. Gertrude P. Rwakatara, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena kwa nafasi hii uliyonipa ili nitoe maoni na ushauri wa Kamati kuhusu pendekezo la Azimio hili. Napenda kumshukuru Katibu wa

Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Makatibu wa Kamati; Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rachel Nyega, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja, lakini ninaendelea kuisisitiza kwamba, Kamati imetoa tahadhari katika kifungu cha 20(2)(a), kinachohusu suala la utoaji wa mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kujitambulisha, ninaitwa Maulidah Anna Komu, halafu naendelea na mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Maoni na ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) wa Mwaka 2008 (*SADC Protocol on Gender and Development*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa ujasiri waliouonesha kwa kuleta Azimio hili ili Bunge lako liweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile malengo ya Azimio ya kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya *SADC* ni kwamba, Nchi za Kusini mwa Afrika, zinawawezesha wanawake na kuwaondolea kero mbalimbali za kuwabagua na kuwadhalilisha kijinsia na kutekeleza sheria, sera na masuala yote yanayoangalia usawa na jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Azimio hili kwa kina na taarifa ya maelezo yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kambi ya Upinzani haina pingamizi lolote la kuridhia Azimio hili; cha kuzingatia ni utaratibu mzima utakaotumika kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, ni vema Nchi Wanachama wa *SADC* zikaingiza vifungu katika Katiba za nchi zao, ili kuelezea kuondoa kero za ubaguzi wa kijinsia katika Sekta mbalimbali za Maendeleo na kutunga sheria za kutoa adhabu kwa yeyote atakayefanya ubaguzi na kutotekelezwa kwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ulemavu unaweza kumpata mtu yeyote aidha akiwa mtoto, mkubwa au kuzaliwa nao, Kambi ya Upinzani inashauri Azimio hili lizingatie jamii hii na kuwawekea sheria na sera za kuwalinda katika sehemu zao za kazi na mahali wanapoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya kumi inayozungumzia haki za wajane na wagane ni ya umuhimu mkubwa sana katika jamii yetu ya Watanzania, hivyo kuna umuhimu wa kuiangalia kwa umakini, kwani inagusa mila, desturi na hasa dini za jamii mbalimbali. Mirathi inachukua

haki za wajane, wagane na hususan watoto wanaoachwa na marehemu. Hii ina pande mbili muhimu:-

(a) Mjane anapoachwa na mali ambayo ingetosha sana kuwalea wototo, lakini hapo hapo hutokea ndugu wa marehemu na kumnyang'anya na kuanza kuweka taratibu za ukoo husika na kusema mtu mwingine nje ya mjane asimamie mali hiyo (msimamizi wa mirathi). Kwa njia hii, dhuluma hutokea na mwisho mjane hunyang'anywa kila kitu kwa udanyanyifu huu.

(b) Pale mjane anapoamua kuolewa, kwani hawezi kuendelea kubaki mpweke kama umri wake bado mdogo, mwanaume anayemuoa huhamia pale akawa ndiye mkuu wa nyumba na anaweza kumuwekea yule mjane masharti ambayo yeye anaelewa malengo yake na mwisho huuza mali zote na watoto huachwa bila chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa angalizo hilo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali pale itakapoleta Muswada wa Sheria ya Ndoa, iweke kifungu ambacho kitaiweka mali iliyoachwa wakati watoto wakiwa wadogo chini ya usimamizi wa Serikali hadi watoto watakapofikia umri wa miaka 21, kwani tunaamini kwa umri huo wahusika watakuwa wana umri wa kuelewa nini wanaweza kufanya na mali za baba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 – 13 inahusu uwakilishi na ushiriki wa kijinsia, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali izingatie Itifaki hii ili kuwe na uwiano sawa katika nafasi mbalimbali ili kuepusha manung'uniko yasiyo ya lazima, ambayo yanaweza kusababisha ugumu wa utekelezaji wa Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ibara ya 14 inazungumzia usawa katika elimu kwamba, ifikapo mwaka 2015, Nchi Wanachama zinatakiwa kuhakikisha kuwa, elimu ya msingi na sekondari, pamoja na viwango mbalimbali vya elimu na mafunzo, zinatolewa kwa usawa. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iweke utaratibu wa kuwarudisha mashuleni wanafunzi wa kike mara baada ya kujifungua ili wasinyimwe haki yao ya msingi ya kielimu na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16 ya Itifaki inazungumzia kuwa, mwanamke ndiye mara zote mwenyekuwa na majukumu mazito ya kukaa na watoto na kuilea familia kimaadili ukilinganisha na mwanaume, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iweke mipango madhubuti ya kumuwezesha mwanamke kupata mikopo yenye masharti nafuu ambayo haina riba kubwa itakayomwezesha kuilea familia kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 27 inahusu VVU na UKIMWI; Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutumia ushawishi wake kwa Nchi za SADC kuhakikisha kuwa, wanaoeneza maambukizi ya Ukimwi kwa makusudi, hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao, hasa taswira inaonesha kuwa Nchi za SADC ndio zinazoongoza kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 30 inayohusu jinsi na vyombo vya habari (*Gender in Media Content*); mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu, kwa kiasi kikubwa,

umechangiwa na machapisho na filamu nyingi kama zinavyooneshwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, kuna tabia ambayo imejitokeza kuwa jinsia ya kike ndiyo inayoweza ku-*promote* mauzo ya bidhaa mbalimbali kama vile mauzo ya kanda za miziki ya dance, wachezaji/wanenguaji wa kike wanavyokuwa wamevaa. Huu ni ukweli kwa kuangalia matangazo kadhaa ambayo yanatolewa katika runinga na baadhi ya magazeti ya udaku yanayotolewa mara kwa mara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaungana moja kwa moja na kifungu cha tatu cha Ibara hii, kwani Serikali kuchelewa kuchukua hatua zinazostahili inaweza kuzilazimu asasi zinazojihusisha na maadili, kujichukulia hatua kwa wahusika wakuu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaomba ipate ufafanuzi; ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Nchi za Jamhuri ya Malawi, Madagasca, Botswana na, Mauritius kuchelewa kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC Protocol on Gender and Development*)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, kwa kusoma maoni ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika uchangiaji, ambapo kwenye orodha yangu hapa nina wachangiaji 14. Kati ya wachangiaji 14, 12 ni akinamama na wawili ni akina baba. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Bujiku Sakila, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Mheshimiwa Bujiku Sakila. (*Makofi*)

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kwa sababu mimi ndio naanza kuchangia kwa mara ya kwanza kwa mwaka huu; natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Kawawa, kwa msiba mkubwa uliowapata wa kupotelewa na mzee wao na kwa Taifa kwa ujumla. Mzee huyo tulimpenda, alikuwa mfano mzuri kwa wananchi wetu, lakini bahati mbaya sana ameondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa nichukue nafasi hii, nitoe pole kwa wale wote waliopatwa na maafa mbalimbali ya mafuriko, pamoja na kufiwa. Marehemu wote, nawaombea wapate mahali pema pa kupumzika. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nichukue nafasi hii, niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Kwimba, kwa ushirikiano ambao wamenipatia kwa miaka minne iliyopita katika kuleta maendeleo mbalimbali katika Jimbo la Kwimba. Bado tuna mwaka mmoja mbele, tutaendelea kushirikiana hivyo hivyo mpaka mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye hii Protokali; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti, wangu amemaliza kusoma maoni ya Kamati hapa hivi punde. Nilifikiri ni vema na mimi nikaongezea mengine ambayo labda hayakujitokeza katika Taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kitu ambacho hakihusiani moja kwa moja na hoja ya Mheshimiwa Waziri. Jina inaitwa ni *Protocol on Gender and Development* (Jinsia na Maendeleo). Mimi nilikuwa sioni tofauti sana, badala ya kuandika Jinsia na Maendeleo ingekuwa Wanawake na Maendeleo. Kwa sababu, ndani ya Protokali, ukisoma sana neno wanawake na wasichana limejitokeza mara 52, neno wanaume na wavulana limejitokeza mara 17 tu. Kwa hiyo, unapongea juu ya jinsia, mimi nilitegemea ingelinganalingana, lakini 52 kwa 17, hapo nadhani *gender* imeegemea upande mmoja. Hilo siyo tatizo kubwa sana, kwa sababu hata ukiupitia mkataba, utakachokikuta zaidi mle ndani ni haki za wanawake. Kwa hiyo, ile kusema Jinsia na Maendeleo bado nahisi kama kuna kitu fulani kilikuwa kimejificha tu mle ndani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali, kwa kuwa inatuletea sheria mbalimbali kuhusu haki za akina mama; ni jambo jema sana. Hapa tulipofika Watanzania, hata katika Protokali hii, utaona kwamba karibu mambo ni yale yale, itakuwa ni rahisi sana hata kupitia. Ninapenda nitumie nafasi hii vilevile kuipongeza Serikali kwa kuiona sehemu ya kifungu cha 20(2)(b). Haya ndiyo yanayojitokeza mara kwa mara ndani ya mkataba, endapo hautausoma vizuri, utakuta mambo ambayo hayaendi sawasawa na mila na desturi za nchi yetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, msipokuwa makini, mnaweza kujikuta mmepitisha mambo ambayo hayalingani na mila na desturi. Mimi ninaipongeza sana Serikali kwa kuwa makini katika kuupitia Mkataba huu na kufikia hatua hiyo. Ninaomba hata katika mikataba mingine itakayokuja baadaye, waendeleo kuwa makini namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninaomba nitumie nafasi hii, kuiomba Serikali kuwa leo tunapitisha Azimio, lakini utekelezaji wake utakuwa na maana zaidi kama sheria za nchi yetu zitalingana na haya ambayo tunayapitisha. Ningependa sasa niombe, baada ya kupitisha Azimio hili, Wizara izipitie tena sheria zote zinazomhusu mwanamke ili zinazohitaji kurekebisha zirekebisha mapema ili haki ya mwanamke tuifikie haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendeleo na kutoa tahadhari kidogo, labda nianze na tahadhari kwa wanaume wenzangu; tumekuwa tukipitisha sheria mbalimbali za haki mbalimbali, ni jambo jema sana na mimi ninakubaliana na jinsi ilivyokaa, kama makundi mbalimbali hayaelewani siyo rahisi sana kupata maendeleo.

Kwa hiyo, ni vema ingeandikwa Jinsia na Maendeleo, lakini sasa kila wakati linapokuja suala la wanawake ni vema tukawa waangalifu sana. Sasa hivi tunaongelea juu ya asilimia 50 kwa 50 na mimi naunga mkono sana hoja hii. Lakini tufike mahali tuishie asilimia 50 kwa 50. Wasiwasi wangu inaweza kufikia 52 kwa 48 ndiyo wasiwasi wangu huo tu. Tumeambiwa tusiogope, tusihofu lakini ni vema ile hofu ikaanza tukuingia pole pole. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu iko hivi; askari Magereza huwa anakwenda na wafungwa kufanya kazi nje, wanakaa pamoja vizuri kule baadaye anaweza kuzoweana sana na wafungwa akaanza kuwaona kama ni rafiki zake. Huyu Askari Magereza, wanaporudi kutoka mahali fulani kuingia gerezani, anatoa funguo kwa mfungwa halafu yeye anaingia ndani kwanza na wafungwa anawaacha nje; hivi akifika mle ndani wakamfungia akiwaambia nifungulieni watamfungulia? (*Makofi/Kicheko*)

Wanaume tunashabikia vizuri sana, hatimaye tutakapofika asilimia 52 kwa 48, wasiwasi wangu ni kwamba, jinsi ya kutoka mle itakuwa kazi kubwa sana. Hiyo ndiyo tahadhari, twende pamoja na wenzetu vizuri sana kwa uangalifu mkubwa sana. Tusije tukafika 60 kwa 40, jinsi ya kutoka mle itakuwa vigumu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Vile vile natoa tahadhari kwa akina mama, inapofika kwenye masuala ya haki zao, wanashabikia sana mpaka baadhi wanasahau kama wanaume wote ni watoto wao. Ninakumbuka tulipotunga sheria ya kujamiiana, mimi naamini waliofungwa zaidi ni wanaume zaidi kuliko wanawake na ni watoto wa akina mama na baadhi ya akina mama wengine watakuwa wanaumia sana kwamba, watoto wao wamefungwa kutokana na sheria hii. Kwa hiyo, tunapotunga sheria tuwe waangalifu sana; tushabikie sawa lakini vile vile tufahamu kwamba, bado tuna watoto wetu wa kiume ambao wanahitaji kulindwa na sheria hiyo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, maoni yetu yameshasemwa lakini nilifikiri ni vema nikaelezea kwamba, Protokali hii badala ya kusema ni *gender and development* ingeandikwa *Women and Development* haitakuwa na athari yoyote. Vile vile akina baba na akina mama kila mmoja achukue tahadhari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwa mchango wako.

Kabla hatujaendelea, nieleze kwa kifupi kwamba, Mheshimiwa Zainab Gama alikuwa ameniandikia kutaka Mwongozo wa Kiti na aliuliza kwamba; endapo Itifaki kama hii tunayojadili ina kipengele kinachopingana na sheria na mila zetu; je, tunaweza kupitisha Azimio hili *minus* hicho kifungu likapita Azimio zima lakini hicho kifungu ambacho kinapingana na mila na desturi zetu tukakiondoa?

Mwongozo ni kwamba, tayari viongozi wetu wamesharidhia kwa maana ya Serikali zetu, kuhusiana na Azimio hili. Kinachotakiwa Wabunge ni kuridhia Mkataba, ndio ombi ambalo Mheshimiwa Waziri amelileta hapa. Kwa hiyo, Bunge tuna uwezo wa kulipitisha lilivyo au kulikataa kama lilivyo, lakini hatuna mamlaka ya kuchomoa kitu kimoja ndani yake, ambacho hatukifurahii na tukasema tumepitisha Azimio lakini *minus* kifungu hiki hilo halikubaliki. Itakuwa vizuri, Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya ziada ili kuliweka vizuri zaidi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe maelezo mafupi kutokana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Zainab Gama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo ya Waziri na pia kwenye Azimio lenyewe, imetamkwa wazi kwamba, Mkataba wa Vienna unaruhusu kwamba, nchi inaweza kuridhia bila kuzingatia vipengele vyote; na kwa msingi huo, inaruhusiwa tu na niamwomba Mheshimiwa Gama asome Azimio tuliloligawa, linaelezea kwamba, tunaomba turidhie Itifiki hii bila kifungu namba 20(2)(a), ndiyo maana ya *domestication*. *Domestication* ni kwamba, unachukua Itifiki unaiweka katika mazingira yako. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unachotuambia ni kwamba, Azimio lililo mbele yetu sasa ambalo tunaendelea kulijadili na kuja kulipitisha baadaye; litapitishwa na Bunge bila kipengele hicho?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nirudie kama nilivyosema kwamba, ile *Vienna Convention*, naomba niisome kwa idhini yako: “Hivyo basi, kwa kuzingatia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Mikataba na Itifaki za Kimataifa (*Viena Convention on the Law of Treaties of 1980*) na kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya kuridhia Itifaki ya *SADC* kuhusu jinsia na maendeleo kwa Taifa letu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Pili, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kumi na Nane linaazimia kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Jinsia na Maendeleo ya Mwaka 2008, isipokuwa Tanzania isitekeleza masharti yaliyomo kwenye Ibara ya 20(2)(a), ambayo ndiyo inazungumzia suala la *emergency conception* ambayo kwa maana nyingine ni utoaji wa mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili limezingatiwa na *Vienna Convention* inaturuhusu kwamba, unaweza kuridhia kwa kuondoa kipengele usichokitaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tupate uzoefu wa Mheshimiwa Dkt. Mongella. Changia moja kwa moja mchango wako kuhusiana na suala hili halafu tutaendelea na wachangiaji wengine. Mwisho, baada ya ushauri mwingine ambao tutakuwa tumeupata, Kiti vile vile kitazingatia suala ambalo linaongelewa na Mheshimiwa Waziri.

MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru dakika usianze kuhesabu lakini mpaka nijibu lile lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosemwa katika mikataba labda niliseme kwa Kiingereza; una-*ratify with reservation*, yaani mkataba unabaki vilevile, lakini wewe unatoa *reservation*. Haina maana kwamba umechomoa, inabaki kama ilivyokubaliwa na Marais hawa lakini *with reservation* hiyo, mnatoa mnaweka hiyo *reservation*. Wakati tunaandaa Beijing, kifungu hiki kilitupa matatizo na tulikitoa katika *Beijing Platform* na hasa tukiwemo wengine ambao tuna *religious convection* kali kama mimi Mkatoliki safi, siwezi kuruhusu utoaji wa mimba na Waislam ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, ilifika mahali hatukutaka *document* yenye *reservation*.

Kwa hiyo, tukafanya *negotiation* hiki kifungu hakikuingia lakini kime-*sleep* kwa sababu jambo limekuwa likijitokeza mara kwa mara kuonesha ya kwamba, jamii fulani fulani zinahitaji sana kutoa mimba na hapa Tanzania wanatoa tu kila siku. Kwa hiyo, hata tukiki-*reserve*, watu wanatoa, tukubaliane hivyo; pamoja na kwamba watu wanaua lakini hatujaruhusu watu

kuchinjana eti tukasema mradi wamechinjana. Kwa hiyo, ni *reservation*; sijui kwa Kiswahili tungesemaje, ndio hiyo anayoieleza Waziri kwamba, turidhie mkataba na tusitekeleze kifungu cha 20(2)(a). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wanafamilia wa Hayati Mzee Rashid Kawawa, mimi familia hii nai-*define* kwa upana zaidi ya kwamba, siyo wale watoto aliowazaa tu, tupo wengi aliotulea katika siasa na wote tuko katika kundi hili. (*Makofi*)

Huyu mzee ndiyo waliofanya tuwe tulivyo leo, wasingejitolea kwa makini iwe ni walioko kwenye Upinzani ama Chama Tawala, tusingekuwa kama tulivyo leo. Kwa hiyo, tunahitaji tutambue mchango wa hawa waasisi ambao wengi sasa wanatoweka na sisi tuliobaki ni lazima tuwe makini kuifanya kazi ambayo waliianza ya kuleta heshima ya Taifa, ya kuleta uhuru wa nchi hii na kuleta maendeleo ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue nafasi hii, pamoja na kwamba, baadaye nitatoa maelezo ya Bunge kufuatana na Kanuni zetu, kuwapa pole sana Wananchi wa Wilaya ya Ukerewe, ambao kwa tukio baya sana la ukatili, la kuuwa wavuvi, kwa sababu tu wameuza samaki na wana pesa. Napenda kuwapa pole, nipo pamoja nao na nitaendelea kuhakikisha kwamba, wavuvi wote popote waliko Tanzania, wanalindwa kwa sababu wanaishi katika mazingira magumu, wakiwemo pia na wavuvi wa Kigoma na Ziwa Victoria, nadhani wana matatizo makubwa ya ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, katika Itifaki hii ambayo tunairidhia leo, ningependa tu niseme kwamba, nina mapendekezo yafuatayo:-

Tuweke baraza la kufuatilia masuala haya siyo Wizara, kwa sababu Wizara inajikita katika eneo ambalo limeainishwa lakini masuala ya wanawake ni masuala mtambuka, yanahusu Wizara zote. Kwa hiyo, liwepo baraza litakalosimamia utekelezaji. Ukiangalia katika Itifaki hii, kumeorodheshwa juhudi za kimataifa za kutaka kuondoa matatizo ambayo yanazungumziwa hapa na zimetajwa ni ndefu kweli; ukianzia na *commission on status of women, conversion on elimination of the violence against women and the charter of the child* na mambo mengi zaidi hata ya 20 lakini utekelezaji wake ndio tatizo.

Kwa hiyo, nataka nipendekeze ya kwamba, katika kuandika labda kanuni, vyovyote vile katika kutekeleza iwemo kuunda Baraza la Taifa. Pia iwepo kuunda Mabaraza ya Wilaya ili iwe kama tulivyounda Mabaraza ya Ardhi katika kila Wilaya kuwepo na Baraza linalosimamia utekelezaji huo. Tukifanya hivyo, tunaweza kwenda kwa haraka zaidi kwa kuzingatia ya kwamba, kila Wilaya zina mazingira yake tofauti kuhusu mambo ya usawa wa jinsia. Nataka niseme tu *point of order* hapa wanazungumza, kuna wilaya nyingine katika *role description* kuna wanaume ambao wanakwenda sokoni, ambapo kuna wilaya nyingine mwanamke ndio anakwenda sokoni, kwa hiyo ni tofauti hizo za usawa.

Kuna makabila nyingine mwanaume ndiyo anatafuta kuni kama watani zangu Wahaya. Mila zetu sisi Wakerewe, wanawake ndiyo wanatafuta kuni wakisaidiwa mara kwa mara kutegemeana na mapenzi ya mume na mke wake. Kazi ya kutafuta kuni ni ya wanawake na kazi

ya kuchota maji nayo inatofautiana, kwa hiyo ndio maana napendekeza kuwe na Mabaraza kama ilivyokuwa Mabaraza ya Ardhi ambayo yatasimamia utekelezaji baada ya kuridhia Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka nilizungumzie ni hali ya usalama wa mwanamke katika jamii; sasa hivi kila kukicha inaonekana ningezungumza kwa Kiingereza niseme, mwanamke sasa ni *endangered species* ambayo ipo katika hali hatarishi wakati wote kama vile yuko vitani. Maisha yake yako hatarini, kwa sababu ya kazi yake ya kujifungua. Maisha ya akinamama yako hatarini kwa sababu ni wanawake. Hili tukio la Rungwe lililotokea ambapo vitoto vidogo vya kike vimeuwawa kwa kubakwa ni jambo chafu na linatokea kila mahali hasa wakati wa vurugu mbalimbali ambazo hazina usalama na akinamama ndio wanaopata matatizo.

Kwa hiyo, suala la usalama kwa maisha ya wanawake limetajwa katika Itifaki hii, lakini halikutajwa kwa uwazi kama ninavyolitaja mimi; ni suala ambalo ni lazima tulitizame katika taifa letu. Kwa nini wanawake wafike mahali iwe ni *endangered species* ya kwamba, wakati wowote mwanamke anaishi kwa hofu ndani ya familia yake, ndani ya jamii yake na ndani ya taifa lake? Kwa hiyo, haya mambo tuyatilie mkazo sana. Katika kulizingatia hili, ningependa pia niseme mambo yafuatayo; tunapozungumzia usawa wa jinsia, mara nyingi watu wanachanganya na usawa wa mwanamke na mwanamume. Usawa wa jinsia kwa mfano hata wanaume wangeweza kulalamikia *research* za kansa, nyingi ni juu ya kansa za maziwa na kizazi.

Prostate cancer ambayo inawapata wanaume, haijafanyiwa utafiti wa kutosha. Hiyo ndiyo maana ya jinsia kwamba, mwanamke hatapata *prostate cancer*, lakini mwanaume ana haki ya *research* ya undani kuhusu masuala yanayomkabili kama mwanaume na mwanamke naye ana haki ya *research* na matibabu ya magonjwa ambayo yanampata tu kwa sababu ni mwanamke. Kwa hiyo, katika maana halisi, kuridhiwa kwa Itifaki hii kutasaidia kuendelea kufafanua mambo yatakayoleta uelewano baina ya wanawake na wanaume katika jamii ya kwamba, wote wana haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala lingine, katika kutekeleza Itifaki hii kutahitajika rasilimali. Tungepitisha bajeti zetu katika kioo cha jinsia; ni pesa kiasi gani tunazotoa hapa zinakwenda kwa wanaume, kuanzia pesa za *construction* kuendelea na pesa mbalimbali. Ukikokotoa utakuta ni kiasi kidogo sana kinachomfikia mwanamke na hii ndio tunaiita *gender budgeting*.

Kwa hiyo, baada ya kuridhia ni lazima tuweze kutumia utaratibu wa kupitisha bajeti katika kioo. Nitatoa mfano ambao ni mwepesi zaidi, ukienda kwenye shule zetu za sekondari, ambazo wasichana wengi wamevunja ungo, hakuna katika bajeti zetu mahali ambapo tumewawekea *facilities* za kutosheleza msichana asipoteze masomo yake. Kwa hiyo, uhesabu kila msichana aliyeko sekondari kwa mwezi anapoteza angalau siku tano haendi kwenye masomo; hakuna maji wala hakuna mahali ambapo mtu anaweza kufua nguo yake akaanika. (Makofi)

Kwa hiyo, mtoto huyu wa kike ingawa tumesema tumetoa usawa wa kuingia shule na kuingia darasani, lakini uhesabu siku tano hayuko darasani kila mwezi, ukiweka kwa mwezi mzima huyu binti hataweza kufikia alama ambazo wenzake wamekuwepo darasani muda wote.

Mimi ninayetoka kwenye visiwa, kuna shule watoto lazima wa-*commute* kwenye mtumbwi kwenda shule na wanapoteza na kwa sababu hili halijachambuliwa vizuri watu wanaliona ni jepesi. Kwa hiyo, mimi nasema mapendekezo yangu ni kwamba, kila mwaka tupitische bajeti zetu kwenye kioo cha jinsia, tuone jinsi zinavyoweza kutatua matatizo ya akinamama.

Tunakuja kwenye suala la uhai, kwa sababu Itifaki hii imeeleza wazi kwamba, uhai wa mwanamke na wa mwanaume lazima ulindwe. Ukiangalia haki za kuishi mwanamke zinakuwa finyu sana na hasa katika umri wa miaka ambayo yuko katika *process* za uzazi, wengi wanapoteza maisha, lakini hatujaiona kwamba ni haki mojawapo ambayo mwanamke anaipoteza. Haki ya kula, akinamama wengi vijijini wanaathirika sana kwa sababu wao ndio wanakula mwisho na wanakula kidogo wakati chakula ndani ya familia hakitoshi. Hhali hii inaathiri sana afya za akinamama na kutuelekeza katika kupoteza maisha. Siwezi kumalizia bila kusema hii suala la kufikia *fifty fifty*, siyo suala la ku-*negotiate*, tukishapitisha hii ni lazima utekelezaji uanze mara moja, kwa sababu hatuwezi tukaridhia halafu tukarudi nyuma tukapinga; kwa hiyo, *fifty fifty* ianze *immediately* baada ya kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwamba, kuridhiwa kwa mkataba huu kunahitaji Mabaraza yatakayosimamia kama tulivyosimamia na Mabaraza ya Ardh.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama ambavyo tumekuwa tukitoa pole kwa familia ya mzee wetu, Mheshimiwa Kawawa, basi kwa mara nyingine tena bado tunamkumbuka na kuzienzi kazi zake nyingi ambazo amekuwa akizifanya katika nchi yetu. Tunaungana na familia, kwa masikitiko makubwa kupoteza hazina ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kusema kwamba, naunga mkono Itifaki hii ya Masuala ya Jinsia na Maendeleo. Ninaunga mkono *reservation* ya kifungu cha 20(2), ambacho kimetolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri. Moja kwa moja nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Wanawake wa Tanzania, hususan wa Mkoa wangu wa Iringa, kwa kazi kubwa ambazo wamekuwa wakizifanya kila iitwapo leo.

Nakumbuka Baba wa Taifa aliwahi kusema kwamba, wakati akinababa wanafanyakazi, wakati mwingine saa nane hadi saa tisa kwa siku, wanawake ni kundi ambalo linafanya kazi saa zisizopungua 16 kila siku. Kwa hiyo, ni watu ambao wamekuwa wakijitoa sana. Pamoja na kujitoa huko, bado kundi hili ambalo katika nchi nyingi wapo asilimia 51 ya idadi ya watu, kwa mfano, Tanzania wanawake ni asilimia 51 ya watu milioni 40; kundi hili limekuwa likiachwa nyuma katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Kuachwa kwao nyuma, kumekuwa kukipewa vichwa vya habari vya aina mbalimbali. Tunasema *titles* mbalimbali, wakati mwingine wanawake wameachwa wakisema kwamba ni mila na desturi, wakati mwingine wanasema ni sheria, wakati mwingine wanasema ni kutokana na dini na sababu mbambali ambazo zimekuwa

zikihalalishwa kwamba, katika jambo hili wanawake yamkini hawastahili, kitu ambacho hakika kinapaswa kitafakariwe. (*Makofi*)

Pia naishukuru sana Wizara na Serikali, kwa kuridhia Itifaki hii, *Protocols na Conventions* nyingi ambazo imekuwa ikiridhia tangu miaka ya 1948, baada ya Vita Kuu ya Pili na mara baada ya Uhuru. Tunayo mikataba, kwa mfano, *Convention on Elimination of Discrimination Against Women, Beijing Declaration*, lakini haya yote pamoja na kuridhia, mpaka leo bado matunda hayajatosheleza. Ndiyo maana kila siku mara kuna *Maputo Protocol*, leo kuna *SADC Protocol* na kesho tutaletewa nyingine. Sasa kuridhia huku lazima kujidhihirishe katika utekelezaji.

Mimi nilikuwa ninajaribu kutafakari kwamba, mbona kila siku tunaridhia hiki na hiki lakini haki za wanawake bado hazijalingana kama ambavyo zinastahili? Kwa hiyo, ningeomba kusema kwamba, pamoja na mikakati mizuri ambayo Wizara imeahidi kuiweka, wakati mwingine Itifaki hizi ukiziangalia, upande wa *International Law* zimeandikwa mambo mazuri sana. Utafiti niliufanya mimi upande wa *women rights* ni kwamba, bila kuweka mikakati, yale mambo yaliyokuwa yameelezwa kwenye Itifaki hii, yakikiukwa huwezi kwenda mbele ya vyombo vya sheria ukasema kwamba, ibara fulani ya Itifaki ya *SADC* ya wanawake na maendeleo imekiukwa hivyo nimekuja kupata haki zangu. Kwa hiyo, hilo nalo ni jambo ambalo wataalam inabidi walitafakari sana.

Baada ya kuridhia bila kuweka mikakati, bila ya ku-*ratify*, bila kufanya *domestication* ya hii mikataba, bado nguvu yake inakuwa ni ndogo sana kutumika. Kwa hiyo, wakati mwingine tusipo-*domesticate* inakuwa inaleta shida. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, maadam ameahidi kwamba, mikakati itakuwepo basi izingatiwe.

Nikianza moja kwa moja na Ibara ya 4, inayozungumzia kuhusu haki za kikatiba (*Constitutional Right*), inaelezea kwamba, kutakuwepo na usawa wa jinsia; hivyo, ningeomba sana aina zote za sheria ambazo kweli zinambagua mwanamke katika nchi yetu, basi zifanyiwe marekebisha. Hadi leo bado tunazo mila na desturi ambazo hazimpi haki mwanamke ya kumiliki *property* kama ardhi na vitu mbalimbali, zipo haki za kimila.

Tunashukuru kwamba, Wizara na Serikali, imerekebisha ile Sheria ya Ardhi kwamba, sasa mwanamke anaweza aka-*posses*, aka-*transfer* na hata akauza ardhi sawa sawa na mwanaume; ile ni hatua kubwa sana ambayo imefanyika. Hizi sheria za kimila ambazo hazimpi haki mwanamke katika Nchi ya Tanzania, wanapokwenda mahakamani sheria hizi za kimila na sheria za kidini, zina nguvu sawa sawa na sheria tunazopitisha hapa Bungeni; zinatambulika.

Kwa hiyo, kutambulika kwa zile sheria za kimila na hasa pale zinapokuwa hazimpi haki sawasawa mwanamke, kwa kweli bado zinakuwa hazimtendei haki huyu mwanamke. Kwa hiyo, ipo haja ya ku-*review* na ku-*amend* sheria hizi mapema katika Bunge letu, tumekuwa tukiomba masuala haya yafanyike muda mrefu sana lakini bado.

Kwa mfano, Sheria ya Ndoa inayosema kwamba, mtoto chini ya umri wa miaka 18 hataruhusiwa kuolewa, Sheria ya Ndoa inasema kwamba, endapo akikubaliwa na baba yake (*with the consent of the father*), pale bado haimtambui mama na sheria inaendelea kusema kwamba, *in the absence of the father then mother* anaweza akaulizwa. Bado naona sheria hizi hazina usawa kabisa, kwa hiyo, ipo haja sheria hizi ziangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala zima ambalo linaendelea kidogokidogo katika nchi yetu; suala la malezi ya watoto. Kimsingi, suala la malezi ya watoto ni wajibu wa pande zote, yaani baba na mama, lakini maeneo mengi sana unakuta akinababa wanawaachia mzigo huu mkubwa wa malezi ya watoto akinamama. Ukienda maeneo ya vijijini, akinababa hawaonekani, akinamama ndiyo wanahakikisha chakula kipo, *uniform* imepatikana, basi ipo haja hakika ya kulisaidia sana kundi hili la wanawake ambao wana mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimenifurahisha zaidi katika Itifaki hii ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Wanawake na Maendeleo ni Ibara ya 10, kwa sababu *conventions* na *protocols* nyingi, mara nyingi tunaridhia lakini zinakuwa zimeundwa nchi za Marekani au Europe na hivyo mambo mengi ambayo yapo Europe hayapo Africa. Sasa kwa kuwa hii Itifaki ni ya Nchi za Kusini mwa Afrika, nimefurahi kuona kile kipengele kinachohusiana na wajane; kumbe ukienda Nchi za Marekani au Ulaya masuala ya wajane hayapo sana kwa sababu wao wana-*cover* ya masuala ya *insurance*. Sasa kipengele hiki katika Ibara ya 10 kinachoelezea haki za wajane, kwa kweli ni muhimu sana hawa wajane tukaangalia ni jinsi gani ya kuwasaidia.

Wajane wengi sana wamekuwa wanafukuzwa kwenye nyumba wakati baba anafariki. Wajane wengine wanatakiwa kurithiwa kutokana na mila na desturi na mambo mengine mengi sana ambayo yanafanyika ambayo ni kinyume kabisa. Hivyo, naomba sana taratibu mbalimbali ambazo zitakuwa zinazingatiwa hata katika Mahakama zetu, kundi hili la wajane na wagane kwa kweli ni kundi ambalo linapaswa lizingatiwe sana katika kutenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, lipo suala la ushirikishwaji katika vyombo vya maamuzi. Kwa kuwa katika idadi ya watu, wanawake na wanaume ni 50% kwa 50%, basi katika vyombo vya maamuzi na sheria zote za masuala ya uchaguzi, kundi hili muhimu la wanawake ni muhimu likazingatiwa.

Pia Vyama vya Siasa ni muhimu vikazingatia sana kwamba, masuala ya uongozi wa kisiasa katika nchi yetu, vinapitia katika Vyama vya Siasa, basi Vyama vya Siasa vifanye jitihada za makusudi. Sambamba na hilo, nikipongeze sana chama kinachotawala, kwa jitihada zake za kuwatambua sana wanawake ambao wamekuwa wakishirikishwa sana katika ngazi mbalimbali kama Ubunge, Udiwani na hata Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji, wamehakikisha kwamba, kunakuwepo na wanawake wasiopungua 30% na ni imani yangu kwamba, huu ni mwanzo tu, haraka na mapema sana tutafikia 50%.

Maeneo mengi sana tukiwa tunasema hebu tuwachague wanawake wanasema hawana sifa. Kwa hiyo, suala la elimu iwe ni jitihada ya moja kwa moja kwamba, wanawake hawa wapewe elimu, lakini si elimu tu, lipo suala la kuwawezesha kiuchumi. Benki nyingi katika nchi yetu bado riba zao ni kubwa na hivyo wanawake wanapokwenda kuhitaji kupata mikopo wanashindwa kwa sababu ya riba, kwa hiyo, wanaopata mikopo wanakuwa ni wanaume tu. Ipo

haja na niishukuru sana Wizara, kuna Benki ya Wanawake lakini jitihada hizo tuendeleo nazo kwa sababu mwanamke akiwa *economic empowered* anaweza aka-*negotiate*, anaweza aka-*bargain*, lakini akiwa *economically weak*, ataambukizwa UKIMWI, atapata matatizo mengi na yeye atakuwa ni mtu wa kupokea *orders* na hapo inakuwa ni *slave master relationship*, lakini mwanamke akiwa *strong* mambo yote mwanaweza mkajadiliana kwa fursa sawa.

Kwa hiyo, nilidhani ipo haja kabisa ya kuweka sera kwamba, haya mabenki yaangalie sana, zinapokuja *institutions* na mashirika kukopa kwa ajili ya kufanya biashara ni sawa, lakini hapa anakuja mwanamke kuhitaji mkopo wa kutunza familia yake au jamii, basi tuangalie jinsi ya kuwawezesha maana mwanamke akiwezeshwa anaweza na ukimuwezeshwa mwanamke umeliwezeshwa Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake wengi wamejikita kwenye masuala ya kilimo, wafanyakazi wengi katika ofisi wana *pension* na wana likizo, lakini 80% ya Wanawake wa Tanzania wako katika kilimo, wanawake hawa hawana likizo wala *pension*; kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia sana kundi hili kubwa la wanawake kwamba, tunaweka mikakati gani kwa ajili ya kuwasaidia, kama itawezekana kuweka *insurance cover* au chochote ili wanawake hawa wawe na nguvu ya kuendelea kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine muhimu ni kile cha 26, ambacho Itifaki inasema tutapunguza vifo vya wanawake wajawazito kwa *ratio* ya 75 ifikapo mwaka 2015. Nilishasema kabla kwamba, wakati wa kupunguza vifo vya wanawake umekwisha na sasa ni wakati wa kuondosha vifo vya wanawake na ningetamani sana hata hiki kifungu tukirekebishe kiwe *reserved*. Sisi Tanzania tukubaliane kwamba, siyo kupunguza vifo vya wanawake, bali kuondosha kwa maana leo hii mwanamke yeyote akiwa mjamzito, mguu mmoja uko kaburini na mwingine uko ardhini; akijifungua salama ule wa kaburini unatoka unakuja ardhini, akifariki wakati wa kujifungua maana yake ule ambao uko ardhini umetoka umeingia kaburini. Wanasema *every pregnant woman, one leg is on the grave*. Sasa hili ni jambo la kusikitisha sana, tunapoteza wanawake wa aina mbalimbali; wakulima, wafanyakazi, wasomi na kadhalika, unasikia amefariki wakati wa kujifungua *oxygen* haikuwepo, *diabetic* hatuku-*check*, *sugar* ilipanda, kwa hiyo, kumekuwa na sababu nyingi sana.

Tunaposema kupunguza ifikie labda 75%, tutakapofikia na kuridhia kwamba wengine waendeleo kufariki hata kama ni watano au kumi, tutasema tume-*meet objectives* zetu, tutasema *well done* na tutapena mikono kwamba tumefikia malengo ya *Millennium Goals* na MKUKUTA, kumbe hapo tumebariki watu wengine wafariki. Kwa hiyo, kwa maoni yangu, hili suala la kupunguza vifo sasa wakati umefika hatutapunguza bali tutaondosha na mwanamke yeyote mjamzito anapofariki, anapotoa uhai kwa kiumbe, lazima tutazamane imekuwaje? *No mother should die when giving birth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine ni juu ya usimamizi wa Itifaki hii kwamba, tuiangalie lakini wataalamu wa masuala ya *international* ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana, kwa mchango wako. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mungai.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya mzee wetu, Muasisi wetu wa Chama cha Mapinduzi na Kiongozi wa Taifa letu la Tanzania, Marehemu Mzee Kawawa. Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Azimio hili la Itifaki ya Jinsia na Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichukue tena nafasi hii, nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete; baada ya kukutana na Wakuu wa Nchi za Afrika Kusini kuangalia masuala ya jinsia na maendeleo, moja kwa moja huwa anafika kwenye nchi yake (Tanzania) na kufanya utekelezaji kamili. Naomba kwa hili, nichukue nafasi kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wetu kwa sababu ameonesha nia njema kabisa, maamuzi anayoyatoa akiwa na viongozi wenzake, anakuja kwenye nchi yake anaangalia Katiba yake na anarekebisha mara moja kama ilivyo kwenye Katiba kwamba, mara ya mwisho walikubaliana kwamba asilimia ya wanawake katika maamuzi iwe 30% na yeye alitekeleza. *(Makofi)*

Tumekuwa tukijijonea anapofanya uteuzi, kama nafasi ni nne basi mbili wanawake na mbili wanaume. Kwa hiyo, hili analizingatia, naomba nimwombe aendelee na moyo huo wa kuhakikisha kwamba, suala hili la jinsia na maendeleo analitekeleza kule tunakoeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na maoni ya Kamati, ambayo tayari yametupa mwongozo wa kuzungumzia Azimio hili. Kweli kwenye Katiba kuna maneno ambayo yalisahaulika tu, lakini kwa kuwa leo sasa Azimio hili tunalipitisha rasmi ndani ya Bunge letu na hayo marekebisho ndani ya Katiba ya kurudisha yale maneno mara kwa mara yatazingatiwa, nina uhakika kabisa kwamba, Bunge ni hili na Waziri ni huyu na ambaye anaonesha nia njema kabisa ya kusimamia jinsia na maendeleo, atalileta ili tuweze kurebisha na kurudisha maneno ambayo yalisahaulika kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Azimio hili liweze kutekelezeka, ninaungana na maoni ya Kamati ya kusema elimu tuipeleke kwa wanaume. Tunapozungumzia jinsia, wengi wanasema tunazungumzia masuala ya wanawake tu, lakini unapozungumzia jinsia ni pande zote mbili. Akinamama wengi hawaelewi, lakini ili yatekelezeka haya ni lazima akinababa tushirikiane katika kulisemea hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ikitolewa kwa akinababa, basi kwetu akinamama itakuwa rahisi sana kuhakikisha kwamba, maeneo mengi yanawadhhalilisha akinamama kwa

mfano tunapozungumzia kwamba, tuongeze viti vingi vya uongozi katika Ubunge au Udiwani, kama hatuwezi kulizungumza katika jamii, kama hatuwezi kuzungumzia mila potofu ambazo kwenye jamii bado zipo ya kwamba, mwanamke anapochukua *form* kwa mfano anapotaka kugombea jimbo ndiyo pale tabia mbaya za mwanamke zinaanza kuchambuliwa. Kama tutaielimisha jamii kwamba, mwanamke anaweza kama wanavyoweza wanaume, kwa hiyo, mwanamke anaweza kuchukua nafasi yoyote ile ya kuongoza taifa lake kama wanaume.

Kwa hiyo, kama elimu itafika kwa akinababa, tutasaidiana sana ili kuhakikisha kwamba, akinamama basi nao hawadhaliliki kwa maneno mabaya ambayo yanatumika kama mtu akijitokeza kugombea tunaambiwa wewe malaya, mlevi, huwezi na kadhalika, lakini akinamama tunaweza, nafasi tunayo, hatuombi upendeleo, elimu tunayo ya kutosha kabisa, kwa hiyo, ninaomba hili lizingatiwe baada ya kupitisha hili Azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninaomba elimu itolewe zaidi ili tupate nafasi zaidi ya elimu katika kuhakikisha watoto wa kike wanasomeshwa shule, tusije kupata kikwazo kwamba, akinamama hawajasoma. Watoto wetu wa kike sasa hivi tunawahimiza wasome hasa masomo ya sayansi, nafasi ziongezeke na uwezo huo wanao. Kwa hiyo, ninaomba baada ya kupitisha Azimio hili, huko mashuleni nafasi za watoto wa kike ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa sisi Tanzania tusiridhie Ibara ya 20(2)(a) ya Azimio, lakini bado naomba baada ya kuliweka pembeni Azimio hili, tuangalie sheria ambayo inasababisha mama anapigwa mpaka mimba inatoka, mwaname anamwona mke wake ana mimba lakini kipigo atakachokipata mpaka mimba inatoka. Sasa tutafute sheria ni nani aliyesababisha hiyo mimba itoke ili na yeye aadhibiwe, tusijiingize katika matatizo haya ya kuhakikisha kwamba mtoto anakosa haki yake ya kuzaliwa, aliyetenda hilo kosa aweze kuhukumiwa.

Nakubaliana kabisa na nchi yetu ikatae kuridhia ibara hiyo kwa sababu kwanza kidini hata kimila, kutoa mimba ni kitendo kibaya na cha kuua motto, lakini lazima tuangalie basi tunamlindaje hata huyu mama ambaye anasababishiwa kutoka kwa mimba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine kwenye mambo ya uongozi wa akinamama; nimesema kwamba, tunaweza tujaribu sasa, hata kwenye Vyama vya Upinzani wenzangu wameshalizungumza, tunaongezaje idadi ya wanawake katika kuhakikisha wanawawakilisha wanawake wenzao ndani ya Bunge, ndani ya Halmashauri zetu na ndani ya Serikali yetu. Basi niungane na wenzangu kuomba vyama vya wenzetu bahati nzuri Chama cha Mapinduzi chenyewe tayari kimeshaiweka kwenye Ilani yake, basi tuombe na vyama vingine vilizungumze hili ili tuweze kuongeza idadi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo linasumbua kidogo kichwani kwangu, ili kujali afya ya akinamama kuna tatizo limejitokeza juzi lakini naona Serikali haijalizungumzia; kuna *towels* ambazo tunatumia akinamama kila mwezi, zimetangazwa na vyombo vya habari kwamba ni feki na zinatumiwa katika hali ambayo mnaelewa kabisa kwamba, akinamama kila

mwezi wanazitumia. Serikali mmekaa kimya, akinamama wengi wanatumia hivi vifaa, naomba wakati wa ku-*wind up* hili Azimio, Serikali itoe tamko kwamba inasemaje na mwanamke atakapoathirika kwa kutumia hivi vitu ambavyo si halali atasaidiwa na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mwaka unaokuja, bajeti za Wizara zote zizingatie jinsia zote ili tunapopitisha bajeti hapa tuzingatie kwamba, kila Wizara inakuja na Mkakati Maalum wa kuhakikisha kwamba, jinsia zote zimezingatiwa. Tumwombe Rais wetu aendelee kuiimarisha nchi hii.

Naliunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Joseph Mungai, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. JOSEPH J. MUNGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ninaomba niseme tangu mwanzo kwamba, naunga mkono kwa dhati kabisa Azimio hili liweze kupitishwa ili turidhie hii Itifaki. (*Makofi*)

Sababu yangu kubwa ya kuunga mkono ni kwa sababu yaliyo katika Itifaki hii, tayari yamo katika Katiba yetu. Nina uhakika kabisa kwamba, yamo katika Katiba, kwa sababu nilikuwa Mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba lililopitisha Katiba hii mnamo mwaka 1977 na kazi hiyo katika Bunge lile Maalum tuliifanya kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania kama ilivyoandikwa kwa usahihi kabisa na kama inavyoweza kusomeka na yeyote anayetaka kusoma katika sehemu ya tatu ya Katiba yetu inayohusu haki ya usawa. Kwa kuwa suala la usawa lipo pia katika mjadala unaoendelea hapa wa vipindi vya Bunge na vipindi vya Viti Maalum, ninapenda katika kuunga mkono Azimio hili tulipitishwe. (*Makofi*)

Nanukuu vifungu muhimu kutoka kwenye Katiba. Ibara ya 13(2) ya Katiba yetu inasema kama ifuatavyo na kwa ruhusa yako naomba ninukuu: “Ni marufuku kwa Sheria yoyote iliyotungwa na Mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano, kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.”

Ibara ndogo ya (4) inaendelea kusema na ninanukuu: “Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa.” Hii inamaanisha mwanamke haruhusiwi kubaguliwa, Mbunge aliyekaa vipindi vitatu haruhusiwi kubaguliwa na mwanamke aliyekaa vipindi viwili Viti Maalum haruhusiwi kubaguliwa. (*Makofi*)

Ibara ndogo ya (4) inaendelea kusema: “... kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya Sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi, ni marufuku popote mtu yeyote kumbagua mtu mwingine.”

Pia katika Ibara ndogo ya (5), Katiba yetu inaendelea kufafanua maana ya neno ubaguzi na inasomeka kama ifuatavyo: “Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara hii neno “kubagua” maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali, kwa kuzingatia utaiifa wao, kabila, pahala walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsia, hali

yao ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni au kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya mashart au sifa za lazima, isipokuwa neno kubagua halitafafanuliwa kwa namna ambayo itaizua Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahususi katika jamii.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa nivinukuu vipengele hivyo, kwa sababu katika mijadala inayoendelea hasa baadhi ya waandishi wa habari, wanaandika maoni yanayotolewa na watu, lakini hawafanyi *reference* kwenye Katiba. Ninawashauri sana wafanye marejeo kwenye sehemu hii ya Katiba, utakuta kwamba hakuna sababu yoyote ya kupoteza muda kuzungumza vipindi vya ukomo kwa Wabunge wala vipindi vya ukomo kwa Wajumbe wa Bunge hili kutokana na Viti Maalum, kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume cha vifungu hivyo vya Katiba ambavyo nimevinukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimevutiwa sana na yaliyosemwa katika Ibara ya 14 ya Itifaki inayohusu *Gender Equality in Education*, yaani kwa lugha ya kutafsiri ili lieleweke haraka, kifungu hiki au ibara hii, inazungumzia usawa wa wanawake na wanaume katika elimu. Sisi hapa Tanzania tukisoma Sheria zetu na tukiiangalia Katiba yetu, hatuna ubaguzi katika elimu, ndiyo maana nimesema naunga mkono, kwa sababu yanayosemwa katika Itifaki hii, katika Sheria zetu na katika Katiba yetu, tayari yamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika suala hili la Elimu, pamoja na kwamba Tanzania hatuna ubaguzi kisheria, wataalamu wa Sheria wanasema *dejure*, lakini kiukweli *defacto* tuna ubaguzi katika elimu. Kwa hiyo, kipengele hiki cha Itifaki ninapenda kukitazama kwa sura hiyo.

Tukiangalia elimu ya msingi, tukitazama takwimu na Mheshimiwa Waziri ambaye ameleta Azimio hili amewahi kuwa Waziri wa Elimu kama mimi; katika elimu ya msingi, darasa la kwanza mpaka la saba, utakuta wasichana wanakuwa wengi kuliko wavulana; ukienda kidato cha kwanza mpaka cha nne wanakuwa karibu sawa; lakini ukienda kidato cha tano mpaka cha sita wavulana wanakuwa wengi kuliko wasichana. Kwa hiyo, unaweza ukasema katika utoaji wa elimu ya kidato cha tano na sita kuna ubaguzi ingawa kisheria hairuhusiwi kufanya ubaguzi, lakini kiukweli pana ubaguzi pale kwa sababu wanaopata elimu ya kidato cha sita wavulana ni wengi zaidi na ukienda chuo kikuu wanaume ni wengi zaidi. Sikuandaa takwimu, lakini anayetaka kuziona anaweza kuziona katika vitabu vya elimu. Kwa hiyo, kiukweli tuna ubaguzi katika ngazi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika masuala ya elimu na takwimu za elimu, tofauti ya kielimu kati ya Nchi za Afrika na Nchi za Ulaya, Ulaya wasichana ni wengi kuliko wavulana katika ngazi zote za elimu; *Primary*, *Secondary* mpaka Chuo Kikuu na Ulaya wasichana wanafaulu vizuri zaidi katika ngazi zote za elimu kuliko wavulana, hata chuo kikuu wanawake wanafaulu vizuri zaidi kuliko wavulana. Afrika ni tofauti; hapa kwetu ukitazama takwimu za elimu, wasichana wanafaulu zaidi ya wavulana katika mitihani ya darasa la kwanza na hata katika mitihani wa kitaifa ya darasa la nne. Baada ya hapo, wavulana wanafaulu zaidi, kwa hiyo, inaonekana wazi kwamba, katika safari ya elimu kuna mahali ambapo wanawake wanaharibikiwa na ni mara tu baada ya kufika darasa la nne wanaanza kupata matatizo.

Kwa maoni yangu ni vizuri tuijue *root cause*, yaani tuijue sababu sahihi ya wanawake katika safari ya elimu kuharibikiwa njiani na kwa maoni yangu inatokana na kuchelewa kuanza shule.

Kwa hiyo, kwa maoni yangu usawa sahihi kati ya wanawake na wanaume ni lazima utokane na usawa katika ngazi zote za elimu. Kwa hiyo, ni muhimu kabisa tufikirie na tufanye uamuzi kurekebisha utoaji wa elimu kwamba, rika sahihi la elimu ya msingi si miaka 7 mpaka 13, kama ilivyo katika Sheria yetu na katika utekelezaji wetu wa elimu. Rika sahihi la elimu ya msingi ni miaka 5 mpaka 11, kama wanavyofanya Ulaya na Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kule Mufindi tumekwishaanza kurekebisha, tumetumia Azimio la Halmashauri, kuanzia mwaka jana tunaandikisha darasa la kwanza wasichana wa miaka 6 na kuanzia mwaka huu kwa Azimio la Halmashauri yetu, tunaandikisha wavulana wa miaka 6 kuanza darasa la kwanza, na kuanzia mwaka 2011 tutapeleka miaka 5. Tumeamua kufanya hivyo kwa sababu tofauti na zamani, Baba wa Taifa alituachia shule ya msingi katika kila kijiji, kwa hiyo, hatuna sababu kuchelewesha mtoto kuanza shule mpaka afike miaka 7.

Matokeo ya uamuzi huu ambao sisi tumekwishaanza kuutekeleza ni kwamba, tutarudisha elimu ya msingi kwenda miaka 5 mpaka 11 na kwa kufanya hivyo, tatizo la mimba katika shule za msingi tutaondokana nalo kabisa. Kwa vile wasichana watakuwa wameanza mapema, makundi yote mawili, yaani wasichana na wavulana, haitatokea wakiwa *primary* wavulana kubadilika sauti kuwa kubwakubwa na wasichana kukua kimaumbile. Kwa hiyo, watapata elimu ya msingi iliyo kamilifu makundi yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narudia kusema kwamba, yote yanayopendekezwa kwenye Itifaki hii, tunayo kwenye Katiba, lakini inatukumbusha kwamba, tusiwe tu na usawa wa kisheria ni mzuri, pia tuwe na usawa wa kiukweli kati ya wanawake na wanaume wa nchi pamoja na nchi nyingine zote duniani, utapatikana pale tu ambapo kuna usawa katika elimu ngazi zote za elimu; *primary*, *secondary* na chuo kikuu.

Hii ya kupeana usawa kwa upendeleo, tuchukulie tu kwamba, ni wakati wa mpito lakini tuzingatie kufanya utafiti, tuchukue hatua zilizo sawa kwa kuzingatia usawa katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maneno hayo na kwa maelezo hayo, ninaunga mkono Azimio la Itifaki hii. Ahsante kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Azimio lililopo mbele yetu. Awali ya yote, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa kuweza kuuona mwaka mpya wa 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na Wabunge wenzangu, kutoa salamu za pole kwa Familia ya Mzee wetu, pamoja na Watanzania wote, kwa msiba mzito uliotupata kwa kuondokewa na Jemadali wetu wa Vita, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wataalam wake, kwa kuweza kulileta Azimio hili muhimu sana hapa Bungeni kuhusiana na kuridhia Itifaki ya SADC ya Jinsia na Maendeleo ya Mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye mchango wangu, masuala yote yaliyoko kwenye Azimio hili ni muhimu na mazuri ila mimi nitachangia kwenye vifungu kadhaa vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na ibara ya saba; Itifaki hii inazungumzia suala la haki za kisheria za mwanamke. Kwa upande wa Tanzania, imekuwa ni tatizo kubwa sana; wanawake wengi sana wamekuwa wakikosa haki zao za kisheria, kwa sababu ya kutokujua wapi waitafute haki yao. Lingine ni kutokujua Sheria na kukosa uwezo wa kufuatilia masuala ya kisheria ili waweze kupata haki zao. Hili limekuwa ni tatizo sana, ipo mifano hai mbalimbali na yapo matukio ambayo yametokea kudhihirisha ni kwa jinsi gani ambavyo Watanzania wengi akinamama wanakosa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linapokuja suala la umiliki wa mali, suala la mirathi au suala la baba na mama wameachana mwanaume kaamua kuo a mwanamke mwingine, mwanamke kupata haki yake inakuwa ni tatizo kubwa sana. Unakuta mwanaume ameamua kuo a, mwanamke aliyemwacha akiwa kule kwenye nyumba ndogo ya pili, anaamua kuuza kinyemela nyumba ile aliyomwachia mwanamke wa kwanza na watoto. Tumeona hata kwenye televisheni jinsi ambavyo masuala yanatokea, unakuta mwanamke anaanza kuhangaika, anashangaa nyumba inapigwa mnada akiwa ndani na watoto; ni tatizo kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni masuala ambayo yanafanywa kutokana na kwamba, hakuna Sheria ambayo inamlinda mwanamke na hakuna mikakati maalum ya kuweza kuhakikisha kwamba, haki za mwanamke zinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kuvipongeza vyombo vya habari kwa sababu vimekuwa vinaibua masuala haya kwa maeneo makubwa sana ambayo yako *very interior*, vijijini kabisa, lakini vyombo vya habari vinafuatilia, vimeibua na kutokea pale angalau hatua zinachukuliwa. Kwa hiyo, navipongeza sana vyombo vya habari na naviomba viendeele na moyo huo huo, kwa ajili ya kuwasaidia akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nazipongeza sana NGOs zinazofanya kazi kubwa ya kutoa msaada wa kisheria kwa akina mama. Zipo NGOs ambazo zinajitolea tena bure kabisa kuwasaidia akinamama ambao wamekosa uwezo kisheria ili waweze kupata haki zao kama TAMWA, TAWLA na kadhalika. Ninawapongeza sana na tunaomba pia waendeele na moyo huohuo na NGOs nyingine pia zijitokeze kwa ajili ya kutambua kwamba, nafasi ya mwanamke katika jamii ni kubwa na hivyo kuweza kuwasaidia kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kuna umuhimu wa Serikali kutunga Sheria na kuweka taratibu ambazo zitalinda haki za mwanamke, siyo kusubiri mpaka tuone *media* imeibua au tuone NGOs zinahusika kuwahudumia akinamama ambao wamekosa haki zao; uwepo utaratibu kamili kwamba, mwanaume anapoamua kuoa, ameacha nyumba na watoto nini kifanyike asijiamulie tu kwa sababu ameamua kuoa na ana mamlaka hayo basi anaamua kumtelekeza mama na watoto na anauza nyumba, basi mama aanze kutangatanga mitaani, hapana. Iwepo Sheria na taratibu za kuweza kumlinda mama kama huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu haki za wajane. Tumeona matukio mengi, tena haya ni masuala ya kusikitisha sana. Haki za wajane na wagane; inapotokea baba amefariki, mama ndiye anayenyanyasika, inapotokea mama amefariki hatuwezi kuyaona matatizo kwa akina baba. Kwa hiyo, tunaona kuwa ni udhalilishaji wa mwanamke; kwa nini anapofariki mama, baba asipate tatizo lakini baba anapofariki mama ndiyo anayenyanyasika?

Kwa hiyo, hakuna haki ya mwanamke pale mwanaume anapofariki, inakuwa ni tatizo sana; ndugu wanaona wakati wakiwa hai walikuwa wanachuma mali zao kwa pamoja, kwa shida na raha, kwa matatizo ya aina zote, lakini anapofariki baba, ndugu wanaona kuwa mwanamke huyu hana haki ya mali hii tena; kwa hiyo, inakuwa ni unyanyasaji wa hali ya juu. Saa nyingine inafikia hatua wanawake wengine wanapata matatizo mbalimbali ya moyo mpaka wanapoteza maisha kutokana na kunyanyasika kwa hali ya juu, wanaona kwamba, siyo binadamu wanaostahili kumiliki mali halali ambazo wameachiwa na mume zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Sheria ya Ndoa itakapokuja hapa Bungeni, iainishe wazi pale mwanaume anapofariki haki za mama na watoto zinakuwaje; na nani anazisimamia? Kusiwepo kuzungushana, pasiwepo na mwanamke kunyanyasika, naomba sana Serikali ilizingatie hilo, hatutaki akina mama wanyanyasike, haki zao za msingi zitambulike, waweze kupata haki zao wanazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la uwakilishi katika nafasi mbalimbali. Sisi Wanawake tunaweza, tena tunaweza sana tukipewa nafasi na hili limetambulika na limeshahiriwa kwa wale akinamama wachache ambao wamepewa nafasi maeneo mbalimbali; kuna Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakurugenzi, wanafanya kazi nzuri inayodhihirika na Watanzania wanaikubali, japokuwa upungufu upo kwa baadhi ya wachache, lakini *majority* wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, tunaomba sana kuwepo Mkakati Maalum wa kuhakikisha kwamba, akinamama wanapewa nafasi za kutosha kwenye ngazi mbalimbali za uwakilishi na ngazi za kutoa maamuzi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na historia ya nchi yetu na kutokana na utamaduni wetu, huko nyuma akinamama tuliachwa, kwa hiyo, hata nafasi za elimu kidogo tulikuwa tumewekwa pembeni. Zipo pia tamaduni na mila nyingine ambazo makabila mengine yanasema; mimi siwezi kumilikiwa au kutawaliwa au kuongozwa na mwanamke, sasa taratibu kama hizo ndiyo zinazorudisha nyuma juhudi za mwanamke kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatokea mpaka sasa hivi, mwanamama anaposimama kwenye nafasi yoyote aidha kugombea Ubunge au Udiwani, mtu wa kwanza kumponda ni mwanamke mwenzie kutokana na kwamba, kuanzia nyuma ni historia ambayo inajirudia. Kwa hiyo, tunaomba ili kuondoa hizi hisia zilizokuwepo na tamaduni ambazo zimepitwa na wakati, ambazo hazitakiwi kuendelea kuwepo, Serikali itoe elimu katika ngazi zote, kuanzia kwa akinababa na akinamama wa ngazi mbalimbali halafu akijitokeza mwanamke kutafuta nafasi yoyote ya kugombea au kuongoza aungwe mkono na Serikali ioneshe nguvu yake kwa yule mama ambaye amejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Siasa navyo vishiriki kikamilifu katika kuwateua akinamama kusimama kwenye nafasi mbalimbali na viwasaidie kwa hali na mali ili waweze kufanikiwa katika nafasi wanazogombea na hivyo kuhakikisha kwamba, ile asilimia hamsini kwa hamsini (50/50) inafikiwa ifikapo mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni nafasi ya mwanamke katika kuongeza Pato la Uchumi wa Taifa. Naungana na Mheshimiwa Pindi Chana aliyesema kwamba, asilimia themanini ya kazi za familia nyumbani zinafanywa na akinamama. Akinamama ndiyo wakulima, ndiyo wa kuangalia familia, ndiyo wanaofanya usafi wa nyumba, ndiyo wanaofanya kazi zote lakini ukijaribu kuangalia ni jinsi gani hizi kazi zinapimwa, utakuta kwamba, hakuna kipimo maalum; kwa hiyo, mwanamke anayeonekana kwamba anafanya kazi ni yule ambaye anakwenda ofisini; Mkurugenzi au nani. Serikali sasa ije na utaratibu wa kutathmini na kutambua mchango wa akinamama wanaoangalia familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke akizembea nyumbani, ndiyo maana tunasema kwamba, ukimuelimisha mwanamama umelielimisha taifa. Mwanamke akizembea nyumbani, familia inakwenda mrama. Mwanamke asipokuwa *strong* nyumbani, tabia za watoto zitabadilika. Hiyo ni kuonesha jinsi gani mama alivyokuwa na nafasi kubwa katika familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, sasa hivi ni muhimu kazi yoyote anayofanya mwanamke lazima itambuliwe na itathminiwe. Alizungumza mwenzangu kwamba, wengine kuna marupurupu wanayopata mfano viinua mgongo, hawa wa nyumbani hawana, lakini michango yao tunaitambua. Tunafanya nini ili na wao waweze kujiona kwamba, wanachangia kwenye Pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kilimo, asilimia kubwa ya mazao yanayopatikana ni mchango wa akinamama; siyo kwamba akinababa hawafanyi kazi, wanafanya lakini akinamama ndiyo wanaoongoza; kama mama ukilala basi ujue na baba naye atalala. Kwa hiyo, naomba sana michango ya akinamama nayo iwe inatambuliwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala linahusiana na utoaji wa mimba. Naungana na Wabunge wenzangu waliochangia kwamba, ninapinga kabisa suala la utoaji mimba na ninashukuru kwamba, Sheria za Ndani ya nchi yetu zinakataza hilo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali isimamie Sheria za Ndani ambazo zinakidhi mahitaji ya Watanzania.

Suala la utoaji mamba linakatazwa na mila, tamaduni na imani zetu. Tunajua kwamba, mtoto anaitwa mtu kuanzia siku mimba ilipotungwa, kwa hiyo, wawili wanavyoshiriki kwa ajili ya kutunga mamba; baba na mama wahakikishe wanaitunza ile mamba. Likitokea tatizo la

kiafya, basi tuwaachie madaktari waone jinsi gani ya kuokoa, lakini sisi kama nchi tusijiingize kwa kuweka Sheria kama hiyo. Vinginevyo, tutatoa mwanya kwa watu waanze kufanya vitu vya ajabu; wanaume watawapachika watoto wa kike mimba wakijua kwamba, watawachika na kuchomoa.

Kwa hiyo, tunaomba sana kwamba, tuendeleo ku-*stick* kwenye Sheria zetu, kikubwa ni kwamba, linapotokea tatizo tunafahamu suala la utabibu au madaktari litafanya kazi kuhakikisha kwamba, wanaokoa ama mtoto au mama kwa jinsi watakavyoona; lakini sisi bado tunasisitiza kwamba, hatukubaliani na kifungu hiki cha 20(2)(a) na kwamba, Sheria zetu za ndani ziendeleo kushika mkondo wake. Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ahsante sana na hapo ndiyo mwisho wa uchangiaji wetu jioni ya leo. Uchangiaji utaendelea kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali na tumepata fursa ya kuwasikiliza wachangiaji sita na maombi yameongezeka hapa ninao kumi na moja zaidi; sina hakika kama wote watakata nafasi kesho, lakini tutaanza na Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Juma Killimbah na wengine watafuata.

Waheshimiwa Wabunge, Mzee Nelson Mandela, anakumbukwa sana kwa maneno aliyoyasema miaka ile ya 1960 kabla hajafungwa, wakati ule wanapigana dhidi ya ubaguzi wa rangi alisema; anauchukia sana ubaguzi wa rangi wa weupe kuwabagua weusi, kama anavyochukia sana ubaguzi wa weusi wa kuwabagua weupe; imemfanya ameheshimika dunia nzima. Leo tuna Mkataba wa Jinsia hapa; ni vizuri katika mambo haya tukajitahidi kutombagua mama kama ambavyo tunapaswa kutombagua baba, tutakuwa tumejenga msingi mzuri sana kwa taifa letu, watoto wetu, wajukuu zetu na kadhalika. (*Makofi*)

Mwisho, Makatibu Mezani ni vizuri mfuatilie suala hili kesho asubuhi liwekwe vizuri kusudi Mwenyekiti atakayehoji hapa kuhusu Azimio hili basi ni vizuri akahoji ikawekwa na ile isipokuwa Ibara ya 20(2)(a) ili Bunge liwe limepitisha hili azimio na ile isipokuwa kiwepo pale pale ili Wabunge wanaposema “ndiyo” au “hapana” ieleweke ile *message* iende kabisa kwamba, wanapitisha isipokuwa Ibra ya 20(2)(a). (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli za leo na muda wetu hauruhusu kuendelea na shughuli nyingine. shughuli zilizopangwa leo Mezani zimekamalika zote, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1. 43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 3 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)